

# **Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA KUMI NA SITA**

**Kikao cha Kumi na Tano – Tarehe 27 Juni, 2009**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatuh Asubuhi)*

## **D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Zubeir Ali Maulid) Alisoma Dua*

## **HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

## **WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA NA MUUNGANO):-**

Randama za Ofisi ya Makamu wa Rais, (Mazingira na Muungano) kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

## **HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2009/2010  
Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge jana wakati Mheshimiwa Spika anamalizia shughuli, jana jioni alitawangazia wachangiaji watatu watakaomalizia mchango leo asubuhi. Kwa hiyo naomba nimwite Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Magale John Shibuda na Mheshimiwa Estherina Kilasi, hivyo ajiandae.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Pia nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote wa Menejimenti ya

Utumishi wa Umma, pamoja na Utawala Bora kwa kuweza kuandaa hotuba hii na kuileta hapa Bungeni ili tuweze kuijadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwenye mchango wangu, mchango wa kwanza unaenda kwenye utendaji wa watumishi hasa Serikalini, imekuwa ni jambo la kawaida kwamba kuna utendaji duni sana kwa watumishi umma usiokuwa na tija kwa taifa. Watumishi wanafanya kazi bila malengo mkuu wa kitengo anakaa mahali mwezi mzima kwenye idara yake hajawa na malengo kwamba amelenga wapi kwa hiyo mwanzo wa mwezi hana malengo kwamba mwisho wa mwezi atakuwa amezalisha kitu gani. Kwa hiyo, imekuwa ni jambo la kawaida kwenye idara mbalimbali tu sina haja ya kuzitaja hapa. Lakini jambo la kawaida kabisa. Ukijaribu kuangalia watumishi wa mashirika ya umma na ukiangalia na wale watumishi wa sekta binafsi ukiangalia watumishi wa Serikali utendaji wao ni tofauti kabisa, wale wa mashirika ya umma wanalipwa vizuri na wanafanya kazi kwa uwajibikaji mkubwa sana na pia wa sekta binafsi wa Serikalini hawawajibiki ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kupiga hatua tunayotaka na tunayoindea sisi Watanzania ni lazima tuhakikishe kwamba watumishi wetu wanawajibika kikamilifu. Ni jambo la kawaida kabisa kwa mtumishi wa Serikali kuingia kazini saa mbili na saa nne akatoka, anasaini ikifika saa nne ametoka. Sasa ni nchi gani ambayo inaweza kupiga hatua kwa mtumishi kukaa masaa mawili ofisini, haiwezekani.

Kwa hiyo, mimi nashauri sana Serikali ihakikishe kwamba watumishi wanawajibika kikamilifu, watumishi wawe na malengo bila kuwa na malengo hatuwezi kubadilika, mimi nilishukuru sana hizi ziara ambazo Mheshimiwa Spika alitupatia Wabunge kwenda nchi mbalimbali kwa kweli tunajifunza mengi.

Hakuna nchi iliyopiga hatua bila watumishi kuwajibika kikamilifu, watu wanafanya kazi usiku na mchana hapa kwetu ikifika saa kumi na moja uteona maduka kwanza saa tisa tu maofisi mengi yamefungwa, wenzetu wanapokezana wanafanya kazi *24 hours*. Kwa hiyo, watu walioendelea hawakufanya kazi kizembe kama tunavyofanya sisi Watanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali sasa iandae mpango wa kupima utendaji wa watumishi kwa kile alichozalisha na sio kwa kuangalia miaka aliyokaa kazini. Kuwepo na utaratibu kabisa ifikie mahali mtumishi aone fahari kwa kujali kazi kwa kuona kile alichofanya kwa kujali manufaa aliyoleta kwa taifa. Kuna mifano mingi, tuangalie mfano mdogo tu ni hao maafisa ugani, Waheshimiwa Wabunge tumekuwa tunalamika sana hapa Bungeni kwamba maafisa ugani ni wachache, na kweli ni wachache.

Lakini swali ninalojuiliza hata hao wachache walioko hawaonekani maofisini hawapo wote wapo kwenye shughuli zao kabisa wanafanya shughuli zao. Kwa hiyo, hao ni watumishi ambao tunategemea wawe na tija kwenye taifa, hali sio nzuri kwa Serikali ni lazima iamke kuhakikisha kwamba watumishi wanawajibika kikamilifu analipwa

mshahara mzuri lakini hata hivyo ule mshahara uweze kuwa na *impact* nzuri kwenye uzalishaji wa taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la upungufu, kwenye hapo hapo kwa watumishi itabidi angalau tuandae sasa ajira kwa mkatuba. Mimi nadhani ajira kwa mikataba zitakuwa na tija zaidi. Kwa sababu mtu anapojuu nipo kwenye nafasi fulani kwa miaka kadhaa, au kwa miaka mitatu, miaka mitano, ni lazima atapimwa kwa kile alichofanya kwa miaka mitano na sio kuhesabu kwamba kakaa miaka 20 lakini hakuna alichozaalisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye mchango mwengine ni upungufu wa watumishi kwenye sekta mbalimbali lakini zaidi afya, elimu pamoja na maafisa ugani. Tunaomba sana Mheshimiwa Waziri ajitahidi sana angalau kwenye Bajeti ya mwaka huu tupate watumishi wa kutosha. Kwenye mkoa wetu wa Tabora ni masikitiko makubwa sana kwanza ni mkoa wa mwisho ambaa una watumishi wachache wa afya, madaktari pamoja na wauguzi, ni mkoa wa mwisho ambaa una walimu wachache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kwamba kwa Tabora kuna karibu hospitali/*dispensary* zisizopungua 55 zimejengwa sehemu mbalimbali wananchi wamejitolea wenyewe wamejenga kwa nguvu ili kurahisisha zile huduma za afya lakini zimekaa miaka saba miaka nane, hazijapata hata kufunguliwa, hakuna hata wahudumu.

Kwa kweli inasikitisha mwananchi anajenga jengo linakamilika kila kitu kimekamilika ni kuletewa mhudumu tu aweze kutoa huduma miaka saba mpaka yale majengo yameanza kuharibika, nyingine *sealing board* zimeanza kudondoka huku wananchi wakiwa wanaendelea kutaabika kwenda umbali mkubwa kufuata huduma za afya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana mwaka huu wa fedha mkoa wa Tabora upewe kipaumbele kupata watumishi wa afya wa kutosha. Wilaya ya Urambo peke yake ina *dispensary* 15 zimejengwa zipo ni nzuri kabisa mpaka na nyingine zina mpaka nyumba za watumishi kwa jasho la wananchi. Lakini hakuna wahudumu, ninaomba sana Serikali itambue mchango wa wananchi kwa jinsi wanavyojitoa ili kurahisisisha huduma zao kuweza kupata huduma kirahisi iweze kuwasaidia wananchi wa Urambo, Tabora na kwa Urambo kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la uhamishaji wa watumishi, niipongeze Serikali kwamba baada ya Wabunge kuchangia sana hapa Bungeni kuhusu watumishi wanaokaa mahali pamoja muda mrefu kwa kweli hatua zimeanza kuchukuliwa na tumeanza kuona utekelezaji wale waliokuwa wamekaa muda mrefu wameanza kuhamishwa ili kuweza kuleta tija na ufanisi wa kazi.

Lakini ningependa pia Serikali iliangalie sana suala hili pale wanapohamisha watumishi waangalie sana wasiharibu misingi ya familia, pale ambapo watumishi

wanafanya kazi wawili aidha mke na mume, kwa hiyo Serikali iangalie uwezekano wa kuwahamisha wote kwa pamoja, lakini wanapohamisha mtumishi mmoja wanamwacha mmoja kwanza inasambaratisha familia, pili inachochea maambukizo ya UKIMWI, kwa sababu ni binadamu, na pia inawakosesha watoto msingi mzuri wa maendeleo ambapo ni elimu na mambo mengine. Kwa hiyo, viongozi wasiwahamishe watumishi kwa sababu labda ya chuki binafsi au kwa sababu ya kitu fulani ambacho kati ya mtu na mtu bali wahamishwe kwa sababu ni haki yake ya msingi na pia kujali sana masuala ya familia kwa sababu hizo familia ndiyo taifa la leo na pia ni taifa la kesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni viwango vyatya chini vyatya mishahara, hasa kwa sekta zisizo za Serikali, lazima Serikali ikubali kwamba mchango wa sekta binafsi unachangia sana sana kuajiri watumishi wengi hapa Tanzania. Wengi wetu, wengi wao wameajiriwa kwenye sekta binafsi kwa hiyo ni lazima Serikali ihakikishe kwamba kule Watanzania hawa wanapofanya kazi ambapo ni kwenye mashirika mbalimbali ni kwenye viwanda wanapata tija na sio kwamba wanakuwa wanafanya kazi tu kwa sababu hawana cha kufanya. Kwa hiyo, mimi nimesikitishwa sana na kitendo cha mwaka jana, Serikali imekaa hapa ikatamka kwamba kiwango cha chini cha mshahara shilingi laki moja na elfu hamsini, wale wenye viwanda na mashirika mbalimbali wanaopenda kuwa na *super profit* wakaanza kulalamika na kuwanyanyasa wale wafanyakazi wao kwamba nyie kama hamkubali mshahara tunaoendelea kuwapa tutawaachisha kazi tunafunga viwanda, na mambo kama hayo. Matokeo yake mimi nikafikiri Serikali ingesimamia msimamo wake na kuona kwamba watumishi hawa mshahara wa shilingi elfu themani hauwezi kumtosha Mtanzania wa leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nani atakayekupa shilingi elfu themanini kwa mwezi siku thelathini hapo hapo hujasafiri, hapo hapo hujala una watoto wa shule una kodi ya kulipa ya nyumba una umeme, una maji elfu themanini huyu mtumishi atafanyaje nazo. Kwa hiyo, mimi nadhani Serikali kitendo cha kwenda kukaa na wale wenye viwanda na wenye mashirika wakakaa na menejimenti wakakubaliana kwanza maofisini *then* wanawahitaji wafanyakazi kwamba kubalini mshahara elfu themanini baadaye tutakaa tujadiliane, hao maslahi wa wananchi hawa yamekuwa wapi? Mimi nashangaa kabisa Mheshimiwa Waziri huyu ambaye amekubali kutoa shilingi laki moja na hamsini mpaka na themanini, yeye akipewa shilingi 2600 kwa siku kuanzia asubuhi anywe chai, ale chakula gharama zimepanda, wenye viwanda hawa wanajua kabisa gharama zimepanda, hata bidhaa zinazozalishwa kwenye viwanda hivi zimepanda nauli zimepanda kwa hiyo lazima tuende na hali halisi, hatuwezi kuendelea kuwabana wafanyakazi hawa kisa kwa sababu hako Serikalini, ni lazima Serikali isimame kidete ihakikishe kwamba Mtanzania yoyote anakuwa na maisha bora. (*Makofi*)

Maisha bora tunayosema ni hayo, Serikali inasema maisha bora hapo hapo inamlazimisha mfanyakazi kupokea elfu themanini kwa mwezi mwananchi huyu hajajaliwa na Serikali kwa hapa naomba ihakikishe kwamba inarudia hili suala na kuangalia kikamilifu ihakikishe kwamba watumishi wote wa kima cha chini kinakuwa ni shilingi laki moja na hamsini na sio themanini ambayo wananchi hawa wananyanyasika na wakikimbilia kwa Serikali, Serikali ndiyo inawaambia kwamba

tulieni tutajadili. Mtanzania ataendelea kunyanyasika hayatakuwepo na mwananchi huyu anaendelea kuteseka siku zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye utawala bora, kuna matumizi mabaya sana ya madaraka na nafasi mbalimbali pamoja na mamlaka wanayopewa viongozi mbalimbali. Imekuwa ni jambo la kawaida kwa kiongozi yoyote kutumia mamlaka aliyopewa kujineemesha mwenyewe, kujilimbikizia mali kunyanyasa wale anaowahudumia na mambo mengine pia. Taifa hili tunahitaji viongozi waadilifu na wenyе upendo kwa wale anaowahudumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwa ni jambo la kawaida kwa wale watendaji wa Serikali, maana Serikali inapotoa maamuzi viongozi wanayapokea kinyume wanayatekeleza kinyume lakini Serikali mpaka ije ichukue hatua inachukua muda mrefu sana. Mfano mdogo kabisa ni mfano wa zoezi la kuhamisha mifugo ambalo lilitangazwa na Serikali. Watumishi wale waliopewa ile kazi ya kushughulikia lile suala wametumia nafasi ya kujilimbikizia mali, wameenda kupora ng'ombe za wafugaji wakajilimbikizia wao, wameanza kuwatoza faini ambazo haziendani na hali halisi ya mifugo yao. (*Makofi*)

Kiongozi alikuwa sio mfugaji anakuwa mfugaji kwa kutumia ng'ombe za mwananchi mwingine, wananchi wale wamefilisiwa lakini viongozi wamejinene pesha haya ni masuala ya kawaida yanatokea na Serikali mpaka tumekuja kugundua Wabunge ni muda mrefu wananchi wamefilisika wengine wamepoteza maisha, Serikali imechukua hatua baada ya muda.

Kwa hiyo, ninaomba hii Wizara ya utawala bora kwenye maamuzi ya Serikali inashirikishwa vipi, wakati wananchi wale wanateseka mpaka viongozi wanachukua mali zao mpaka wanawafilisi utawala bora ilikuwa wapi, masuala mengine haya pia ya kuchangisha michango, wananchi wanajitolea wanajichangisha, lakini *the way* wanavyoichukulia viongozi wanawaambushi wale wananchi, wananchi wanakosa amani wengine wanakimbia nyumba zao kisa kwa sababu tu ya michango.

Hii siyo hali nzuri, viongozi wachukue maagizo walivyopewa na utawala bora ifuatilie tumeshuhudia akinamama wanajifungulia kwenye ofisi za watendaji wa Kata kisa kwa sababu amefungwa *lockup* kwa sababu akiwa mjazito wa kujifungua kwa sababu ya mchango wa shule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Serikali ichukue hatua za uhakika kuhakikisha kwamba maagizo ya Serikali yanachukuliwa kikamilifu na yanatendeka kama ilivyoagizwa na sio kinyume chake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho dogo ni kuhusiana na suala la hili hili la viongozi, WaheshimiwaWabunge tunaposimama hapa tunazungumzia masuala ya uwajibikaji wa viongozi au Mheshimiwa Mbunge anavyosimama anasema kwamba kiongozi fulani kafanya haya na haya sio kwamba hatutambui mazuri yaliyofanywa, tunatambua mazuri yaliyofanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yale mazuri tunayapongeza tunajua amefanya mazuri na yale ambayo amefanya mabaya lazima tumwambie hapa kwamba hapa hakufanya vizuri ni wajibu wetu sisi Wabunge kwa sababu sisi tunawakilisha wananchi. Kwa hiyo tusije tukaambiwa sasa kwamba msimseme fulani kwa sababu kumbukeni mazuri yale mabaya ni njia ya ye ye kujifunza na mwingine pia kiongozi aliyeo nyuma ajifunze kwamba hakufanya vizuri na mimi niige hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua sana mambo mazuri na pale anavyofanya mtu vizuri tunampa *credit* ana anapokuwa hajafanya vizuri tunamwambia kwamba hapa ulifanya vibaya. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tusifungwe midomo kwamba tusizungumzie makosa ya viongozi kwa sababu kafanya mazuri hatukubaliani nalo, tunataka tuwe huru, nchi huru *we are independent* tunataka tuwe huru kuzungumzia viongozi wanavyofanya vibaya.

Ili aweze kujifunza na kiongozi aliyeo nyuma aweze kujifunza, vinginevyo kusema tusimguse, kwa hiyo ina maana sasa kila kiongozi akiwa madarakani atatumia nafasi yake tofauti akijua kwamba sitaguswa lakini tutakuwa hatujawatendewa haaki Watanzania kwa sababu rasilimali za Watanzania ni kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania, na sio vinginevyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana ahsante. (*Makofi*)

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana na mimi kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja hii iliyoko mbele yetu hasa tukizungumzia Bajeti ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala na Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nianze tu kwanza kwa kumpongeza kwa kweli Mheshimiwa Waziri Mkuu jinsi alivyofanya kazi jana ye ye ni mtumishi namba moja anatutia moyo sana sidhani kama kuna watu waliosikiliza jana watumishi wote wa umma na sisi Wabunge tukifuata mwendo anaokwenda Mheshimiwa Mizengo Pinda, nafikiri tutafika mbali sana naomba nikupongeze kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa na michango kidogo sana lakini naomba tu niipongeze Serikali kwa kweli kuna mabadiliko makubwa sana sana ndani ya Serikali yetu ninavyosema mabadiliko ni kwa upande wa mazingira ya utendaji kazi, maana yake kabla hujamuuliza mtumishi awajibike vipi lazima umuandalie mazingira mazuri ya kufanya kazi. Kwa hiyo, mpaka tulipofikia kwa kweli Serikali imejitahidi

sana nakumbuka mimi nimefanya kazi miaka 20 nikiwa shirika la umma, nikitumwa kwenda kwenye ofisi za Serikali yaani unashangaa hii ofisi ya Waziri, hii ofisi ya Mkurugenzi jinsi zilivyokuwa ovyo ovyo.

Lakini sasa ukiangia kwenye ofisi ile hadhi ya ofisi na nafasi ya mtu ipo naomba niwapongeze wale wote walioleta hayo mageuzi. Kwa hiyo, nasema yeze Mheshimiwa Mkapa na wenzake mpaka awamu nne kwa kweli tunaenda vizuri sana naomba mwendelee na kazi hiyo nzuri. (*Makofi*)

Tunasema tuiseme viongozi lakini kuna *limit* ya viongozi wa kuwasema kuna wale ambao tuko katika *level* moja lakini kwa ngazi za juu kwa kweli alichofanya mtu kizuri, hivi Rais akiondoka madarakani tunataka akawe omboomba mitaani asiwe na chochote?

Kwa hiyo, ni lazima kile ambacho amefanya kama Watanzania wengine walivyofanya tukiheshimu na kama kuna makosa kama alivyosema Mheshimiwa Waziri Mkuu mimi naamini kabisa kuna hitaji na yeze mwenyewe anaweza akarekebisha. Kwa hiyo, naomba hilo Watanzania tuone viongozi wetu wametufanyia mambo makubwa na kuna mageuzi makubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende kwa watumishi. Mheshimiwa Waziri tumepitisha mkataba hapa wa huduma kwa wateja. Sasa nilikuwa nataka nijue hayo marejesho ameyaona. Nataka tu nitoe mfano ndugu zangu pale Mheshimiwa Sophia Simba na Hawa Ghasia hivi siku moja tu muende katika ofisi zo zote mvae tu kandambili khanga mjifunike muingie, ujifanye una tatizo ili angalau upate yale marejesho. Kwa sababu unapoingia pale kama hujajitambulisha kwenye ofisi kwa watumishi wetu mpaka ajue wewe ni nani ndiyo anaweza akakusikiliza.

Je, Watanzania wa kawaida wale ambao wanatakiwa kuingia kwenye zile ofisi wanasikilizwaje. Mimi naamini hilo ni jambo la msingi sana kwa Serikali yetu, kwa watumishi wetu mimi nawaasa watumishi kwamba maadam tumeingia mkataba wa kuwashudumia wananchi wetu kwa niaba ya watu wote basi tufuate ile misingi iliyowekwa. Anapokuja mtu umchangamkie kwamba huyu ni mteja wangu anahitaji kuhudumiwa bila kujali nafasi yake, bila kujali ana nani bila kujali amevaa nini maana yake mpaka amesafiri kuja kwenye ofisi ina maana ana tatizo na anahitaji kusikilizwa. (*Makofi*)

Kwa hiyo, hilo ilikuwa nafikiri ni jambo la muhimu sana. Lakini inawezekana Serikali sasa tumeshaweka mazingira mazuri kwa wafanyakazi, tumeshaweka kile ambacho mfanyakazi anahitaji. Sasa tunaangalie ni nini kinachopelekea wafanyakazi sasa wasitimizie wajibu wao. Mfanyakazi anaingia kazini saa mbili asubuhi na anatoka saa tisa kamili, hivi inawezekanaje? Ni kazi kweli zote zimekwisha?

Mimi nafikiri hivi ni kwanini mfanayakazi auze nyaraka za Serikali amuu zie mtu kuna tatizo gani. Lazima tujifunze hapo. Kwa hiyo, hapo nilitaka nizungumzie kwa sababu limekuwa likinigusa sana huko nyuma tulikuwa tunaangalia mazingira tulianza mbali sana tulisema tujaribu kuweka ngazi za wafanyakazi.

Kazi ambazo ni *very risk* ambazo zina matatizo tuwalipe kiasi fulani walikuwa wanaita *rear professional* zile ambazo ni ajira ambazo hazipatikani kwa urahisi nao wapewe mishahara yao lakini sasa hivi inawezekana mfanyakazi hajui mwisho wake nini. Kwanini tusiweke mazingira ili mfanyakazi huyu anapomaliza muda wake wa kazi awe anajua mimi nikistaafu maisha yangu yatakuwa ya uhakika kwa kiwango gani yaani asiwe anabahatisha maisha.

Baada ya pale, akisema mimi nilikuwa ofisi ya utumishi wa umma unamwona kweli anafanana, lakini mtu akistaafu kazi unamwona mtaani akisema mimi nilikuwa mwalimu Mkuu shule fulani utamshangaa kwamba alikuwa mwalimu, akisema mimi nilikuwa Mkurugenzi wa ofisi fulani huwezi kuamini jinsi alivyocho, amechakaa, amekwisha, kwa sababu haoni *future* yake na ndiyo maana anapokuwa ndani ya kazi sasa anafikiri atumie njia zozote anazoweza kusudi baada ya kustaafu aweze kumudu maisha yake. Wala siendi mbali kwa nafasi hata za Wabunge hapa hata anapomaliza ubunge ukikutana naye hata kandambili saa nyingine hana akisema mimi nilikuwa mbunge unashangaa sana. (*Makofii*)

Hata mabalozi wetu walioko nje, humu nafikiri mifano mingine mnayo hata nyie wenzangu mliyoko mbele hapo kuna mabalozi waliostaafu muda mwingi wamekaa nje kwa muda ukikutana naye huwezi kuamini kama huyu mtu alikuwa balozi wa nchi fulani jinsi alivyocho na kwa sababu alikuwa hana maandalizi ya kumwandalia maisha vizuri.

Mimi nafikiri ili kuondoa hili tatizo la kuuza uza nyaraka na jinsi ya kutafuta na kuomba ombo rushwa na vitendo vingine viovu.

Mheshimiwa Waziri ninamini kabisa kuwa una uwezo wa kukaa na kubuni mkajua mfanyakazi huyu aishi maisha vizuri akistaafu ajue pesa yake ya kustaafu ipo, ajue itamwezesha kuishi mpaka maisha yake yatakapofikia mwisho. Hii ni ili kusiwe na tofauti kubwa. Kwa hilo nilitaka nitie msisitizo na ninaamini kabisa watumishi wenzangu wote mtazingatia ule mkataba kwa wateja. Mjali kila Mtanzania anapokuja ofisini kwenu kwa sababu sasa mazingira ya kazi tumewawekea ambayo yanafaa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili nilitaka nichangie ndani ya ofisi ya Rais huu mfuko wa uwezeshaji unaitwa *PTF*. Huu mfuko mwenzenu nimejifunza ni mzuri sana nafikiri kuna baadhi ya Wabunge ambao wamepata huu mfuko nimpongeze sana Mwenyekiti wa Bodi na Mkurugenzi wa Mfuko huu wa *PTF* kwa kazi nzuri ambazo wanafanya. Pendekezo langu kwa Mheshimiwa Waziri sijajua umejipanga katika kanda zipi na utaendeleaje, kwangu mimi umeanza mwaka jana na kwa kuanza tu mpaka sasa

nina wateja karibia wananchi kama 1200 ambao wamenufaika na mfuko huu kwa kutoa mikopo.

Lakini mpaka baadaye nilipojifunza vizuri ndani ya mfuko huu wa *PTF* nimefikiri kumbe tulichelewa sana hata wakati ule pesa za Mheshimiwa J K, asilimai 50 tungeweza kuwapa watu wa mfuko huu kwa sababu unaanza kwa Mtanzania wa kawaida kwa mwananchi wa kawaida wa kijiji kumwezesha kwa sababu kuna mikopo ya aina tatu wanayotoa hawa watu wa *PTF* katika mfuko wa Rais wa kuwawezesha wananchi kumsomesha mtoto akifaalu kwenda sekondari kama umeshindwa kulipia wanakukopesha halafu unalipa kidogo kidogo.

Lakini la pili kwa kujenga nyumba za bei rahisi wanakukopesha mpaka milioni kumi.

Lakini la tatu ni ile ya vikundi wanakopesha watu watano watano milioni moja na imesaidia sana kwa miezi sita tu ambayo wamekaa Mbarali nimeona mabadiliko makubwa sana.

Wito wangu ninaoutoa sasa ninaomba wananchi wangu wa Mbarali wachangamkie sana huu mfuko ili kuongeza mfano mzuri sana na watu wengine waweze kuiga. Ninaomba Mheshimiwa Waziri anapohitimisha hili, atueleze kwamba amejipanga vipi katika kuongeza mfuko huu ili kusudi Wabunge na wananchi wengine wa Tanzania waweze kunufaika kwa sababu inaanza kwenye watu wa chini sana mpaka watu wa juu sana kwa hiyo nimpongeze na ninawapongeza wafanyakazi wote walioko chini ya mfuko huu na ofisi ya Mheshimiwa Waziri kwamba msaidie sana huu mfuko kwa sababu ni chanzo pekee, ukiondoa *SCART*, ukaondoa *TASAF*, ukaleta nao mfuko ninaamini umaskini tutakuwa tumeupunguza kwa asilimia 50 kwa miaka hii inayokuja.

Kwa hilo nilikuwa na hilo la kusema lakini la msingi kabisa nilitaka niulize hivi tunaposema hao watumishi wanaotutumikia sisi tunaangalia *cadre* za juu lakini naamini watumishi ndio wanaofanya Serikali iende, watumishi hao kwa maana ya kima chini tuanzie kwenye kima cha chini msemaji aliyepita amezungumzia kwa makini elfu themanini na laki moja kwa kweli ni kiwango kidogo sana shilingi 2000 haimfanyi Mtanzania akaishi na ninaamini wale wa *cadre* za juu ukiangalia na sisi tunawapima kwa kuangalia mkataba wa kazi zao kwa maana ya *performance contract* kwamba akifanya vizuri, kwamba akifanya vizuri maana yake alipwe zaidi. (*Makofii*)

Sasa huyu mwenzangu wa chini hapa ambaye analipwa 80,000/- leo au mesenja umwambia apeleke barua ya siri kwenda ofisi nyingine na y eye ana 80,000/- akikutana na watu wa ovyo ovyo hebu niuzie hiyo barua, yuko tayari kuuza ili apate hiyo 100,000/- au 200,000/= aweze kuishi. Kwa hiyo, baada ya kufikiria hilo, nikaona ni vizuri ofisi iangalie jinsi ya kuweza kuongeza kima cha chini kutokana na umuhimu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vibali vya ajira na kupandishwa vyeo, kuna walimu wamekaa muda mrefu sana katika *cadre* hiyo hiyo moja hawajawahi kupandishwa vyeo na kwa sababu kwenye hotuba yako umesema kutakuwa na wafanyakazi zaidi 6000 na zaidi na walimu wakiwepo na madaktari kwa maana wahudumu wa afya watakuwemo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mheshimiwa Waziri azingatie sana kwa sababu lengo letu ni kuhakikisha kwamba walimu wanaboreshwa ili kusudi waweze kutumikia Serikali yetu na waweze kuboresha elimu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakikaa wanunung'unika, wakikaa wanadai mafao yao, wakikaa wakidai vyeo vyao viongezwe, inakuwa si vizuri na hatutawapa motisha ya kuweza kufundisha.

Ninaomba Mheshimiwa Waziri uangalie sana kwa upande wa elimu na upande wa afya na hasa ukizingatia vibali vyote ambavyo vimekuja ofisini kwako, tukiomba mahitaji ya walimu, tukiomba wahudumu wa afya, tunaomba vipite haraka sana hasa kwenye Halmashauri zetu naamini viko ofisi kwako. (*Makofî*)

Mkavipitie kwa sababu tumeleta tuna maana tuna mahitaji makubwa sana ya hawa walimu, hasa walimu na wahudumu wa afya. Hilo nalo Waziri ameliusia kwenye hotuba yake atalizingatia ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono hoja hii kwa asilimia mia. (*Makofî*)

**MHE. MAGALLE J. SHIBUDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata fursa hii, kwanza naomba nipongeza sana sana Mheshimiwa Hawa Ghasia, Mbunge pamoja na Mheshimiwa Sophia Simba kwa juhudzi za kuhakikisha kwamba gurudumu la maendeleo linaweza kufikiwa ndani ya ofisi ya Mheshimiwa Rais. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba niwapongeze washika dau wote wa hizi Wizara mbili, ndani ya ofisi ya Mheshimiwa Rais kwa juhudzi za mbalimbali za kuboresha ustawi na maendeleo. Vilevile nitakuwa mwizi wa fadhilu nisipompongeza Mheshimiwa Rais kwa juhudzi zake za kuhakikisha kwamba nchi yetu inaendeshwa na kwa utekelezaji wa Kanuni za Sheria pamoja na Katiba ili tuweze kupata utawala bora, napongeza sana juhudzi hizo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hizi zinamguso mkubwa sana ndani ya ustawi na maendeleo ya jamii yetu, nina machache ya kuchangia katika hotuba hii. Kwanza kabisa napongeza Chama cha Mapinduzi kwa vile hiki ndiyo Chama chenye sera ambacho kimezaa ilani ya uchaguzi pamoja na miongozi mbalimbali. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, binadamu unaweza kumpa ushauri mzuri huwezi kumpa tabia njema, kwa hali hiyo ofisi ya utawala bora ina jukumu kubwa sana la uendeshaji wa nchi yetu za kuhakikisha kwamba haki inatendeka kwa Watanzania hususani kwa sababu binadamu hatuishi hila na visa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilani ya uchaguzi ya CCM inaelekeza kwamba naomba ninukuu: “Utawala uimarishe ili kuhakikisha kwamba nchi inaendeshwa kwa misingi ya sheria kanuni na taratibu zilizowekwa za kidemokrasia nchini kote, kuanzia ngazi za vitongoji, vijiji, mitaa, kata na wilaya”.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningewomba Mheshimiwa Waziri wa Utawala Bora apange safari za kwenda vijiji ili asaidie kuinua au kuumba haja ya wanachi kujiamini pale wanapoona kwamba pana dhuluma katika maeneo yale. Vilevile namwomba Waziri wa Menejimenti ya Utumishi wa Umma ajitahidi kuelewa matatizo ya watumishi vijijini. Unapokwenda vijijini unakuta mfanyakazi Afisa Kilimo ana miaka mitano au kumi haijui nyongeza ya mshahara. Lakini yote haya yanatendeka hayawezi kuondokana kama sisi Wabunge na Serikali tutakuwa hatuna umoja na mshikamano wa kushauriana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema ya kwamba ni vema tukakubaliana ya kwamba hapa Bungeni sote tunakuja kwa minajili ya kuhakikisha kwamba tunaisadia Serikali na kuishauri. Hapa hatupo kukomoana bali tupo katika kuimarishana kwa sababu kukosoana ni kuimarishana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niliona hili niliseme kwa sababu ni hoja muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nguvu ya umoja ni upendo lakini napenda kushauri ya kwamba kukosoana kuzae upande ambao utajenga mshikamano. Mihimili hii miwili yaani Bunge na Serikali tunahitajiana sana. Kwa hiyo, ningeomba *Management* ya Utumishi wa Umma ijaribu kuona ya kwamba je wabunge wanapokuwa Mikoani wanathaminishwa vipi? Wanasadikishwa vipi kwamba ni wawakilishi wa mhimili wanapokuwa katika Wilaya na vilevile ningeomba Idara ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma ijaribu kuandaa kanuni na sheria ambazo zitawasaidia watumishi ndani ya idara zao wanapoona ya kwamba kiongozi anaamua kutumia dhamana yake siyo nguvu za hoja wakikataa wasiambiwe kwamba hawana maadili wala heshima. Hili litatusaidia kupunguza maamuzi ambayo yana mwegemo wakutumia cheo badala ya kutumia utafiti na nguvu za hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba vilevile Mheshimiwa Waziri wa Utumishi wa Umma awasaidia wataalamu kupata thamani ya kusadikisha kwamba wanatumika vema, ni aibu sana mtu ambaye amewahi kuwa mtushi katika wizara moja akipata kazi Umoja wa Mataifa anapewa kipaumbele cha kusikilizwa lakini alipokuwa ndani ya Wizara alikuwa anadhulumika kusikilizwa.

Kwa hiyo, ningeomba pawe na kanuni za kusadikisha wataalamu wetu na kuthaminisha kwamba wana mchango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba viongozi wakuu wanapaswa kuheshimika. Lakini vilevile ningependa paandaliwe miongozo ambayo itasaidia wataalamu wanaposema kwamba hili halina maslahi ya Taifa. Kwa mfano mikataba mibovu, nina uhakika kabisa uzalendo wa Watanzania upo mkubwa sana, lakini ilishindikana kutimiza hayo kwa sababu hawakuweza kuwa na fursa ya kusikilizwa kwa sababu ya unyonge wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupongeza usikivu wa Serikali baada ya jana Mheshimiwa Waziri Mkuu kuzungumza na kutamka wazi kwamba bei ya pamba inafanyiwa majadiliano ya kupitiwa upya ili ipatikane nyongeza. Natumia fursa hii kuwaomba wakulima wa Maswa wote wanaouza Pamba muahirishe kupeleka pamba yenu mkisubiri bei nzuri ili msije mkapunjika na wale waliouza watanze risiti zao kwa ajili ya nyongeza itakayotolewa. CCM Hoyee kwa maazimio mazuri ya kuongoza na kujali shida za wanyonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kusema ya kwamba umoja wetu na mshikamano ndani ya Serikali na Bunge au Mihimili yote mitatu naomba sana sana uendelezwe kwa usikivu wa kwamba kila binadamu ana viwango vyta uelewa. Tukubali ya kwamba kuwa na cheo siyo kuumbwa upya kwa nguvu ya hoja, uongozi ni kuongeza nyongeza ya maarifa, uongozi usiwe wa kutumia cheyo kama ndiyo kauli mbiu ya maangalizo ya kuongoza hiyo itakuwa inabishana na wataalamu wetu na ndiyo maana tunajikuta kwamba tunasigana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vilevile kusema ya kwamba jana Mheshimiwa Riziki hapa alizungumzia kuhusu Mahabusu mmoja ambaye alinyang'anywa mke wake na Askari Magereza. Naomba kutoa taarifa ya kwamba mtuhumiwa huyo alitoka tarehe 15 lakini nitasitiri jina lake na Askari aliyetenda jambo hilo alifunguliwa mashakata tarehe 24/2/2009 na ninapenda vilevile kutumia nafasi hii kumpongeza Kamishna Mkuu wa Magereza kwa kuhakikisha kwamba kuna nidhamu katika watu wake wote ikiwa ni pamoja na Watumishi na askari.

Aidha, natumia fursa hii kumpongeza Mkuu wa Gereza la Maswa Ndugu Shakumu Yaumba kwa juhudini zake za kuwa ni mtu ambaye anasimamia urekebishaji wa wafungwa au Mahabusu kwa kufuata haki za binadamu. Aidha, naomba kuwashakikishia ya kwamba Serikali ya CCM pamoja Kamishna wa Magereza wako imara Maswa na haki itatendeka na wala msiwe na mashaka kwamba kuna dhuluma inatendeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda vilevile kusisitiza ya kwamba utawala bora naomba idara hii sasa iende na wakati. Tunaposoma katika majarida ya kimataifa kwamba watu wa Usalama wa Taifa walihujumu haki za binadamu za baadhi ya wafungwa mfano ni Rais Obama anahangaikia sasa kwamba watapelekwa wapi watuhumiwa.

Sasa na sisi Tanzania wakati umefika tuwe na chombo cha kuhakiki utendaji kazi wetu kwa sababu kila binadamu kazaliwa na hulka na silka yake. Hulka na silka ndiyo tabia ya binadamu na hakuna binadamu aliyekamilika. Hivyo tusifikirie kwamba kila litokalo kwa Afisa Usalama basi ni jambo la kheri kwa sababu wanasema ya kwamba binadamu huwezi ukaamua uzaliwe na baba tajiri au maskini au uzaliwe na baba na mama ambao ni watiifu ndiyo maana wakasema mtoto wa nyoka ni nyoka na hulka na dhamana hufichana kama vile kikwapa kinavyofichwa na poda. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipendelea vilevile kusisitiza ya kwamba ninaomba sana Mheshimiwa Waziri wa Utawala Bora utembelee Maswa. Maswa kwa kweli naomba ielewewe au Mkoa wa Shinyanga kwa ujumla tuna bahati mbaya ya kutopata elimu. Kwa hiyo, elimu ya uraia pamoja na haki za binadamu kule ni duni sana. Hili ni jambo ambalo utakuta watu wanabambikwa kesi na vilevile napenda kutumia fursa hii kuomba serikali ihakikishe ya kwamba wale watuhumiwa wanaofungwa walioko Mahabusu wanapata fursa ya kutendewa haki, hasa wale matajiri wa Ng'ombe kwa sababu wanabambikiwa kesi za ajabuajabu. (*Makofi*)

Baada ya kusema hayo napongeza juhud zenu na hivyo Mwenyezi Mungu awajaalie katika juhud zenu enyi akina Mama, Amin! Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Shibuda kwa mchango wako.

Waheshimiwa wabunge, naomba nitoe matangazo mafupi sana machache kabla sijamwita Mheshimiwa Spika kuja kuchukua kiti ili tuendelee.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala anawaomba wajumbe wa Kamati yake wakutane saa 5 asubuhi katika Chumba Namba 219.

Tangazao lingine ni kwa wale ambao walikuwa wanachangia kwa maandishi, kwamba sasa hivi Mawaziri wataanza kuja kujibu hizo hoja mbalimbali ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge. Kwa hiyo, majibu ya wale wale ambao wanaleta hivi sasa hivi wanaweza wasipate majibu yao moja kwa moja sasa hivi.

Lakini la mwisho ni la Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, anawaomba waheshimiwa Wabunge kwamba kesho anafanya hitma ya Mama yake itakuwa tarehe 28 saa saba mchana *opposite na Martin Luther King School* kwenye *transformer* ya pili, nafikiri panafahamika.

Mwisho wa matangazo, sasa naomba nimwite Mheshimiwa Spika ili aje achukue kiti.

*Hapa Spika (Mhe. Samue J. Sitta) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge, ni vizuri tusalimiane kwa sababu mambo ya jana kidogo yalikuwa si ya kawaida. Napenda kuwahakikishia kwamba niko salama na kwa waandishi wa habari mimi sikwenda kuvamia jukwaa la Mbillia Bell niliitwa nilitamkwa niende kwa niaba ya Wabunge. Kwa hiyo, isije ikasemekana kwamba labda Mheshimiwa Spika, alipandwa na jazba sijui kitu gani basi akavamia jukwaa, hapana! Nilikaribishwa na Mbillia Bell. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea lakini kwanza niseme tu kusudio letu ni kwamba sasa saba tuweze kumaliza ili mchana tuweze kuwa sawa sawa. (Makofi)

Sasa wamekwishachangia wale waliopangwa na sasa ninamwita Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye.

**MHE. CYNTHIA HILDA NGOYE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie machache katika hotuba iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Kwanza kabisa, napenda niwapongeze hawa mawaziri wanawake wenzetu jinsi ambavyo wanafanya kazi vizuri. Sisi wanawake tunajivunia sana kwa kazi ambayo wanaifanya na wanatuwakilisha vizuri. Hongereni sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mimi nilitaka kuzungumzia mambo machache, kwanza ninapenda nizungumzie suala la utendaji wa kazi katika maeneo ya ofisi za Serikali na Umma hii ni pamoja na Mashirika ya Umma na vile vile katika Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Spika, katika utendaji wa kazi za Umma mwananchi wa kawaida anategemea kuona matokeo lakini vilevile wewe kama mtumishi unayeajiriwa katika eneo lolote mimi ningetazamia kabisa kwamba mtu aone mwenyewe kwamba anatakiwa kuona matokeo ya kazi anayoifanya. Maana yake nini? Ni kwamba umepewa dhamana ya kusimamia eneo la kazi, maana yake watu wanaokugalia wanataka kuona matokeo ya kazi ambayo umepewa. Hata unapoondoka katika eneo fulani la kazi ni lazima wenzio wanaobaki katika eneo lile na vilevile hata umma uweze kusema kwamba naam huyu mtu ameacha *landmark* fulani katika ofisi. Kuna matokeo fulani ambayo aliyafanya na sisi kama wananchi au kama wafanyakazi wengine tunaona kwamba kweli alipokuwepo alifanya hiki na hicho lazima kiwe alama.

Lakini Watanzania tunafanya kazi kwa mazoea, tunafanya kazi kwa mazoea tu hatujibidiishi hata kujielimisha ili walau kuwepo na mabadiliko fulani katika utendaji wa kazi na hili ni tatizo kubwa. Ndiyo maana tunasimama hapa tunalamika kwamba utendaji wa kazi haupo baadhi wala hawajishughulishi namna alivyoingia katika eneo la kazi hivyohivyo ndivyo anatoka. Hilo lazima tujisahihishe.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka nizungumzie katika eneo hilo hilo ni watumishi kukaa katika eneo moja kwa muda mrefu sana. Hilo ni tatizo, watu wanakaa mpaka wanasahauliwa, nendeni katika Serikali za Mitaa kwenye Halmashauri za Wilaya jamani kuna matatizo. Ukisikia watu wanafanya mambo ya ajabu ni wale ambao wamezoea katika eneo hilo miaka kumi na tano au ishirini katika eneo moja, anafanya nini hapo? Unategemea atatoa matokeo gani? Huyu mtu ni lazima ataingia sasa katika haya mambo tunayoyazungumzia hapa kuwa na *laxity* katika kufanya kazi, hana jipya, hapa nini, kazoea na kazi yake ni mambo ya kudokoadokoa tu hela za umma. Kwa hiyo, ninaomba sana uchunguzi wa kina ufanyike kwamba hawa watumishi ambaowamekaa katika maeneo fulani kwa muda mrefu. Je, wanatoa matokeo mazuri? Hapo ninachotaka kusisitiza ni mtumishi amekaa zaidi ya miaka mitano katika eneo moja inatosha, inatosha kabisa huyu apangiwe katika eneo lingine.

Mheshimiwa Spika, sasa niwasemee wanawake wenzangu wafanyakazi. Hili mimi linanitatiza sana la uhamisho unaofanywa kwa wafanyakazi wanawake, hususani walimu na watumishi wengine ambaowameolewa katika maeneo fulani lakini lazima ahamishiwe katika eneo lingine. Anaondolewa kutoka pale Dar es Salaam na kupelekwa Mtwara au Shinyanga au Lindi. Jamani anaambiwa mume wako muache hapo hapo.

Huyu ni kijana wengi sasa walio katika ajira ni vijana, unamwondoaje huyu mbali na mume wake? Hili ni lazima tulifanyie kazi ni rahisi kusema ah! Kama wewe unataka basi aidha unabaki na mume au unakwenda kazini.

Hayo siyo majibu sahihi kwa Serikali, siyo eneo la utawala bora wala jibu la kiutawala bora hata kidogo. Lazima tuangalie sasa mbinu ya kufanya yaani tufanye nini ili tusivunje ndoa, Serikali isionekane ndiyo inayovunja ndoa za watu.

Mimi nimepata malalamiko mengi sana, nimejiwa na wafanyakazi wanawake wengi sana ambaowanalalamika wanasema tazama Mbunge, mimi niko hapa kama mwalimu, mume wangu nimemwacha Shinyanga nimekuja hapa ninafanya nini?

Sasa jibu liko katika muundo wenyewe, tuangalie muundo huu unakuwaje mpaka sasa ionekane ni kero mtu kuhama kutoka katika eneo fulani kwenda katika eneo lingine bila kuambatana na mume wake. (*Makofit*)

Labda wanaume nao niwasemee, sasa mke anaondoka wewe unafanyaje? Unabaki na nani? Hapo naomba niwasemee kidogo ingawa siyo kwa uzito sana kama mwanamke. Ninaomba sana tena sana tumwangelie huyu mwanamke ambaye mara nyingi ndiye anayebebeshwa lawama inapotokea kwamba kuna maadili fulani yamevunjwa. Mwanamke kila wakati ataandamwa badala ya mwanaume.

Kwa hiyo, ninaomba sana kwamba Serikali ikae chini iangalie ni namna gani ambavyo hawa watumishi sasa tutawatendea haki katika unyumba wao lakini waweze kutekeleza wajibu wao wa kufanya kazi bila manung'uniko na bila kuathiri utendaji wa kazi.

Tume ya Maadili ya Viongozi, mimi naiopongeza kwa kazi nzuri wanayofanya, kazi ni nzuri na ninaamini kabisa kila kiongozi ambaye anapewa jukumu la kutaja mali yake anataja mali yake yote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, bado uaminifu katika hilo haupo. Wengine hawataji mali zote hiyo ni kweli kabisa, wengine wanaficha mali na ni mali kubwa kubwa hazitajwi.

Kwa hiyo, Waziri wa Utawala Bora naomba hilo uwatake wenzetu walio katika Tume ya Maadili hilo walifanyie kazi na kulifutilia kwa nguvu kwamba kila kiongozi anayetajwa kuelezea au kueleza wazi mali aliyonayo basi afanye hivyo kwa uaminifu mkubwa sana. Mimi ninakubaliana na utaratibu wa mtumishi awe anatakiwa kukaguliwa mali zake ambazo amezijaza katika *form*.

Tunachoomba ili isionekane kiongozi amekwepa kukaguliwa mali yake ninaomba Tume ya Maadili ya Viongozi watoe ratiba zao mapema ili viongozi wanaokaguliwa wawe wanaelewa mapema na wajue mapema kwamba mimi ifikapo mwezi fulani tarehe fulani nitakuwa na ugeni wa viongozi hawa wa Tume ya Maadili ili kuja kuhakiki mali yangu kuliko hali ilivyo hivi sasa unapewa muda mfupi mno wa kujiandaa ili uweze kukaguliwa mali ulizozitaja katika *form*.

Hii mara nyingi inajitokeza na na tunaonekana kana kwamba tunataka kuficha kitu fulani lakini wakati mwininge inakuwa ni ratiba kutotolewa mapema na wale wahusika kutojiandaa mapema. Kwa hiyo, inakuwa kama tunaficha. Kwa hiyo, ninaomba sana utaratibu uwe mzuri, wote tuna nia njema kabisa ya kuonyesha mali tunazozipata.

Mheshimiwa Spika, hili suala la mishahara limezungumziwa sana, ninaomba Serikali ijitahidi, tusingependa kila wakati kuwe na malalamiko malalamiko. Unapompa mtumishi mshahara ulio chini ya kiwango cha umasikini yaani *below poverty line* unategemea nini? Naomba sana siyo lazima litangazwe hadharani maana yake nako kutangaza hadharani pengine linaweza likaleta mushkeli kidogo na hasa baadhi ya watu ambao wanatumia sana hiyo nafasi ya mshahara ukipanda nao wanapandisha bei za vitu.

Lakini hata kama ni kwa utaratibu wa kiutawala utakaofanywa wa kupandisha mishahara ya watumishi, naomba tuzingatia hali halisi ya maisha ya Mtanzania, wengi sana wanashindwa kukidhi mahitaji yao.

Walimu tunaokaa nao huko vijijini mara nyingi unawaonea hata huruma ndiyo maana wanaingia hata kwenye vitu kama *DECI*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wanaingia huko kwenye *DECI* ni kwa sababu wanataka kukidhi mahitaji yao. Kwa hiyo, si ajabu ukamkuta mwalimu anatembea na ndala hivi hivi bila kuwa na viatu. (*Makofi*)

Lakini unamuuliza hivi wewe hujui hata maadili ya kazi yako kwamba unatakiwa kuwa nadhifu na uonyeshe mfano?

Anasema kiwango changu cha mshahara ni hiki, Mheshimiwa Mbunge, nifanye nini?

Sasa tuliangalie hilo na tuangalie kwamba tunaishi katika wakati mgumu na wakati ambao mafuta yamepanda bei kwa hiyo na huyu mtumishi tumwangalie ili na yeze aweze kukidhi mahitaji yake ya siku hadi siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na nimezungumza kwa bahati tu naomba sana kuunga mkono hoja hii na ninawendelea kuwasifu Mawaziri wenzetu wanawake wenzetu kwa kazi wanayoifanya waendelee kufanya kazi kwa ushirikiano mzuri na sisi Wabunge tutawaunga mkono kila wakati wanapofanya kazi zao.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye. Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa orodha niliyokuwa nayo mezani huyo ndiye alikuwa mchangiaji wa leo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge sasa nitaanza kuwaita Waheshimiwa Mawaziri kwa mpangiliano waliokubaliana nao ni kwamba atatangulia Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utawala Bora, Mheshimiwa Sophia Simba, kwa muda wa dakika zisizozidi dakika 15 na atahitimisha Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Mheshimiwa Hawa Ghasia, kwa muda usiozidi dakika 30.

Sasa namwita Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora, Mheshimiwa Waziri Sophia Simba. (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu.

Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa leo. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa dhamana hii aliyonikabidhi. Nami nampongeza kwa kuendelea kuiongoza nchi yetu kwa amani na hekima kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kumpongeza sana Mtoa hoja, Mheshimiwa Hawa Ghasia, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, kwa kuwasilisha hotuba yake vizuri sana. Aidha, namshukuru kwa ushirikiano

mzuri uliopo kati ya Ofisi zetu ambao umetuwezesha kutekeleza majukumu yetu ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika, pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kutuongoza vizuri katika kikao hiki cha Bajeti na vikao vyote viliviyotangulia.

Vilevile kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Wenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala Bora kwa miongozo na ushauri wao mzuri ambao umetuwezesha kufikia hapa tulipo. Pia shukrani kwa hotuba ya Upinzani ilijojaa changamoto ambayo ilitolewa na Mheshimiwa Grace Sindato Kiwelu. (*Makofi*)

Nawashukuru pia Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao ambayo imesaidia katika kuboresha utendaji wetu wa kazi kwani inatoa changamoto kubwa katika suala zima la utawala wa Sheria, uwazi na uwajibikaji.

Kwa namna ya pekee nawashukuru wanawake wote wa Tanzania kwa imani kubwa waliyoionyesha kwangu kwa kunichagua kwa kura nyingi kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT). (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, eneo la Utawala Bora ni pana sana lakini ni eneo ambalo linasemwa sana hapa Bungeni, nje ya Bunge na kwenye vyombo vyahabari hususani masuala ya rushwa ambayo ni kero kubwa kwa taifa letu. Rushwa ni adui wa haki na ni lazima idhibitiwe.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya awamu ya nne imejizatiti katika eneo hili na ipo mikakati madhubuti ambayo inalenga kuleta uadilifu katika utendaji wa Serikali na jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, suala la kupamba na na kuzuia rushwa ni suala mtambuka, kwa kuelewa hivyo Serikali inaendelea na jitihada zake katika kuboresha utawala katika nyanja zote. Kwa mfano, maboresho katika utumishi wa Umma, sekta ya fedha, Serikali za Mitaa, Sekta ya Sheria pamoja na program ya kupambana na umaskini kama vile MKUKUTA, TASAF NA MKURABITA. (*Makofi*)

Aidha, kutungwa kwa sheria mpya ya rushwapamoja na kuundwa kwa Kamati za Maadili katika Idara zote za Serikali kwa lengo la kutathimini kila wakati maadili, hali ya rushwa pamoja na kuziba mianya ya rushwa kutasaidia sana katika mapambano dhidi ya rushwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo haya ya utangulizi naomba sasa kujibu hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge. Hata hivyo, mengi yaliyoulizwa ni ushauri na mengi yametolewa ufanuzi mzuri sana na Mheshimiwa Waziri Mkuu na haitakuwa busara kiongozi wangu wa juu ameshazungumza masuala haya na mimi kuyarudia.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nianze kujibu hoja mbalimbali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuanza na Mheshimiwa John Paul Lwanji Mbunge wa Manyoni, ye ye kwanza amefurahi kwamba MKURABITA imepiga hodi Singida na kwamba kuna vijiji vimepimwa kama kijiji cha Sanjaranda na vinginevyo na wananchi wamefurahi. Lakini anatoa rai kwamba Serikali iyatarishe mabenki ili wananchi watakaopewa hati miliki za kimila waweze kukopesha bila usumbu.

Mheshimiwa Spika, awamu ya nne ya MKURABITA pamoja na mambo mengine itashirikiana na vyombo vya fedha ili kuwezesha raslimali zilizorasimishwa kutumika kama dhamana ya mikopo na katika kupata fursa nyingine za kiuchumi.

Mheshimiwa Juma H. Killimbah wa Iramba Magharibi, Mheshimiwa Mhonga said Ruhwanya Viti Maalum nao pia wameshauri kwamba MKURABITA itenye fungu maalum kwa wananchi ili kupata uelewa wa kutosha ili waweze kutumia fursa hiyo vizuri kujikomboa kiuchumi. Aidha, taasisi zinazohusika na MKURATIBA zishirikiane na chombo hiki ili kuongeza ushirikiano.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mkakati wa habari, elimu na mawasiliano utaanza katika mwaka wa fedha wa 2009/2010. Utekelezaji wa mkakati huu utawezesha kutoa elimu, habari na mawasiliano kwa wananchi. Aidha, MKURABITA pia itashiriki katika maonyesho ya kitaifa ikiwa ni pamoja na maonyesho ya NANENANE. (*Makofii*)

Katika mpango wake wa kazi ambao utekelezaji wake umeanza mwaka 2008/2009 MKURABITA inashirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo Aizar ya Ardhi katika kushughulikia masuala ya urasimisha wa ardhi na biashara.

## **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naipongeza hatoba kutokana na jinsi ilivyogusia na kuainisha maeneo mengi muhimu.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu ni kama ifuatavyo:-

Kutokana na hali ilivyokuwa ngumu hasa upande wa miundombinu ya barabara ilivyo, viongozi wa kitaifa wamekuwa pia wagumu kutembelea maeneo ya Wilaya ya Chunya. Nashauri Mheshimiwa Waziri wa Nchi, apange ziara Wilayani Chunya.

Wilayani Chunya wapo watumishi wa umma ambao wamekaa sehemu moja kwa muda mrefu, hasa wa ugani na sekta mbalimbali; wengine wamekaa sehemu hizo kwa zaidi ya miaka 25. Nashauri watumishi wa aina hiyo, wahamishiwe sehemu nyingine.

Posho wanayopata watumishi wastaa fu ni ndogo sana, ni vyema Serikali ikaangalie jinsi ya kuboresha posho hizo.

Wilaya ya Chunya yenyne Kata 23 ina upungufu wa Mahakimu wa Mahakama ya mwanzo; wapo Mahakimu watatu tu. Nashauri utaratibu ufanyike wa kutuongezea Mahakimu Wilayani kwetu.

Pamoja na kazi nzuri TAKUKURU inayoifanya mbona taasisi hii haifanyi kazi yake ipasavyo ndani ya Vyama vya Siasa? Sehemu hizo rushwa iko wazi na Taasisi ya TAKUKURU inajua na inayaona.

Baadhi ya Miradi ya TASAF hucheleweshwa sana kuanzishwa kuto kana na TASAF kutogawia fedha miradi hiyo. Nashauri TASAF ikumbushwe kushughulikia miradi husika mapema.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Napongeza Waheshimiwa Mawaziri Hawa Ghasia (Mb) na Mheshimiwa Sophia Simba (Mb) na Makatibu Wakuu, Ofisi ya Rais na Wasaidizi wote, kwa kazi ngumu sana mnazozifanya katika ofisi hizi kuu za utumishi katika nchi yetu. Mchango wangu ni kama ufutao:-

Kufunga kabisa semina, warsha na kongamano za aina zote liwe ni jambo la muda, kuna mabadiliko mengi duniani yanayotokea na ni muhimu watumishi kuelekezwa mabadiliko husika kupitia njia ya semina na kadhalika, kwa mfano, njanja za Kilimo, Mifugo, Uvuvi, Afya, Elimu, Utumishi wa Umma na kadhalika.

Nashauri tusifute kabisa semina, warsha na kongamano, ila ziwe chache, zenyetija, zilizo katika bajeti na ruhusa zake ziwe chini ya Wakurugenzi na Makatibu Wakuu.

Wabunge ambao ni *professionals* na hawajazidi umri wa miaka 55, waruhusiwe kuajiriwa katika utumishi wa umma waachapo Ubunge. Hapa Bungeni tuna Walimu wa Vyuo Vikuu, Madaktari, Wanasheria, Wahifadhi, Wahandisi, Administrators na kadhalika. Kama nafasi zipo Serikalini, naomba nao wafikiriwe kuwa *deployed* na wachangie kujenga taifa.

Pensheni za wastaa fu zimeongezeka hongereni, lakini bado malalamiko ni mengi hasa Wilayani na Vijijini kuhusu haki zisizotekelawa kwa miaka mingi. Watumishi wa zamani waangaliwe, pensheni zao ndogo mno ikiwa ni pamoja na Makatibu Wakuu wa zamani wanaadhirika mitaani.

Wabunge nao wapewe pensheni hasa baada ya kutumikia Bunge kwa *minimum* ya miaka kumi. Jambo hili lipo Kenya, Uganda, Rwanda, Zambia na kwingineko. Miradi ya TASAF katika Wilaya ya Kongwa safari hii haipo kabisa katika bajeti; ni kwa nini? Miradi hii ni mizuri sana na ni ukombozi, irudi tena haraka.

Maslahi ya Watumishi katika Utumishi wa Umma, ikiwa ni pamoja na walimu kuanzia Vyuo Vikuu hadi shule za awali na watumishi wengine, naomba yaongezwe. Madai ya mapunjo na malimbikizo yalipwe na hoja za walimu ziishe jamani. Kama wana madai ya kweli walipwe. Nafasi za juu za uongozi katika Utumishi wa Umma hazitangazwi katika magazeti na *Media* nyininge kwa nini? Nafasi hizo ni fursa kwa Watanzania wote, wenye elimu tosha, uzoefu na uwezo wa kufanya kazi hizo. Watanzania wapo hapa nchini na nje ya nchi. Katika hili, nakubaliana tusitangaze nafasi eneo la Ulinzi na Usalama, lakini kama kuna nafasi ya Afisa Mifugo Mkoa, hivi tunaficha hii nayo kwa nini? Afisa Kilimo, Afisa Wanyamapor, Afisa Utumishi, Mganga Mkuu, Afisa Misitu!

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MAULIDAH ANNA KOMU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuwapongeza Mawaziri wetu; Mama Hawa Ghasia na Mama Sophia Simba, kwa kweli wanani moyo wa matumaini kwamba, wanawake si wa jiko la mapishi ya chakula tu, lakini hata mapishi ya maendeleo wanaweza wapewe tu.

Mheshimiwa Spika, nianze na rushwa; kwa kweli rushwa hapa kwetu imefikia mtu kuona kwamba ni haki yake kupewa, kwani kauli inayotoka ni kwamba, mishahara haitoshelezi. Kwa hiyo, kama unataka huduma umliple kwanza ndio upate huduma.

Mheshimiwa Spika, kabla hatujafanya chochote, lazima kufikiria njia gani tutafanya kupata fedha ili tuweze kuongeza mishahara hasa ya wale wanaotoa huduma ya moja kwa moja kwa wananchi, mfano, kama Madaktari, Walimu, Wauguzi, Polisi na Mahakimu, inabidi tuwaangalie sana kwani wanadumisha imani ya kutoa rushwa ili upate haki.

Mheshimiwa Spika, Watanzania wamepoteza kabisa moyo wa kufanya kazi na hata heshima ya kazi pia imepungua. Wafanyakazi hawaoni umuhimu wa kuhakikisha uwajibikaji, wamesahau lazima ufanye kazi saa nane kwa siku za kazi na wamesahau kwamba, Jumamosi pia wamesamehewa. Ushauri wangu:-

Taratibu za kuhakikisha saa nane ya mfanyakazi inatumika ipasavyo; Mkuu wa Idara apewe dhamana kamili kama mfanyakazi hayupo kazini saa za kazi, yeye ndio wa kuwajibishwa.

Siku ya Jumamosi irudishwe wafanyakazi wafanye kazi kama ilivyokuwa, kwani hakuna mantiki yoyote ya kutokfanya kazi Jumamosi.

Fedha zilizopangwa za kulipa muda wa ziada, zipangiwe shughuli nyingine ila mishahara kwa wale wanaoonekana inabidi wafanye kazi zaidi ya saa yanayohitajika (8) iongezwe, lakini sio kupangwa fungu la *overtime*. Hii itazidi kufanya watu wasitumie muda wao wa saa nane ipasavyo, kwani wataona ni bora kubakisha ili afanye saa za ziada alipwe.

Wakuu wa Idara wewe wakali, sio eti gari haikumfuata mhusika basi yeye hafiki kazini kabisa au atafika saa sita mchana kwa kisingizio cha shida ya usafiri.

Mikataba ya ajira irekebishwe ili iendane na wakati wa sasa.

Kazi ya kutathmini utendaji wa mfanyakazi irudishwe kwa umakini sana na zawadi za utumishi bora zilizo nzuri zitolewe kwa heshima Siku ya Mei Mosi.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na udadisi wa mishahara hewa ya wafanyakazi Serikalini; je, uchunguzi huo umefikia wapi? Je, wafanyakazi hewa wameisha?

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENG:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Mawaziri wote wawili, kwa hotuba yao nzuri. Aidha, nawapongeza Watendaji wote wa Ofisi ya Rais, kwa maandalizi ya hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, Serikali itumie uzoefu wa *Transparency International (TI)* wa kulinganisha nchi mbalimbali duniani, kwa nia ya kuangalia nchi zenye Utawala Bora na ambazo zina utawala usioridhisha kwamba, uzoefu huo sasa utumike nchini kwetu kwa kulinganisha Taasisi, Wizara, Halmashauri na Mikoa ili kuona ni namna gani zinazingatia Utawala Bora katika maeneo yao ya kazi.

Kwa mfano; kulinganisha Halmashauri zote nchini katika vigezo vyta rushwa, matumizi mabovu, utoaji huduma; na kulinganisha viwango vyta utoaji huduma katika Mawizara, Mashirika na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Mashirika, Taasisi na Wizara, zitumie taarifa hizi kuboresha Utawala Bora katika maeneo yao. Mashirika, Taasisi na Wizara zitakazofanya vizuri, wapewe zawadi au zitambuliwe waziwazi. Utaratibu huu uwe wazi kama ule unaofanywa sana na Ofisi ya CAG, ambapo Mashirika, Taasisi na Wizara, matumizi yao yanakaguliwa bayana.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuwapongeza Mheshimiwa Hawa Ghasia na Mheshimiwa Sophia Simba.

Mheshimiwa Spika, naomba nijikite kwenye masuala ya Utawala Bora.

Tume ya Haki za Binadamu iko wapi hati kuacha mambo yanavurugika kule Zanzibar hasa unapofikia wakati wa uchaguzi?

Mheshimiwa Spika, Zanzibar hivi sasa kuna suala la vitambulisho vya ukazi, ambavyo vimefanywa ndiyo tiketi ya kuweza kupata shahada ya kupigia kura. Bahati mbaya sana, kitambulisho hicho hupewi hadi uwe Mwanachama wa CCM au mtoto wa CCM au mtu kutoka Tanzania Bara ili achague Rais wa Zanzibar. Je, huo sio ukiukwaji wa haki na sheria?

Mheshimiwa Spika, inakuwaje mtu kutoka Tanzania Bara, apewe haki ya kuchagua Rais wa Zanzibar kwa kisingizio cha ukazi, ina maana mzaliwa hana haki mkazi ndio mwenye haki? Kama ni hivyo, basi tuondoe cheti cha kuzaliwa kule Zanzibar tubaki na ukazi.

Mheshimiwa Spika, pili, naomba wafanyakazi waongezewe mishahara ilingane na matumizi. Pamoja na msukosuko wa uchumi ambao na nchi yetu pia imeathirika, lakini tuwaangalie sana watumishi wetu ili waweze kufanya kazi kwa utulivu, kwani kiwango cha mshahara hakilingani na mahitaji.

Mheshimiwa Spika, Sh. 5,000 kwa kutwa haitoshi sikwambii Sh. 1,600!

Mheshimiwa Spika, namtakia Mheshimiwa Waziri, utendaji mwema wa kazi na mafanikio katika utendaji wake.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kumpongeza Waziri kwa Hotuba yake nzuri, yenye ufanuzi wa kina kuhusu masuala mbalimbali ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Pili, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono hoja hii, naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Kwa kuwa Chuo cha Utumishi wa Umma ni muhimu sana, kwa kuwa mafunzo yanayotolewa yana lengo la kuwaongeza uwezo watumishi wa umma ili watoe huduma bora kwa wananchi; na kwa kuwa Chuo hicho kina matawi mawili, yaani Chuo cha Utumishi wa Umma cha Tabora na hivi karibuni Mtwara wamepata Tawi la Chuo cha Utumishi wa Umma; Chuo cha Utumishi wa Umma cha Tabora majengo yamechakaa, yanahitaji ukarabati mkubwa na kujenga mabweni ili kuongeza idadi ya wanachuo. Chuo cha Mtwara ni kipy, kinahitaji ukarabati mkubwa na kujenga mabweni ili kuongeza idadi ya wanachuo watakaopata mafunzo katika chuo hicho. Je, Serikali imetenga fedha kiasi gani kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa mabweni katika vyuo hivyo na pia ukarabati wa Chuo cha Utumishi wa Umma cha Dar es Salaam? Je, ni lini Serikali itajenga Chuo cha Utumishi wa Umma kwa ajili ya Viongozi wa Umma/Serikali?

Kwa kuwa *TASAF* Awamu ya Kwanza na ya Pili imefanya kazi kubwa na nzuri ya kuwaleta maendeleo wananchi; je, kwa nini chombo hiki muhimu kisiongezewe fedha za kutosha kwa kuwa OC ya shilingi bilioni tatu haitoshi kutekeleza miradi mingi na kuwaleta maendeleo Watanzania?

Je, Serikali ina mpango gani wa kutunga sheria ili TASAF itambulike kisheria na kuweza kuchangiwa na vyombo vingine na kupata fedha za kutosha badala ya kutegemea mkopo kutoka Benki ya Dunia?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Nawapongeza Mheshimiwa Hawa Ghasia, Mheshimiwa Sophia Simba na Watumishi wote wa Wizara hiyo.

Mheshimiwa Spika, Miradi yote ya TASAF, ambayo haijakamilika kwa mwaka uliopita ni busara mwaka huu ikamilishwe, kwani fedha nyingi ya Serikali imetumika, pia kuwapa moyo wananchi ambao wameibua miradi hiyo kwa 20% kama itakamilika kwa wakati. Miradi iliyoletwa ipewe kipaumbele kuliko watakayoibua sasa.

Serikali itoe ajira zaidi kwa Wataalam wa TASAF ili wawe wengi zaidi, waweze kutoa elimu kwa wananchi hususan vijijini. Pia kufundisha wananchi jinsi ya kuibua miradi. Vilevile itoe ajira kwa watumishi wa ugani; na Ofisi za Serikali ziwekewe vitendea kazi.

Masekretari walegezewe masharti ya kupandishwa cheo ambayo yanamtaka mwajiri awe na sifa zifuatizo:-

Awe amechukua shorthand/hatimkato ili aweze kupandishwa cheo. Kwa hivi sasa teknolojia inamtaka Katibu Muhtasi awe anajua Computer Stage One na *Stage Two*.

Je, kwa ninini masomo hayo ya sasa yasiwe badala ya hatimkato?

Makatibu Muhtasi wapewe motisha ya mazingira magumu, kwani hawa ndio wanaotunza siri za Serikali pia wanakaa na nyaraka nyingi za nchi, kutokumjali mtumishi huyu kunamfanya asiipende kazi yake.

Kwa kuwa Chuo cha Uhazili Tabora ni cha kihistoria, ningeshauri au kuomba ukarabati upewe kipaumbele. Pia kipewe vitendea kazi, kwani chuo hicho huchukua wanafunzi wengi kutoka nchi nzima. Chuo hicho kijengewe uzio kwa usalama wao, kuzuia uhalifu. Chuo kipewe Huduma ya Afya kwa kupewa dawa za kutosha ili matron aweze kutoa huduma ya kwanza kwa wanafunzi hao. Bwalo la chakula (ukumbi), lifanyiwe ukarabati kwani linatumika kwa shughuli mbalimbali na kuweza kujipatia mapato makubwa kama kitega uchumi kwa Serikali; hutumika mara nyingi kwa harusi na sherehe nyingine.

Hazina wasicheleweshe mafao ya wastaafu. Kumbukumbu za wastaafu watarajiwa zipelekwe mapema Hazina. Serikali iweke bayana madai ya wajane

waliofiwa na waume zao, wake zao wanapodai haki zao wasisumbuke kutafuta kumbukumbu.

Pongenzi kwa Serikali kuongeza mafao ya wastaa fu kwa kima cha 50%.

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia uzima na afya njema.

Mheshimiwa Spika, nakupongeza wewe, Naibu Spika, Wenye viti wa Bunge na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, kwa kutuongoza vizuri.

Mheshimiwa Spika, mishahara ya Watumishi wa Umma, iongezwe kulingana na hali halisi ya maisha. Pia watumishi katika sekta binafsi, wanapaswa waangaliwe upya ili wafiki angalau kima cha chini cha mshahara katika Utumishi wa Umma. Hii itasaidia kuondoa rushwa.

Mheshimiwa Spika, ununuzi wa magari ya fahari upunguzwe, hasa ikilinganishwa na hali mbaya ya uchumi duniani, ambayo imeathiri nchi yetu pia.

Mheshimiwa Spika, ni vema fedha za ziada zikaelekeza kwenye Sekta ya Kilimo hasa kutokana na kaulimbiu ya Kilimo Kwanza. Kilimo kikipewa kipa umbele, kitasaidia kukuza kipato kwa wakulima na hivyo kukuza uchumi wa nchi na kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Spika, suala la vitambulisho vya ukaazi Zanzibar limekuwa ni tatizo, kwani bila ya kitambulisho hicho mtu hawesi kuandikishwa kuwa mpiga kura. Kuna mikakati ya makusudi ya kutowapatia vitambulisho baadhi ya wananchi kama mbinu za kisiasa ili wasiandikishwe kuwa wapiga kura na hasa wale wanaoonekana kuwa Wafuasi wa Chama cha CUF. Ninaiomba Serikali ya Muungano kuitia Mheshimiwa Waziri Mkuu, walione tatizo hili na kuweza kulipatia ufumbuzi ili lisije likaleta matatizo hapo baadaye.

Mheshimiwa Spika, Utawala Bora ni ule unaohakikisha kwamba, misingi ya sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa, zinafuatwa kikamilifu. Utawala Bora ni pamoja na uwajibikaji na kupiga vita maonevu ya aina yoyote, unyanyasaji na ukandamizaji, pia kupambana na rushwa kubwa na ndogo. Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kazi nzuri na juhudi zake.

Mheshimiwa Spika, naomba nielewe; Serikali ina mipango gani ya kuzuia watumishi wazuri katika fani mbalimbali hasa Afya, Elimu na kadhalika, kukimbilia nchi za nje au kwenye mashirika binafsi na baadaye kuacha pengo kubwa katika sekta nilizozitaja? Serikali ina mipango gani ya kuzuia hilo na sio kwa mabavu, lakini kwa kuboresha maslahi pamoja na mwamko wa watumishi hawa kutumiwa na nchi yao?

Mada ya pili ni kuhusu Utawala Bora. Ibara ya 13(5) inayohusu kubagua, mimi sitaki nidhanie kwamba, mambo yanayofanyika Unguja na Pemba ya kujiandikisha kitambulisho cha ukazi, ajira za polisi, jeshi na usalama wa taifa kwamba, Jamhuri ya Muungano haina habari au hajui. Siwezi kuamini kwamba, Katiba ya Zanzibar ipo juu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano.

Kwa maana hiyo, sipendi majibu ya kisiasa, napenda nifafanuliwe na Bunge hili Tukufu liambiwe kwa nini Wapemba wanabaguliwa? Kama Waziri haliamini au anataka ushahidi arudie (*a-refer*), Tume ya Hashu Mbila na Ripoti ya Makubaliano ya Muafaka ambaao haukusainiwa.

Bila Uchaguzi halali Zanzibar ni tatizo pia kwa Uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano. Hivyo basi, Utawala Bora ni kwa Tanzania, Tume ya Haki za Binadamu ni kwa Tanzania nzima.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo ambalo nimeshtuka na pengine Mheshimiwa Waziri akitoa ufanuzi mzuri na mimi nitaelewa. Jumla ya fedha inayoombwa ni Tshs. 213.177.143.000, kati ya fedha hizi Tshs. 165.739.471 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Tshs. 47.437.672 kwa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nashindwa kuelewa ninapoelezwa fedha ya matumizi ya kawaida ni kubwa mno kuliko za maendeleo; naomba ufanuzi.

Mheshimiwa Spika, la mwisho katika mchango wangu, naomba Mheshimiwa Waziri wa Utawala Bora atufafanulie; hawa watu wote ambaao ni Viongozi ambaao hawakurejesha fomu za maadili ni akina nani ambaao wao wako juu ya Sheria na hawawezi kushtakiwa au kuchukuliwa hatua za kinidhamu kama Sheria ya Maadili inavyotaka? Je, kuna sababu za muhimu za watu hawa kutokurejesha fomu za maadili? Hatua gani zimechukuliwa kwa wale wenye kasoro?

Haki sawa kwa wote. Ahsante.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, naomba mishahara iendelee kuboreshwa, ilingane na hali halisi ya maisha. Aidha, wawekezaji wabanwe ili ajira zitokanazo na rasilimali zao wanazowekeza zinufaishe wananchi wetu na sio kuleta watu wao hata kwa kazi zinazoweza kufanywa na watu wetu hapa nchini. Kisingizio cha *language barrier* kwamba, Watanzania hatumudu lugha zao sio cha msingi, kwa sababu huleta hata walinzi kutoka nje.

Aidha, wafanyakazi wa hoteli, wapagazi na wale wote wanaofanya kazi za kuwahudumia wageni, viwanja vya ndege na wateja kwenye hoteli/baa na sehemu zote za starehe, wahakikishiwe bahashishi (*Tip*) ili waweze ku-supplement mishahara midogo inayolipwa na waajiri wao, ambaao nao huilipa Serikali kodi kubwa. Nchi kama Misri ni mfano kwamba, Watumishi kama hawa ni lazima walipwe *tips* na wale wanaowahudumia na ni ishara ya upendo na ubinadamu. Hii hukuza tija kwa wahudumu na upendo kati ya wahudumu na wateja. Wizi wa mizigo hupungua. Napendekeza Serikali iliangularie hili na kuelekeza vivilivo kuhakikisha hili linatekelezwa.

Rasilimali Watu na Rasilimali Fedha ziendane na Sera ya *D by D*, kusiwepo na mrundikano wa rasilimali hizo Serikali Kuu, bali zihamishiwe Mikooani na Halmashauri za Wilaya kuimarisha mipango ya maendeleo na kupunguza mipango ya sasa ya kuimarisha mipango na masuala ya Utawala zaidi.

TAKUKURU imejipanga vizuri Wilayani ila sasa ni kuiimarisha Taasisi hii kwa rasilimali na nyenzo za kazi ili *ku-narrow gap* kati ya uchunguzi na hatua kwa watuhumiwa. Kuchelewa kwa *process* za hatua dhidi ya watuhumiwa, kunapunguza imani ya wananchi kwa Serikali na wananchi huingiwa hofu kwenda kutoa taarifa TAKUKURU, pale wanapoona hatua hazichukuliwi na hivyo kuhisi kuwa wameuzwa na kuwa *victims* wa watuhumiwa. Hata hivyo, TAKUKURU ni chombo kizuri.

Naipongeza Serikali kwa kuja na MKURABITA. Singida, MKURABITA wamepiga hodi na wamepima Kijiji changu cha Saujaranda na vingine. Wananchi wamefurahi sana. Hakuna migogoro kama sehemu nyingine, kwa sababu viongozi wa vijiji walijipanga vizuri na Wataalam wa Mkurabit walitoa elimu nzuri, wananchi wakaelewa. Rai yangu ni kwamba, Serikali iyatayarische mabenki ili wananchi watakaopewa hati miliki za kimila, waweze kukopeshwa bila usumbufu.

Mheshimiwa Spika, TASAF inafanya kazi nzuri. Serikali iendelee kutenga rasilimali fedha za kutosha ili wananchi waweze kuibua miradi zaidi ya maendeleo.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri. Pamoja na hayo, naomba Wizara yake izingatie yafuatayo katika Utumishi wa Umma:-

Watumishi waheshimu na kutii Kanuni, Sheria na Mikataba yao ya kazi. Wako Watumishi wa Serikali/Umma wanaokataa uhamisho, kwa sababu wanazozijua wao wenyewe. Watumishi wa aina hiyo, wafukuzwe kazi mara moja.

Watumishi wengine wamezama zaidi katika biashara zao kuliko ajira ya umma na inapotokea uhamisho au mabadiliko yoyote yanayomhusu mtumishi huyo, anatafuta kila sababu asiende au asitekeleze mabadiliko hayo. Wapo baadhi ya Walimu Wakuu wa Shule za Msingi, walionufaika kiuchumi kwa kuwaoza wanafunzi wa kike. Tabia hii mbaya, lazima ikemewe na Wizara na Jamii kwa jumla.

Mheshimiwa Spika, nakutakia kazi njema.

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA:** Kwanza kabisa, naunga mkono hoja mia kwa mia. Pia ningependa mambo machache yazingatiwe.

Kwa nini kundi la Walemvu wenye uwezo (wasomi) wa kushika nyadhifa mbalimbali Serikalini hawapewi nafasi kubwa za Uongozi Serikalini kama vile TAKUKURU na Ukurugenzi wa Mashirika ya Umma?

Mbona safari nyingi za viongozi waendapo nje ya nchi na hata ndani ya nchi hawawahusishi walemaru ambao wana uwezo na matokeo yake hurudiwa watu walewale? Hivi kweli huo ndio Utawala Bora?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Kwa kuwa nilishawahili kuwa Mtumishi, nakiri kuona mabadiliko yenye mafanikio, ukilinganisha na hapo awali. Pongezi sana.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 18 sehemu (b) inasema; kuweka na kusimamia utaratibu mzuri zaidi wa kupokea kero za wananchi na kuhakikisha kuwa zinapatiwa ufumbuzi wa haraka.

Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, anapozungukia Mikoa huchukua kero mbalimbali na kuwapa wasaidizi wake washughulikie, lakini wenyewe kero hizo huwa vigumu kupata majibu au ufumbuzi wake.

Naomba kero ya Ndugu Msenda toka Wilaya ya Kilwa (Mstaifu), ipatiwe ufumbuzi.

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nawapa pongezi Waheshimiwa Mawaziri; Mheshimiwa Hawa Ghasia na Mheshimiwa Sophia Simba, kwa hotuba nzuri na kazi nzuri. *Keep it up.* Waliopo Upinzani, hawana ujuzi wa kuendesha Serikali, kazi yao ni kulaumu tu. Nawatakia kila la kheri.

Naomba wawe na uvumilivu na moyo wa kupokea maoni ya kila aina; maoni ya kujenga na ya kubomoa yote yanaelekezwa kwao. Ukubwa ni kichuguu. Ahsante.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi, kuipongeza hotuba nzuri sana ya Mheshimiwa Hawa A. Ghasia (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, ambayo ameisoma kwa ufasaha wa juu, pia imeandaliwa vyema kwani imeweka wazi mambo yote yanayotegemea kutekelezwa kwa nguvu mpya, ari mpya na kasi mpya.

Mheshimiwa Spika, vile vile ninampongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora, Katibu Mkuu, pamoja na Watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii nzuri, ambayo imeunganisha Wizara mbili.

Mheshimiwa Spika, ili nisije nikasahau, kabla sijaanza kutoa ushauri wangu kwa niaba yangu binafsi, pamoja na Wanawake wa Mkoo wa Singida, Wana-CCM, pamoja na wananchi wote, chini ya kiongozi mahiri sana Mheshimiwa Parseko Kone, Mkoo wa Mkoo wa Singida. Napenda kutamka kwa moyo mkunjufu kuwa, ninaunga mkono bajeti hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuunga mkono hoja hii, sasa nianze kutoa mchango wangu kama ifuatavyo; nikiwa na matarijo kuwa Serikali itayopokea mawazo yangu na wakati wa majumuisho, yatatolewa maelezo kwa maslahi ya Wananchi wa Singida na Taifa kwa ujumla:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuikumbusha Serikali kuwa, Hospitali ya Mkoa wa Singida, inayo Daktari Bingwa mmoja tu, ambaye naye yupo kwa Mkataba. Ninaomba sana Serikali, pamoja na uhaba wa Madaktari Bingwa, nasi tufikiriwe kupatiwa Daktari Bingwa wa Wanawake au Watoto, ambao ndio wengi wenye matatizo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali, kwani imekuwa ikisikiliza sana kero za Mkoa wetu na Taifa kwa ujumla. Hivyo, ninaiomba inapopata Watumishi wapya mfano Walimu, Wauguzi, Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo na kada nyinginezo; Singida isisahaulike. Itasaidia kututoa kwenye umaskini, kwani takwimu zinaonesha kuwa, Singida ni ya kwanza kwa umaskini.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na tatizo la Idara mbalimbali kwenye Halmashauri nyingi kuongozwa na Makaimu Wakuu wa Idara. Napenda kuitahadharisha Serikali, Makaimu wengi kwa vile wanatambua ni wa muda, basi wengi wao hufuja fedha na mali ya Serikali. Ninaomba sana Serikali, izibe pengo haraka; mara Mkuu wa Idara anapostaafu, kuhamishwa, kwenda kusoma muda mrefu ama kufariki.

Mheshimiwa Spika, napenda kuikumbusha Serikali kuwa, hata Wakuu wa Idara kukaa kituo kimoja muda mrefu ni tatizo kubwa sana. Mfano, Halmashauri ya Manispaa ya Singida, Afisa wa Afya wa Manispaa, Ndugu John Natumwa, amezaliwa Singida, amesomea Singida na amefanya kazi miaka yote Singida, jambo ambalo limekuwa kero kwa Halmashauri hiyo. Ninaomba sana Serikali impe uhamisho.

Mheshimiwa Spika, vile vile Mganga Mkuu wa Manispaa ingawa hana muda mrefu, lakini ameonekana mapema kuwa ana upungufu wa kiutendaji kwa kiasi kikubwa, hata Halmashauri iliazimia apewe uhamisho endapo Serikali inamhitaji.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza sana Serikali kwa kupandisha kima cha chini cha mshahara kutoka Tshs. 80,000 hadi Tshs. 100,000, inaonesha kuwa Serikali inawajali Watumishi wake, pamoja na kima cha chini cha pensheni kuwa Tshs. 52,000.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiojificha kuwa, suala la mishahara bado ni tatizo, kulingana na hali halisi ya maisha ya kila siku. Hivyo, bado Serikali tunaihimiza kuendelea kuangalia maslahi ya Watumishi, kulingana na hali halisi ya maisha tena ya kawaida kabisa. Hii itasaidia kupunguza wizi na visingizio kazini.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kukiri kuwa, Serikali inajitahidi kupambana na rushwa kwa kiwango kikubwa, ingawa bado ni tatizo, kero kubwa hasa kwenye maeneo ya kazi.

Ninaomba kuishauri Serikali kuwa, bado kuna umuhimu wa kuendelea kutoa elimu kwa wananchi ili waichukie rushwa. Hivyo, wakiichukia ama kuikinai, wananchi hawatatoa rushwa kwani huduma zitolewazo ni bure hazilipipi.

Mheshimiwa Spika, vile vile ninaishauri Serikali, iajiri Watumishi maeneo yote yenye harufu kubwa ya rushwa kwa siri, wawe na ajira mbili; ajira moja ijulikane ila ya kuangalia suala la rushwa, iwe ajira iliyojificha hata Watumishi wenzie wasimtambue kabisa. Ninategemea itasaidia utoaji na upokeaji wa rushwa kazini, vile vile wanaobainika kuwa wanapokea na kuomba rushwa, hatua kali zichukuliwe bila huruma.

Mheshimiwa Spika, bado tatizo la ajira kwa vijana ni kubwa sana, kwani vijana wengi wanaomaliza elimu kwa viwango mbalimbali, wapo mitaani na vijijini wanazurura tu na hatimaye wanajiingiza kwenye ulevi, dawa za kulevyta na ujambazi.

Mheshimiwa Spika, hata wale vijana wanaomaliza JKT kwa kujitolea kwa miaka miwili, kurudi kijiweni ni tatizo, tunaongeza wahalifu. Kwa kuwa Wizara hii ndiyo inayotoa ajira, naomba ifikirie namna ya kuwanusuru vijana.

Mheshimiwa Spika, *PTF* ni Shirika ambalo limeonesha ufanisi wa utendaji wao kwa kiwango cha juu.

Kwa kuwa sasa *TASAF* inatoa mikopo mbalimbali, napenda kuishauri Serikali kuwa, mabilioni ya Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kiasi cha fedha kipewe *TASAF* ili waweze kutoa mikopo kwa akina mama wa kipato cha chini, kwani mabenki yetu hayana urafiki sana na wateja maskini, mara nyingi wananaufaika wananchi wenye mitaji au biashara kubwa kubwa.

Mheshimiwa Spika, nina matumaini sana kuwa, *PTF* atawakomboa wanawake na vijana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maoni yangu, ambayo nina matumaini kuwa Serikali itatoa maoni yake, ninarudia tena kuunga mkono hoja hii mia kwa mia na ninawatakia utekelezaji wenye tija na Mungu awatangulie na kuwatia nguvu.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali kwa kuthubutu kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*). Naomba sana *TASAF* waharakishe kushughulikia miradi, hasa ile inayotoka sehemu za pembezoni kama Wilaya ya Chunya, kuna vijiji

ambavyo viliibua miradi yao mwaka juzi na kukamilisha taratibu zote, lakini vijiji hivyo vimepata fedha toka Makao Makuu ya TASAF mwaka huu. Huu ni ucheleweshaji mkubwa sana, hasa ukizingatia kuwa mradi mmoja ukiisha, inabidi kijiji kiibue mradi mwingine.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kuweka juhudi kubwa sana katika kupambana na rushwa, bado tatizo hili lipo, hasa kwenye rushwa kubwa kubwa. Hapa mwanya upo kwenye Mikataba mikubwa na manunuzi makubwa. Rushwa imejificha humo na ni vigumu sana kuonekana. Naiomba sana Serikali, inapodurusu Sheria ya Manunuzi ya Mwaka 2004, iweke vipengele vitavyoiwezesha TAKUKURU kuweza kuchunguza Mikataba mikubwa kabla haijapelekwa.

**MHE. KHADIJA SALUM AL-QASSMY:** Mheshimiwa Spika, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia kuwa mzima na kuweza kuchangia hoja hii iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kuwapongeza Mawaziri wote wawili, pamoja na Watendaji wao wote, kwa kuandaa hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, naanza na *TASAF* wamefanya vizuri sana miradi yao yote, sasa nasikia kuna *TASAF II* inaanza; naiomba Serikali ianze haraka sana ili Wananchi waweze kufaidika zaidi na miradi inayoibuliwa.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iiongezee fungu Sekretarieti ya Maadili, kwani inafanya kazi kubwa ya kutembelea sehemu zote za nchi, kufuatilia viongozi na kukagua mali zao kwa umakini mkubwa.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali izidi kushughulikia rushwa, kwani ni aibu kubwa kwa nchi yetu. Isipochukuliwa hatua madhubuti, watu wengine watakuwa hawawezi kuacha tabia hii mbaya, kwani wataona Serikali haiwezi kuwafanya chochote.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Watumishi wa Umma, kipato chao ni kidogo kiasi kwamba, hawakai maofisini au sehemu zao za kazi na hawawezi kufanya kazi kwa uadilifu, kwani muda mwingi wako nje kutafuta biashara nyingine, wanazohisi kwamba, zitawaongezea kipato. Naiomba serikali iwaongezee mishahara ambao utakidhi mahitaji yao na wataweza kufanya kazi kwa uadilifu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, Madaktari ni kidogo sana, pamoja na Walimu, naiomba serikali ijithahidi kuwaajiri hata kutoka nchi za jirani na huku tukisubiri wananchi wetu wamalize kusoma.

Mheshimiwa Spika, Madaktari wanafanya kazi kubwa sana na vipato vyao ni vidogo sana na hawa ni watu muhimu sana, naiomba serikali ijithahidi sana kuwaangalia kwani wanahudumia wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, natumai Serikali itayaangalia maoni yangu na kuyafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. CHARLES N. MWERA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kukushukuru wewe, Mheshimiwa Hawa Ghasia na Mheshimiwa Sophia Simba (Mb), kwa hotuba nzuri.

Niwapongeze kwa kazi nzuri mnayofanya ya kutumikia Taifa letu ili liweze kuondokana na hali hii duni ya umaskini inayowakabili wananchi wetu licha ya kuwa na rasilimali nyingi za kumtoa Mtanzania kutoka katika hali duni ya maisha kwenda kwenye hali bora ya maisha.

Mheshimiwa Spika, napenda kupongeza miradi yote ya *TASAF* kwa sababu imefanyika na kusimamiwa vizuri na “*value for money*” imeonekana. Nitapenda kufahamu kama *TASAF* itaendelea awamu ya tatu maana katika Wilaya ya Tarime, kuna baadhi ya vijiji kama Itivyo, Gibaso, wananchi walikuwa wamechangia tayari kwa kusomba mawe, mchanga, kokoto lakini taarifa ambayo wananchi walipata, ni kuwa pesa za mradi wa *TASAF* zimeisha na wamekata tamaa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Serikali kuangalia kima cha chini cha wafanyakazi wake maana kwenye bajeti hatukuona ongezeko la mishahara kwa wafanyakazi. Gharama za maisha inazidi kupanda, mahitaji ya muhimu kama vile mchele, mkaa, nyama mafuta ya kupikia, gharama za usafiri, zinaendelea kupanda. Kwa hiyo, kuna umuhimu wa Serikali kupandisha mishahara kwa wafanyakazi ili waweze kumudu hali ya maisha.

Mheshimiwa Spika, watumishi waendele kupata mafunzo mbalimbali ili kuwa na ufanisi sehemu zao za kazi. Maeneo mbalimbali katika Idara za Serikali, rushwa ni tatizo kubwa sana, hasa katika Idara za Polisi, Mahakama, Hospitali na kwenye mikataba ambayo Serikali imekuwa ikiingia na wawekezaji (*investors*). Kwa hiyo, TAKUKURU ifanye kazi kwa bidii ili kupunguza au kuondoa tatizo la rushwa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inakabiliwa na msukosuko wa uchumi ambao unaikabili dunia nzima. Serikali lazima ipange matumizi yaendane na hali halisi ya maisha. Matumizi ya Ikulu yapo juu sana pamoja na ziara za Rais zinakuwa na ujumbe mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na wafanyakazi hewa na Serikali imekuwa inapoteza fedha nyingi kwa kulipa mishahara hewa. Watumishi wasiokuwa waaminifu wawe wanachukuliwa hatua za nidhamu pamoja na kuwafikisha kwenye vyombo vyasheria.

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kupata nafasi hii.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote kabisa, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais J.K, kwa jinsi anayoendelea kuiongoza nchi kwa amani, utulivu na upendo mkubwa baina ya wananchi wake. Nampongeza sana na Mwenyezi Mungu aendelee kumlinda.

Aidha nampongeza zaidi Mheshimiwa Rais kwa jinsi alivyoipokea nchi na miradi mbalimbali ya maendeleo kutoka Serikali ya Awamu ya Tatu na jinsi anavyoendelea kuitekeleza miradi hiyo hatua kwa hatua, kwa ustawi na maendeleo ya nchi yetu. Nampongeza sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya pondezi hizo kwa Mheshimiwa Rais, naomba pia kutumia fursa hii, kuwapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri wa Nchi, waliomo katika ofisi hii, Mheshimiwa Hawa A. Ghasia (Utumishi) na Mheshimiwa Sophia Simba (Utawala Bora). Nawapongeza akina mama hawa kwa utaratibu wao, upole na heshima kwa watu wa aina zote. Waheshimiwa hawa, tangu wateuliwe katika Wizara zao, Wizara hizo, kama wao wenyewe, zimetulia sana. Kwa uchapakazi wao, Wizara zao zinaendelea kuwa Wizara za mifano.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo hayo, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza, kuimarisha uendelezaji wa Sera. Naipongeza Serikali kwa kuhusisha Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za mwaka 1994. Mahitaji na mazingira yamebadilika, hivyo ni jambo muafaka sana kuhuishwa kwa Kanuni hizo ili zilingane na mahitaji na mazingira ya watumishi wa umma wa sasa, napongesa sana. Nashauri iwe inahuishwa kila baada ya miaka mitano kwa kuwa mabadiliko yanatokea kwa kasi.

Mheshimiwa Spika, pili, maslahi ya watumishi katika utumishi wa umma. Mishahara, ajira na upandishwaji vyeo. Ni jambo la kuvutia kama Serikali inayaangalia kwa makini maeneo haya kwani ndiyo yanayofanya watumishi wengi kuihama sekta hii na kuingia sekta binafsi. Maslahi, ni kivutio cha msingi kwa mtumishi ye yeyote. Hivyo, kila uwezo unaporuhusu, ni vema mafao nayo yakawa yanaangaliwa mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, tatu, uwajibikaji na usikivu wa umma. Eneo kubwa linaloonesha udhaifu wa utumishi wa umma na Serikali kwa jumla, ni eneo hili la malalamiko ya wananchi kuto kupatiwa majibu mapema.

Wananchi wanachohitaji, ni majibu ya vilio vyao. Majibu wanayoyahitaji siyo lazima yawe mazuri au yanayokubalika, cha msingi ni jibu siyo ubora wa jibu. Hali ilivyo, mara nyingi vilio/kero hazijibowi.

Afadhalii kama majibu yangekuwa yanachelewa kutolewa lakini yanachelewa kiasi hata cha kukatisha tamaa. Nashauri Wizara iongeze nguvu katika kuzitaka ofisi ziwe zinajibu barua mapema.

Mheshimiwa Spika, nne, ni Chuo cha Utumishi wa Umma. Hii ni hatua nzuri sana, naipongeza Serikali kwa hatua hii. Ninachokiomba ni, idadi ya watumishi wanaopitia katika vyuo hivyo iongezeke na uongozi ni kipaji kinachohitaji kuibuliwa kukuzwa na kuendelezwa. Ni vyema Serikali ikaingiza somo la utumishi au uongozi katika hatua za chini za elimu za vijana wetu. Tuendapo kwenye mahafali za shule na vyuo vyetu, tunakuta vijana wanaozawadiwa kwa uongozi bora, vijana hao tunawaandaa na kuwaendeleza vipi baada ya hapo? Je, vijana hawa hatimaye watavifikiaje vyuo vilivyotajwa kwa manufaa ya utumishi wa nchi yetu na hasa kama hawatakuwa wanajiweza sana kitaaluma?

Mheshimiwa Spika, tano, *TASAF*, ni chombo ambacho kimefanya kazi nzuri sana hapa nchini. Kimeshiriki katika kuwapatia wananchi uwezo wa kuibua miradi yao na kuisimamia wakati wa utekekelezaji. Ninachopenda kufahamishwa, ni kwa nini fedha za miradi ya *TASAF* zinachelewa sana kutolewa hadi kufikia hatua ya kuchelewesha miradi kukamilika? Naomba kufahamishwa fedha za miradi kama ni ndogo au kama kuna urasimu mkubwa wa fedha hiyo kutoka kwenye chanzo cha fedha (Hazina) hadi mahali pa mradi.

Mheshimiwa Spika, kama tatizo ni fedha kidogo basi fedha itengwayo kwa kila Wilaya ipunguzwe kulingana na fedha iliyopo. Iwapo ni urasimu, basi ninashauri tena kwa dhati, utaratibu ufupishwe/urahisishwe. *TASAF* ni chombo kizuri sana kasoro zake ni hizo tu za ucheleweshwaji wa fedha za miradi na udhaifu wa watendaji wake katika Halmashauri za Wilaya zingine, kwa kushindwa kutoa maelezo ya mikwamo ya miradi vizuizi, huku wakijifanya wao ndio “final”. Hivyo, ni vyema ofisi ya *TASAF* ikapitia mara kwa mara uwezo wa watendaji kazi wake na kuwataka kutoa maelezo ya wazi na dhati ya matokeo yanapotokea.

Mheshimiwa Spika, Mawaziri ni wazuri, wana uwezo, hotuba ni nzuri. Aidha watendaji wote wa Wizara hizi wengi si wababaishaji hivyo, naunga mkono hoja.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Utawala Bora, Makatibu Wakuu, Manaibu Katibu Wakuu, Wakuu wote wa Idara, Mashirika yaliyo chini yao. Nawapongeza sana kwa kazi nzuri mnayofanya ya kulipeleka Taifa letu mbele.

Mheshimiwa Spika, nipongeze sana shughuli zote za utumishi, mnavyosaidia kuwatetea watumishi wote ili wapate haki zao na pia kuhakikisha wanafanya kazi zao kwa misingi iliyowekwa.

Mheshimiwa Spika, namuomba sana Mheshimiwa Waziri afanye jitihada ya kuangalia upya Maafisa Utumishi waliopo kwenye Serikali zetu za Mitaa, wengi wamepitwa na miongozo ya kiutumishi bali siku hizi hufanya kazi kwa mazoea. Nashauri waanze kupigwa msasa na wale waliokaa muda mrefu kituo kimoja cha kazi, wahamishwe.

Mheshimiwa Spika, ni muda mrefu sasa umepita toka watoe tamko la kuleta *Standing Order* mpya, hivi mpango huo umeishia wapi?

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Utawala Bora, kwa kazi nzuri inayofanywa na vitengo vilivyo chini yake hasa upande wa usalama. Kwa kweli, ninampongeza sana kiongozi wao na wasaidizi wake wote. Nawashukuru sana kwa kazi ya kuhakikisha Taifa letu linabaki kwenye hali ya usalama na amani. Ninachoomba ni kuhakikisha watumishi walioko kwenye Wilaya zetu, wanafuatilia na kutolea taarifa mambo yanayoharibu amani kuchochea vurugu, mambo ya siasa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa usimamizi mzuri wa *TASAF* mpaka kukahikisha mambo mazuri yanafanyika upande wa elimu, afya, miundombinu, kilimo na kadhalika. Naomba sana mpango huu mzuri wa *TASAF* uendelee na maandalizi mazuri yafanyike ili mpango wa sasa ukiisha mpango mwingine uanze haraka sana. *TASAF* ni mkombozi wa wananchi wa vijijini.

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza sana kwa kuimarisha vita dhidi ya rushwa na ninampongeze sana kiongozi wa kitengo hiki na wasaidizi wake wote. Naomba sana wajitahidi kupambana na rushwa za aina zote mijini na vijijini. Sasa hivi pamoja na rushwa zingine, rushwa wakati wa chaguzi zetu, zinashamiri sana kwenye chaguzi za Chama na Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu tuna chaguzi zetu za Serikali za Mitaa, naomba sana wasaidizi walioko Wilayani wawe macho ili tupate viongozi wanaostahili.

Mheshimiwa Spika, watumishi ambao wakati wanaajiriwa sifa wawe wamemaliza Darasa la Saba wasionewe kwa kufukuzwa kazi sasa, waachwe mpaka wamalize muda wao la sivyo itabidi wote wa aina hiyo waachishwe kazi.

**MHE. AMEIR ALI AMEIR:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia uzima na kukutana hapa katika Bunge lako Tukufu ili kujadili hutuba hii.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze sana Mawaziri, Mheshimiwa Hawa na Mheshimiwa Sophia pamoja na watendaji wote.

Mheshimiwa Spika, kitabu cha hutuba ya Waziri, kwa kweli kimeeleza mambo mengi ambayo yametekelizwa na yale yaliyotakiwa kutekelizwa. Yale yaliyotekelizwa, tumeyaona na utekelezaji wake unaridhisha na hayo yametokana na usimamizi mzuri wa

viongozi imara waliowekwa kusimamia Ilani ya Uchaguzi wa CCM na hii ni ishara njema kuwa yale yaliyopangwa kwa kipindi hiki yatakekelezwa.

Mheshimiwa Spika, nichangie kwenye MKURABITA. MKURABITA ni Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania. Mambo mengi yamefanywa na wananchi wamefaidika na Mheshimiwa Waziri kutaja baadhi ya vijiji vilivyofaidika pia ameitaja Zanzibar kuwa mradi huu umefika, naipongeza Serikali kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, lakini utendaji wa mradi huu, haujafanya kazi ya urasimashaji wa ardhi. Zanzibar wananchi wengi wamelima katika maeneo mengi ya wazi na wana mashamba makubwa lakini hawana Hati Miliki ya maeneo hayo na kuna usumbufu mkubwa kutafuta Hati Miliki. Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, kuwa MKURABITA sasa uhamie Zanzibar kwa kazi hiyo ili kuwanusuru wananchi hao na kufaidika na malengo yaliyokusudiwa pia kuwaondoshea migogoro ya mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika kwa mchango wangu huu mfupi, naunga mkono hoja.

**MHE. HEMED MOHAMED HEMED:** Mheshimiwa Spika, ni vema nimshukuru Mola kwa kunijalia siku ya leo kuweza kuchangia hutuba iliyio mbele yetu. Pia nikushukuru wewe Mheshimiwa Spika pamoja na wasaidizi wako kwa umahiri wenu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hotuba iliyowasilishwa na Waziri, Mheshimiwa Hawa, utajua nia ya Wizara katika kufanikisha azma yake kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nia yangu ni kutoa mchango katika Wizara hii, sasa ni vizuri nianze kuhusu TASAF. Sina budi kuishukuru TASAF kwa kazi zake nzuri ambazo zinaonekana nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utawala bora, ili uchumi wetu ukue na kuwepo kwa utawala bora, katika hili ndio unapatikana usimamizi wa rasilimali zetu kupitia rasilimali watu na hii itachangia kuwepo kwa nidhamu ya hali ya juu katika nchi yetu. Kwa kuzingatia upana wa utawala bora, ni pale jinsi utendaji wa Serikali unavyoweza kutumia mapato yake na kutoa huduma za msingi kwa wananchi. Kutekelezeka kwa hili, ni kwenda sambaba na kutetea na kulinda haki za jamii zote zikiwemo za kisiasa.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu bado haijakidhi haja juu ya usimamizi wake wa utawala bora. Kuna uhakika wa baadhi ya Watendaji Wakuu wa asasi na idara mbalimbali za umma, hushindwa kufanya kazi zao ipasavyo. Kwa hali ya sasa, Serikali inachofanya ni kumhamisha kituo cha kazi. Hii ni kusema tunalindana, kazi ni kuwajibika katika kutoa huduma kwa jamii.

Mheshimiwa Spika kuhusu uchaguzi, mara nyingi Wakuu wa Nchi yetu, huamua kwa makusudi kuvunja sheria za nchi kwa kisingizio cha uchaguzi. Kitendo cha kutumia nguvu za ziada, kwa kutumia vyombo vyaya Serikali kama vile Polisi kuwatesa wananchi

eti kwa sababu ni Mpinzani, hakipaswi kuendelea. Tumewaondoa Askari wetu kuwa wana siasa lakini Serikali ndio inayowaingiza Askari wetu kulinda Chama kimoja.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu Tume ya Maadili ya Viongozi. Kwa kuzingatia majukumu ya ofisi hii, ni wazi utaona fedha zao hazitowasadida. Ni vizuri Wizara iwaonee jicho la rehema, waongezewe fedha ili waweze kufanya kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hayo, sina budi kuwatachia kheri Mawaziri wangu na Mungu awabariki.

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Spika, katika ziara zangu jimboni na katika maeneo mengine nchini nimebaini yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Hakuna wataalam wa kada mbalimbali vijijini kama Bwana na Bibi Maendeleo, Maafisa Ugani wa Kilimo, Misitu, Uvuvi, Wauguzi, Waganga na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, mipango inay buniwa na wananchi katika ngazi ya kijiji, haitekelezwi ipasavyo na mara nyingi kisingizio ni fedha. Basi hakuna sababu ya kuwataka wananchi hawa kubuni miradi isiyotekelzeza.

Mheshimiwa Spika, watendaji wengi hawana ufahamu wa kutosha wa majukumu yao, hivyo, ni vyema wakajengewa uwezo na mkazo mkubwa uelekezwe katika ngazi ya chini. Aidha, mishahara, makazi na mafao mengineyo yaboreshwe ili kuwapa ari ili hali ya kufanya kazi kwa bidii na tija iwepo.

Mheshimiwa Spika, TAKUKUKURU, ni chombo ambacho kinapigiwa sana kelele na kwa mujibu wa jedwali lililopo katika hotuba, inatosheleza kabisa kuthitibisha madai ya wananchi kutokana na taarifa walizopokea, kufanya kazi na kuchukua hatua, ni aibu isiyo na mfano.

Mheshimiwa Spika, wahamiaji haramu ni kwa kukosa uaminifu wa wasimamizi wa mipaka yetu. Ni lazima eneo hili, liangaliwe kwa kuboresha maslahi yao.

Mheshimiwa Spika, chombo ambacho kitasimamia vitambulisho, kiwe huru na kisiwe na mwelekeo wa kisasa ili kuwatendea haki wananchi.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Haki za Binadamu ijengewe uwezo wa kufanya kazi nchi nzima maana wanashindwa kuwafikia na kujua madai ya wananchi ambao haki zao nyingi zinavunjwa.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi kwa Waziri, Mheshimiwa Hawa Ghasia, kwa juhudhi zake na bidii kwa kazi anazozifanya, kwani Wizara hii ndio jicho la Watanzania watenda kazi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia eneo moja la sekta binafsi. Sekta hii, baadhi yao hawawatendei haki wafanyakazi wao, kwani mishahara yao ni midogo, haikidhi haja na iko chini ya kiwango cha kima cha chini, hii ni hatari sana. Pia hawa wafanyakazi wanafanya kazi nyingi zaidi ya muda.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuzungumzia kuhusu kazi za Madereva wa Wakuu wa Mikoa, kwani wafanyakazi hawa hufanya kazi muda mwingi hata kama ni siku za sikukuu lakini hawapati *allowance* yoyote na badala yake wanalipwa Sh.3000/= tu kama *lunch*, hana hata pesa ya kukodi *tax* anapotaka kurudi nyumbani, hata kama ni usiku. Hawa wako kazini, muda wote, hawana hata muda wa kujitafutia riziki nyingine, naomba wafikiriwe.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, nashauri mshahara, kima cha chini kifiki Shs.315,000/= kwani maisha yamepanda sana na shilingi yetu imeshuka. Vitu vimepanda bei, mshahara huo wanaopata sasa ni mdogo, hauendani na hali halisi. Mchele kilo moja sasa ni Shs.1,400/=, nyama kilo Shs.4,000/= mpaka Sh.4,500/=, maharagwe kilo Shs.1,300/= mpaka Sh.1,500/=, unga vivyo hivyo. Sasa tuijilize ingekuwa sisi zingetutosha?

Mheshimiwa Spika, katika Kitabu cha Hali ya Uchumi kimeonyesha, pato la Mtanzania kwa siku ni Sh.641 kwa mjini kama Dar es Salaam na Sh.532 kwa miji mingine. Bado hawajalipa karo za watoto wao, kodi za nyumba, mavazi, matibabu, kwa kweli Serikali iangalie upya suala hili kwani bila hivyo watumishi wenyewe roho ndogo wataendelea kurubuniwa kwa rushwa na hivyo kuwa vigumu kupiga vita dhidi ya rushwa wakati wanajitafutia kitu kidogo kwa ajili ya maisha yao ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iangalie vifungu vya bajeti visivyo na vipaumbele vya maendeleo hasa vile vya *Allowances In Kind*, Takrima na vile vya *bedding and clothing, footwear and services*, fungu (220660) na kile cha *other operating expenses* (229900) na lile fungu dogo la (231100) la *routine maintenance expenses not elsewhere classified*, vyote vinapatikana katika *program 10*, vipunguzwe kwani pesa hizo ukizijumlisha katika Wizara zote, ni pesa nyingi hivyo zaweza saidia kuongeza pato la mtumishi, tuache kupendelea wakubwa.

Mheshimiwa Spika, tuangalie pia gharama isiyo ya lazima kama kukimbiza mwenge nchi nzima. Kweli ni Mwenge wa Uhuru lakini uwashwe *as for symbol then uzimwe*, kuliko ilivyo sasa unazungushwa nchi nzima. Gharama hiyo bora iongezee pesa za mishahara angalau watumishi waweze kujikimu.

Mheshimiwa Spika, vyanzo vya mapato viko vingi, fuaeni pia ushauri uliotolewa na Kambi ya Upinzani, pesa itapatikana, tubadili *mind-set* zetu. Nchi hii ina rasilimali nyingi tukiamua tunaweza.

Mheshimiwa Spika, rushwa na fUfisadi. Bado Serikali ina kazi ya kufanya. Yapo malalamiko mengi sana juu ya rushwa kubwa kubwa katika makampuni mengi yakiwemo *Deep Green*, *Tangold*, Meremeta, Kiwira na mengine mengi. Serikali inavyoendelea kukaa kimya, inasababisha wananchi wajiulize kuna nini? Kwa nini Serikali haichukui hatua madhubuti, mbona imewezezana kwa wabahirifu wachache na wanaofanya wizi wa “*EPA*”? Hili ni jambo la msingi lisifumbiwe macho kama sheria ishike mkondo wake.

Mheshimiwa Spika, MKURABITA. Elimu itolewe kwa wananchi hasa vijijini, wengi hawajui *program* hii faida yake ni nini. Vile vile kasi iongezwe katika utekelezaji wa *program* hii, ili iweze kuwasaidia Watanzania wengi ili waweze kutumia rasilimali walizonazo ikiwemo ardhi, kujkwamua kiuchumi kwa sababu kasi ni ndogo sana.

Mheshimiwa Spika, vile vile Wizara hii ihusike au ishirikiane na Wizara ya Ardhi, ili waweze kuboresha Sheria za Ardhi na Kanuni zake, ili wananchi wafaidike na *program* hii.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii, nimpongeze Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi, Katibu Mkuu Kiongozi, Ndugu Philemon Luhanjo na Watendaji wengine wote wanohusiana na Utumishi.

Pia nimpongeze Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora, Mheshimiwa Sophia Mnyambi Simba (Mb). Wote kwa pamoja nawapa pungezi sana kwa namna wanavyofanya kazi hasa wanavyomsaidia Rais katika kuimarisha Taasisi ya Ikulu pamoja na Taasisi nyeti kama vile Takukuru, Usalama wa Taifa na Sekretarieti ya Maadili ya viongozi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, mpango wa utendaji wa Wizara hii nyeti sana, unahitaji uadilifu wa hali ya juu kwani kwenda kinyume na utendaji wa kimaadili, ni tendo la kusaliti Ofisi ya Rais na hivyo kuipaka matope, jambo ambalo haliwezi kupendeza machoni mwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Mawaziri, ni chombo cha juu sana kinachoongozwa na Rais. Chombo hiki, kinahitaji utendaji uliotukuka na wenye usiri wa hali ya juu sana. Inashangaza kuona mambo mengi yanayohusu utendaji wa Serikali na siri nyingi zinavuja? Nani mvujishaji wa siri za Serikali na iweje nyaraka nyeti za Serikali zinakuwa mikononi mwa watu ama vyombo vya habari?

Mheshimiwa Spika, kwa mtazamo wa haraka haraka, lazima wapo watu wasio waaminifu wanaovujisha siri. Ni kwa nini Serikali kuitia Taasisi zake, haijabaini wanaovujisha siri? Kwa nini siri nyingi za Mawizara zinavuja?

Mheshimiwa Spika, ni muhimu sasa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, ikatazama upya na kwa kina maadili ya Viongozi wa Umma hasa Mawaziri,

Makatibu Wakuu, Wakurugenzi, Wakuu wa Idara na walio chini yake, wote ili kuweka udhibiti wa siri za Serikali. Aidha, wale wanaobainika kutenda makosa haya ya uvujishaji siri, basi Sheria za Kimaadili, zichukuliwe na ziwe kali sana.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), kwa kazi nzuri inayoifanya hasa kwa mapambano dhidi ya rushwa kubwa (*grand corruption*). Katika hatua hii, naomba nguvu zaidi zielekezwe kwenye Halmashauri za Wilaya ambako fedha nyingi za maendeleo zinaelekezwa huko. Ukaguzi wa miradi mbalimbali iliyotekelizwa kuititia fedha za maendeleo, TAKUKURU ifuatilie kwa karibu sana hasa kwa kuzingatia thamani ya fedha (*value for money*) na kazi iliyotekelizwa.

Mheshimiwa Spika, dhana ya utawala bora, kwa kufuata nguzo zake za uwajibikaji, ushirikishwaji na uwazi. Dhana hizi pamoja na kwamba kwa kiwango kikubwa imehubiriwa zaidi kwa viongozi na Watendaji wa Umma lakini bado haijahubiriwa vya kutosha kwa wananchi. Katika kufanya hivyo, dhana hii imekuwa na uelewa wa upande mmoja zaidi yaani kwa viongozi na watendaji.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri aone umuhimu wa kutoa elimu kwa wananchi juu ya dhana hii. Katika kufanya hivyo, kutatoa uelewa wa kutosha kwa wananchi kujua ukweli wa mambo mengi na hivyo kuwa na uwezo wa kuhoji juu ya matumizi mabaya ya madaraka unaofanywa na baadhi ya watendaji na viongozi katika nia ya kufifisha dhamira nzuri ya Serikali ya kuwaleta maendeleo wananchi.

Mheshimiwa Spika, TASAF, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii. Mfuko huu ni mzuri sana katika kuharakisha maendeleo ya wananchi hasa kwa matumizi ya utaratibu wa uibuaji wa miradi. Nashukuru Serikali kwa kutekeleza miradi ya aina hii Jimboni Iramba Magharibi, isipokuwa utaratibu wa kuacha miradi hii kunaendelezwa na Kamati za Maendeleo za maeneo ya utekelezaji wa miradi.

Mheshimiwa Spika, kwa uzoefu nilioupata kuititia Jimboni kwangu, ni kwamba imejionyesha uwezo mdogo kwa Kamati hizi wa kusimamia kwa ukamilifu miradi hii. Hivyo ni vyema semina elekezi katika kujengea uwezo Kamati zifanyike. Kadhalika, Kamati za Maendeleo ya Kata kwa kushirikisha Sekretarieti ya Kata, kimaendeleo lazima iwe karibu na Kamati hizi katika udhibiti na usimamizi wa miradi ili kuwa na miradi bora na endelevu.

Mheshimiwa Spika, MKURABITA, pamoja na Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge, kuandaliwa kwa dhamira ya kuzipa uhai wa kisheria ardhi na nyumba ambazo bado hazitambuliki kisheria, utaratibu ni mzuri lakini tatizo lililopo ni kwamba mpango huu bado haujaeleweka sawa sawa kwa wananchi kwani wananchi walio wengi hawaelewii waanzie wapi ili waweze kutumia ardhi waliyonayo katika kujipatia mikopo na kuendelea leo kimaisha. Naomba Serikali itoe

ufafanuzi namna mpango huu unavyoweza kutekelezeka na iandae *programe* maalum katika kuelimisha jamii kupitia mpango huu.

Mheshimiwa Spika, maisha yanazidi kupanda siku hadi siku, kiwango cha mashahara wa kima cha chini hakiendani na takwimu stahili za kipato cha Mtanzania kwa siku, cha dola moja kwa siku. Katika hali hiyo, ni sawa na dola 30, iweje mtu mwenye familia ya watu sita amudu maisha kupitia kiwango hicho? Naomba Serikali iongeze mshahara wa kima cha chini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Utumishi, Mheshimiwa Waziri wa Utawala Bora, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi na Kamishna, kwa michango yao iliyowezesha kuandaa hotuba hii yenye mipango mikakati ya kupiga vita rushwa, kuboresha mazingira ya Watumishi wa Umma na kuendeleza azma ya Serikali ya kuwaleta wananchi mafanikio.

Mheshimiwa Spika, baada ya pungezi hizo, naomba sasa nichangie kwa kutoa ushauri katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, *TASAF*, Ibara ya sita, ukurasa wa 43. Naipongeza Serikali katika kusimamia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*) tangu kuanzishwa kwake. Miradi ya jamii 4,125 yenye thamani ya shilingi 56,941,107,472 iliibuliwa na kutekelezwa katika Halmashauri zote za Tanzania Bara na Zanzibar. Haya ni mafanikio makubwa ni bora mpango maalum uandaliwe wa kutoa taarifa baada ya miezi sita kwa Halmashauri zote. Halmashauri zilizofanya vizuri zizawadiwe ili kuleta ushindani.

Mheshimiwa Spika, jedwali Na.2, kuhusu idadi ya miradi iliyoidhinishwa Mkoa wa Mara, Halmashauri ya Wilaya mpya ya Ranya ambayo katika awamu ya pili ya *TASAF* ilitekelezwa kwa asilimia kubwa na ilipendekeza miradi mipyä lakini haikuonyeshwa katika jedwali hilo. Inawezekana imejumuishwa na Halmashauri ya Tarime, ukurasa wa 55.

Mheshimiwa Spika, uwajibikaji na usikivu kwa umma. Napongeza hatua hii ya Serikali kuandaa mwongozo kwa ajili ya utekelezaji wa mfumo wa kushughulikia malalamiko katika Idara na Taasisi za Umma. Mwongozo huu uwafikie viongozi katika ngazi zote za Idara na Taasisi. Elimu kwa wahuksika ifanyike kwa makini. Katika kila Idara ya sekta, Ofisi na Taasisi, mfumo wa kuelimisha wananchi ueleweke ili wananchi waweze kuhamasikia na mfumo huu. Ofisa ateuliwe katika kila Taasisi ambaye atakuwa na jukumu la kusimamia mfumo huu. Maelezo yatolewe katika vyombo vya habari kama vile *Television*, Radio na magazeti ili kuwawezesha wananchi kuelewa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Mawaziri na Watendaji Wakuu wote pamoja na Wasaidizi wao kwa matayarisho mazuri ya hotuba hii ya bajeti ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Utumishi wa Umma, Tabora. Naipongeza Serikali kwa kutenga fedha kwa ajili ya kuendeleza ukarabati wa majengo ya Chuo. Nasisitiza, Serikali iwe makini katika kumpata Mkandarasi mwenye uwezo wa kutekeleza ukarabati/ujenzi kwa ufanisi mzuri na kwa wakati.

Aidha, naiomba Serikali ifikirie uwezekano wa kukipanua Chuo cha Utumishi wa Umma Tabora, kwa kuongeza madarasa na mabweni ili kiweze kuchukuwa wanafunzi wengi zaidi. Nafasi ya kufanya hivyo katika eneo la Chuo, Tabora ipo tena kubwa sana. Ili kufanikisha hivyo, labda ni vema kwa Serikali kuhamisha Makao Makuu ya Chuo toka Dar es Salaam na kuyapeleka Tabora.

Mheshimiwa Spika, gharama za ujenzi/upanuzi wa Chuo cha Tabora. Wizara mama ifanye mazungumzo na Wizara ya Fedha ili Chuo kiweze kupata udhamini wa kukopa toka Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (*NSSF, PPF, LAPF, PSPF* n.k.), ili kiasi cha fedha zinazohitajika kugharimia ujenzi/upanuzi wa Chuo ninao upendekeza ziweze kupatikana.

Wizara ya Fedha isiwe na hofu ya kukidhamini Chuo hiki kupata mikopo/mikopo toka Mifuko ya Hifadhi ya Jamii au hata Taasisi nyingine za fedha, kwani chuo kina uwezo wa kulipa mikopo hiyo kutokana na fedha zake za karo. Nasisitiza utaratibu huu utumike kukiwezesha Chuo kupanuliwa haraka.

Mheshimiwa Spika, Tume Ya Mipango, nashauri Wizara ya Nchi, ifanye utafiti wa muundo mzuri wa Tume hii kwa kutembelea baadhi ya nchi nyingine duniani kama vile India.

Binafsi, napendekeza Serikali ikubali kuboresha muundo wa Tume yetu ya Mipango kwa kufuata mfano wa Tume ya Mipango ya India. Taarifa za Muundo wa Tume ya India zinapatikana kwa urahisi kupitia mtandao wa *Internet*.

Aidha, Maafisa wetu wanaweza kwenda India kufanya utafiti ninaoupendekeza kwenye Tume yenyewe.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, mimi naomba mchango wangu wote uwe utawala bora. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa juhud zake za kupambana na ufisadi. Ufisadi, unakiua Chama Tawala. Ufisadi imekuwa propaganda kubwa ya wenzetu wanaotafuta utawala.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais anapaswa kuungwa mkono katika jitihada zake. Yeye ndiye Waziri kamili wa Utawala Bora. Nawasihi wanaomsaidia wamsaidie kikamilifu na wazi wazi kupiga vita ujisadi bila ya kigugumizi. Huku duniani si vyema kuwa katikati ni vyema uwe kushoto au kulia.

Naisihi Serikali yote imuunge mkono Rais asibakie peke yake, kazi itakuwa nzito kwake. Ujisadi ni lazima tuumalize. Ni vyema ielevweke kwamba kamwe hatupaswi kulala hadi tufike mwisho.

Mheshimiwa Spika, suala la ujisadi halitaki uswahiba, tukiendekeza uswahiba tutajutia amani ambayo ndiyo tunayoringia sana. Nchi iking'ang'ania uswahiba, kwenye ujisadi tutaimaliza nchi. Mheshimiwa Rais amefungua milango, halali anahangaika kuondosha ujisadi.

Je, anapata msaada wa kutosha kwa sisi wasaidizi wake?

Mheshimiwa Spika, Naunga mkono hoja.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, napenda kujuu, Watumishi wengi wana tabia ya kuchukua madaraka ya kuwanyanyasa Watumishi wengine, je, Serikali huwa inawachukulia hatua gani?

Kwa mfano *DC* aliyepiga Walimu viboko eti akisimamishwa kazi, mimi sioni adhabu kubwa kwa mtu aliyefanya kitendo hicho.

Mheshimiwa Spika, hapa Bungeni Sheria ilipitishwa, Mwalimu yejote haruhusiwi kupiga mtoto viboko na endapo atafanya hivyo, atachukuliwa hatua, adhabu ingeongezwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kujuu mtumishi yejote mwanamke akiwa Dodoma, mume wake yuko Arusha, anaomba uhamisho wamefunga ndoa, ni kwa nini ananyimwa uhamisho, anazungushwazungushwa mpaka anakata tamaa ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, watumishi Wizara mbalimbali wanafuja mali za Serikali na baada ya kubainika, anahamishwa, je, uhamisho ndio dawa au ni kulea ugonjwa. Hata huyo anayehamia pale, anaweza akaendelea kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi hasa Madereva, wanatumia magari ya Serikali kuyalaza mitaani, yakiibiwa anapelekwa Mahamani, kesi inakaa muda mrefu, je, huo sio ucharibifu wa mali ya Serikali? Nilikuwa nayaona mambo haya kwenye mafungu ya Mawizara kwenye Kamati ya *P.A.C*, watumishi wana njia nyingi za kuharibu mali za Serikali, itafutwe adhabu ambayo itakuwa fundisho kwa wengine.

Mheshimiwa Spika, Watumishi Wizara ya Afya, Bukoba ambao ni watumishi wa Hospitali ya Mkoa, walikuwa wanaumwa kwa muda mrefu, wakaandikiwa kwenda Muhibili. Wakaomba pesa, wakanyimwa, wakatumia pesa zao, wakaambiwa watarudishiwa, mpaka sasa hawajarudishiwa hata nauli za kurudi kwenye matibabu bado wanazungushwa zungushwa. Je, mwisho si watakata tamaa maana huwezi kufanya kazi ukiwa unaumwa. Naomba litolewe tamko, walipwe hela hizo ili waweze kurudi kwenye matibabu na kazini pia.

Mheshimiwa Spika, majengo ya Watumishi wa Serikali kwa Mawizara mengi yamechakaa, ukiangalia, yanatia aibu sana hasa yaliyoko kwenye mipaka yetu kwa wanaokusanya pesa za Serikali hasa *TRA*, *Immigration* huko Tarakea, Rombo. Ni kama mabanda ya kuku ukilinganisha na ya wenzetu Wakenya. Ukilinganisha na kazi wanayoifanya ya kukusanya pesa, hayafai kabisa.

Mheshimiwa Spika, tunalea rushwa, naomba Wizara itoe amri kuhusu pensheni za waliokuwa watumishi wanaonyanyasika, kuja kupata mpaka watoe rushwa. Tunavyoju wote pensheni ndio wanaitegemea.

Mheshimiwa Spika, nyumba ya Serikali wanazoishi watumishi, ni kwa nini wasiuziwe, waishi wenyewe kwa sababu majengo yenyewe yamechakaa, naomba wayanunue wenyewe watumishi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha maoni au mchango wangu na kuomba majibu.

Mheshimiwa Spika, kila la heri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningewomba Mheshimiwa Waziri wa Utawala Bora apange safari za kwenda vijiji ili asaidie kuinua au kuumba haja ya wanachi kujiamini pale wanapoona kwamba pana dhuluma katika maeneo yale. Vilevile namwomba Waziri wa Menjimenti ya Utumishi wa Umma ajitahidi kuelewa matatizo ya watumishi vijijini. Unapokwenda vijijini unakuta mfanyakazi Afisa Kilimo ana miaka mitano au kumi hajui nyongeza ya mshahara. Lakini yote haya yanatendeka hayawezi kuondokana kama sisi Wabunge na Serikali tutakuwa hatuna umoja na mshikamano wa kushauriana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema ya kwamba ni vema tukakubaliana ya kwamba hapa Bungeni sote tunakuja kwa minajili ya kuhakikisha kwamba tunaisadia Serikali na kuishauri. Hapa hatupo kukomoana bali tupo katika kuimarishana kwa sababu kukosoana ni kuimarishana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niliona hili niliseme kwa sababu ni hoja muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nguvu ya umoja ni upendo lakini napenda kushauri ya kwamba kukosoana kuzae upande ambao utajenga mshikamano. Mihimili hii miwili

yaani Bunge na Serikali tunahitajiana sana. Kwa hiyo, ningeomba *Management* ya Utumishi wa Umma ijaribu kuona ya kwamba je wabunge wanapokuwa Mikoani wanathaminishwa vipi? Wanasadikishwa vipi kwamba ni wawakilishi wa mhimili wanapokuwa katika Wilaya na vilevile ningeomba Idara ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma ijaribu kuandaa kanuni na sheria ambazo zitawasaidia watumishi ndani ya idara zao wanapoona ya kwamba kiongozi anaamua kutumia dhamana yake siyo nguvu za hoja wakikataa wasiambiwe kwamba hawana maadili wala heshima. Hili litatusaidia kupunguza maamuzi ambayo yana mwegemo wakutumia cheo badala ya kutumia utafiti na nguvu za hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba vilevile Mheshimiwa Waziri wa Utumishi wa Umma awasaidia wataalamu kupata thamani ya kusadikisha kwamba wanatumika vema, ni aibu sana mtu ambaye amewahi kuwa mtushi katika wizara moja akipata kazi Umoja wa Mataifa anapewa kipaumbele cha kusikilizwa lakini alipokuwa ndani ya Wizara alikuwa anadhulumika kusikilizwa.

Kwa hiyo, ningeomba pawe na kanuni za kusadikisha wataalamu wetu na kuthaminisha kwamba wana mchango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba viongozi wakuu wanapaswa kuheshimika. Lakini vilevile ningependa paandaliwe miongozo ambayo itasaidia wataalamu wanaposema kwamba hili halina maslahi ya Taifa. Kwa mfano mikataba mibovu, nina uhakika kabisa uzalendo wa Watanzania upo mkubwa sana, lakini ilishindikana kutimiza hayo kwa sababu hawakuweza kuwa na fursa ya kusikilizwa kwa sababu ya unyonge wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupongeza usikivu wa Serikali baada ya jana Mheshimiwa Waziri Mkuu kuzungumza na kutamka wazi kwamba bei ya pamba inafanyiwa majadiliano ya kupitiwa upya ili ipatikane nyongeza. Natumia fursa hii kuwaomba wakulima wa Maswa wote wanaouza Pamba muahirishe kupeleka pamba yenu mkisubiri bei nzuri ili msije mkapunjika na wale waliouza watanze risiti zao kwa ajili ya nyongeza itakayotolewa. CCM Hoyee kwa maazimio mazuri ya kuongoza na kujali shida za wanyonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kusema ya kwamba umoja wetu na mshikamano ndani ya Serikali na Bunge au Mihimili yote mitatu naomba sana sana uendelezwe kwa usikivu wa kwamba kila binadamu ana viwango vya uelewa. Tukubali ya kwamba kuwa na cheo siyo kuumbwa upya kwa nguvu ya hoja, uongozi ni kuongeza nyongeza ya maarifa, uongozi usiwe wa kutumia cheyo kama ndiyo kauli mbiu ya maangalizo ya kuongoza hiyo itakuwa inabishana na wataalamu wetu na ndiyo maana tunajikuta kwamba tunasigana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vilevile kusema ya kwamba jana Mheshimiwa Riziki hapa alizungumzia kuhusu Mahabusu mmoja ambaye alinyang'anywa mke wake na Askari Magereza. Naomba kutoa taarifa ya kwamba mtuhumiwa huyo alitoka tarehe 15 lakini nitasitiri jina lake na Askari aliyetenda jambo hilo alifunguliwa mashakata

tarehe 24/2/2009 na ninapenda vilevile kutumia nafasi hii kumpongeza Kamishna Mkuu wa Magereza kwa kuhakikisha kwamba kuna nidhamu katika watu wake wote ikiwa ni pamoja na Watumishi na askari.

Aidha, natumia fursa hii kumpongeza Mkuu wa Gereza la Maswa Ndugu Shakumu Yaumba kwa juhudzi zake za kuwa ni mtu ambaye anasimamia urekebishaji wa wafungwa au Mahabusu kwa kufuata haki za binadamu. Aidha, naomba kuwahakikishia ya kwamba Serikali ya CCM pamoja Kamishna wa Magereza wako imara Maswa na haki itatendeka na wala msiwe na mashaka kwamba kuna dhuluma inatendeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda vilevile kusisitiza ya kwamba utawala bora naomba idara hii sasa iende na wakati. Tunaposoma katika majarida ya kimataifa kwamba watu wa Usalama wa Taifa walihujumu haki za binadamu za baadhi ya wafungwa mfano ni Rais Obama anahangaikia sasa kwamba watapelekwa wapi watuhumiwa.

Sasa na sisi Tanzania wakati umefika tuwe na chombo cha kuhakiki utendaji kazi wetu kwa sababu kila binadamu kazaliwa na hulka na silka yake. Hulka na silka ndiyo tabia ya binadamu na hakuna binadamu aliyekamilika. Hivyo tusifikirie kwamba kila litokalo kwa Afisa Usalama basi ni jambo la kheri kwa sababu wanassema ya kwamba binadamu huwezi ukaamua uzaliwe na baba tajiri au maskini au uzaliwe na baba na mama ambao ni watiifu ndiyo maana wakasema mtoto wa nyoka ni nyoka na hulka na dhamana hufichana kama vile kikwapa kinavyofichwa na poda. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipendelea vilevile kusisitiza ya kwamba ninaomba sana Mheshimiwa Waziri wa Utawala Bora utembelee Maswa. Maswa kwa kweli naomba ielevweke au Mkoa wa Shinyanga kwa ujumla tuna bahati mbaya ya kutopata elimu. Kwa hiyo, elimu ya uraia pamoja na haki za binadamu kule ni duni sana. Hili ni jambo ambalo utakuta watu wanabambikwa kesi na vilevile napenda kutumia fursa hii kuomba serikali ihakikishe ya kwamba wale watuhumiwa wanaofungwa walioko Mahabusu wanapata fursa ya kutendewa haki, hasa wale matajiri wa Ng'ombe kwa sababu wanabambikiwa kesi za ajabuajabu. (*Makofi*)

Baada ya kusema hayo napongeza juhudzi zenu na hivyo Mwenyezi Mungu awajaalie katika juhudzi zenu enyi akina Mama, Amin! Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Shibuda kwa mchango wako.

Waheshimiwa wabunge, naomba nitoe matangazo mafupi sana machache kabla sijamwita Mheshimiwa Spika kuja kuchukua kiti ili tuendelee.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala anawaomba wajumbe wa Kamati yake wakutane saa 5 asubuhi katika Chumba Namba 219.

Tangazao lingine ni kwa wale ambao walikuwa wanachangia kwa maandishi, kwamba sasa hivi Mawaziri wataanza kuja kujibu hizo hoja mbalimbali ambazo

zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge. Kwa hiyo, majibu ya wale wale ambao wanaleta hivi sasa hivi wanaweza wasipate majibu yao moja kwa moja sasa hivi.

Lakini la mwisho ni la Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, anawaomba waheshimiwa Wabunge kwamba kesho anafanya hitma ya Mama yake itakuwa tarehe 28 saa saba mchana *opposite na Martin Luther King School* kwenye *transformer* ya pili, nafikiri panafahamika.

Mwisho wa matangazo, sasa naomba nimwite Mheshimiwa Spika ili aje achukue kiti.

*Hapa Spika (Mhe. Samue J. Sitta) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge, ni vizuri tusalimiane kwa sababu mambo ya jana kidogo yalikuwa si ya kawaida. Napenda kuwashakishia kwamba niko salama na kwa waandishi wa habari mimi sikwenda kuvamia jukwaa la Mbillia Bell niliitwa nilitamkwa niende kwa niaba ya Wabunge. Kwa hiyo, isije ikasemekana kwamba labda Mheshimiwa Spika, alipandwa na jazba sijui kitu gani basi akavamia jukwaa, hapana! Nilikaribishwa na Mbillia Bell. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea lakini kwanza niseme tu kusudio letu ni kwamba sasa saba tuweze kumaliza ili mchana tuweze kuwa sawa sawa. (Makofi)

Sasa wamekwishachangia wale waliopangwa na sasa ninamwita Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye.

**MHE. CYNTHIA HILDA NGOYE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie machache katika hotuba iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Kwanza kabisa, napenda niwapongeze hawa mawaziri wanawake wenzetu jinsi ambavyo wanafanya kazi vizuri. Sisi wanawake tunajivunia sana kwa kazi ambayo wanaifanya na wanatuwakilisha vizuri. Hongereni sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mimi nilitaka kuzungumzia mambo machache, kwanza ninapenda nizungumzie suala la utendaji wa kazi katika maeneo ya ofisi za Serikali na Umma hii ni pamoja na Mashirika ya Umma na vile vile katika Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Spika, katika utendaji wa kazi za Umma mwananchi wa kawaida anategemea kuona matokeo lakini vilevile wewe kama mtumishi unayeajiriwa katika eneo lolote mimi ningetazamia kabisa kwamba mtu aone mwenyewe kwamba anatakiwa kuona matokeo ya kazi anayoifanya. Maana yake nini? Ni kwamba umepewa dhamana ya kusimamia eneo la kazi, maana yake watu wanaokugalia wanataka kuona matokeo ya kazi ambayo umepewa. Hata unapoondoka katika eneo fulani la kazi ni lazima wenzio wanaobaki katika eneo lile na vilevile hata umma uweze kusema kwamba naam huyu

mtu ameacha *landmark* fulani katika ofisi. Kuna matokeo fulani ambayo aliyafanya na sisi kama wananchi au kama wafanyakazi wengine tunaona kwamba kweli alipokuwepo alifanya hiki na hicho lazima kiwe alama.

Lakini Watanzania tunafanya kazi kwa mazoea, tunafanya kazi kwa mazoea tu hatujibidiishi hata kujielimisha ili walau kuwepo na mabadiliko fulani katika utendaji wa kazi na hili ni tatizo kubwa. Ndiyo maana tunasimama hapa tunalamika kwamba utendaji wa kazi haupo baadhi wala hawajishughulishi namna alivyoingia katika eneo la kazi hivyohivyo ndivyo anatoka. Hilo lazima tujisahihishe.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka nizungumzie katika eneo hilo hilo ni watumishi kukaa katika eneo moja kwa muda mrefu sana. Hilo ni tatizo, watu wanakaa mpaka wanasaauliwa, nendeni katika Serikali za Mitaa kwenye Halmashauri za Wilaya jamani kuna matatizo. Ukitabu watu wanafanya mambo ya ajabu ni wale ambao wamezoea katika eneo hilo miaka kumi na tano au ishirini katika eneo moja, anafanya nini hapo? Unategemea atatoa matokeo gani? Huyu mtu ni lazima ataingia sasa katika haya mambo tunayoyazungumzia hapa kuwa na *laxity* katika kufanya kazi, hana jipy, hapa nini, kazoea na kazi yake ni mambo ya kudokoadokoa tu hela za umma. Kwa hiyo, ninaomba sana uchunguzi wa kina ufanyike kwamba hawa watumishi ambao wamekaa katika maeneo fulani kwa muda mrefu. Je, wanatoa matokeo mazuri? Hapo ninachotaka kusisitiza ni mtumishi amekaa zaidi ya miaka mitano katika eneo moja inatosha, inatosha kabisa huyu apangiwe katika eneo lingine.

Mheshimiwa Spika, sasa niwasemee wanawake wenzangu wafanyakazi. Hili mimi linanitatiza sana la uhamisho unaofanywa kwa wafanyakazi wanawake, hususani walimu na watumishi wengine ambao wameolewa katika maeneo fulani lakini lazima ahamishiwe katika eneo lingine. Anaondolewa kutoka pale Dar es Salaam na kupelekwa Mtwara au Shinyanga au Lindi. Jamani anaambiwa mume wako muache hapo hapo.

Huyu ni kijana wengi sasa walio katika ajira ni vijana, unamwondoaje huyu mbali na mume wake? Hili ni lazima tulifanyie kazi ni rahisi kusema ah! Kama wewe unataka basi aidha unabaki na mume au unakwenda kazini.

Hayo siyo majibu sahihi kwa Serikali, siyo eneo la utawala bora wala jibu la kiutawala bora hata kidogo. Lazima tuangalie sasa mbinu ya kufanya yaani tufanye nini ili tusivunje ndoa, Serikali ioneerikane ndiyo inayovunja ndoa za watu.

Mimi nimepata malalamiko mengi sana, nimejiwa na wafanyakazi wanawake wengi sana ambao wanalamika wanasema tazama Mbunge, mimi niko hapa kama mwalimu, mume wangu nimewwacha Shinyanga nimekuja hapa ninafanya nini?

Sasa jibu liko katika muundo wenyewe, tuangalie muundo huu unakuwaje mpaka sasa ioneerikane ni kero mtu kuhama kutoka katika eneo fulani kwenda katika eneo lingine bila kuambatana na mume wake. (*Makofii*)

Labda wanaume nao niwasemee, sasa mke anaondoka wewe unafanyaje? Unabaki na nani? Hapo naomba niwasemee kidogo ingawa siyo kwa uzito sana kama mwanamke. Ninaomba sana tena sana tumwangelie huyu mwanamke ambaye mara nyingi ndiye anayebebeshwa lawama inapotokea kwamba kuna maadili fulani yamevunjwa. Mwanamke kila wakati ataandamwa badala ya mwanaume.

Kwa hiyo, ninaomba sana kwamba Serikali ikae chini iangalie ni namna gani ambavyo hawa watumishi sasa tutawatendea haki katika unyumba wao lakini waweze kutekeleza wajibu wao wa kufanya kazi bila manung'uniko na bila kuathiri utendaji wa kazi.

Tume ya Maadili ya Viongozi, mimi naiopongeza kwa kazi nzuri wanayofanya, kazi ni nzuri na ninaamini kabisa kila kiongozi ambaye anapewa jukumu la kutaja mali yake anataja mali yake yote. (*Makofi*

Mheshimiwa Spika, bado uaminifu katika hilo haupo. Wengine hawataji mali zote hiyo ni kweli kabisa, wengine wanaficha mali na ni mali kubwa kubwa hazitajwi.

Kwa hiyo, Waziri wa Utawala Bora naomba hilo uwatake wenzetu walio katika Tume ya Maadili hilo walifanyie kazi na kulifutilia kwa nguvu kwamba kila kiongozi anayetajwa kuelezea au kueleza wazi mali aliyonayo basi afanye hivyo kwa uaminifu mkubwa sana. Mimi ninakubaliana na utaratibu wa mtumishi awe anatakiwa kukaguliwa mali zake ambazo amezijaza katika *form*.

Tunachoomba ili isionekane kiongozi amekwepa kukaguliwa mali yake ninaomba Tume ya Maadili ya Viongozi watoe ratiba zao mapema ili viongozi wanaokaguliwa wawe wanaelewa mapema na wajue mapema kwamba mimi ifikapo mwezi fulani tarehe fulani nitakuwa na ugeni wa viongozi hawa wa Tume ya Maadili ili kuja kuhakiki mali yangu kuliko hali ilivyo hivi sasa unapewa muda mfupi mno wa kuijandaa ili uweze kukaguliwa mali ulizozitaja katika *form*.

Hii mara nyingi inajitokeza na na tunaonekana kana kwamba tunataka kuficha kitu fulani lakini wakati mwininge inakuwa ni ratiba kutotolewa mapema na wale wahusika kutojiandaa mapema. Kwa hiyo, inakuwa kama tunaficha. Kwa hiyo, ninaomba sana utaratibu uwe mzuri, wote tuna nia njema kabisa ya kuonyesha mali tunazozipata.

Mheshimiwa Spika, hili suala la mishahara limezungumziwa sana, ninaomba Serikali ijithidi, tusingependa kila wakati kuwe na malalamiko malalamiko. Unapompa mtumishi mshahara ulio chini ya kiwango cha umasikini yaani *below poverty line* unategemea nini? Naomba sana siyo lazima litangazwe hadharani maana yake nako kutangaza hadharani pengine linaweza likaleta mushkeli kidogo na hasa baadhi ya watu amba wanatumia sana hiyo nafasi ya mshahara ukipanda nao wanapandisha bei za vitu.

Lakini hata kama ni kwa utaratibu wa kiutawala utakaofanywa wa kupandisha mishahara ya watumishi, naomba tuzingatie hali halisi ya maisha ya Mtanzania, wengi sana wanashindwa kukidhi mahitaji yao.

Walimu tunaokaa nao huko vijijini mara nyingi unawaonea hata huruma ndiyo maana wanaingia hata kwenye vitu kama *DECI*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wanaingia huko kwenye *DECI* ni kwa sababu wanataka kukidhi mahitaji yao. Kwa hiyo, si ajabu ukamkuta mwalimu anatembea na ndala hivi hivi bila kuwa na viatu. (*Makofi*)

Lakini unamuuliza hivi wewe hujui hata maadili ya kazi yako kwamba unatakiwa kuwa nadhifu na uonyeshe mfano?

Anasema kiwango changu cha mshahara ni hiki, Mheshimiwa Mbunge, nifanye nini?

Sasa tuliangalie hilo na tuangalie kwamba tunaishi katika wakati mgumu na wakati ambao mafuta yamepanda bei kwa hiyo na huyu mtumishi tumwangalie ili na yeze aweze kukidhi mahitaji yake ya siku hadi siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na nimezungumza kwa bahati tu naomba sana kuunga mkono hoja hii na ninawendelea kuwasifu Mawaziri wenzetu wanawake wenzetu kwa kazi wanayoifanya waendelee kufanya kazi kwa ushirikiano mzuri na sisi Wabunge tutawaunga mkono kila wakati wanapofanya kazi zao.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye. Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa orodha niliyokuwa nayo mezani huyo ndiye alikuwa mchangiaji wa leo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge sasa nitaanza kuwaita Waheshimiwa Mawaziri kwa mpangiliano waliokubaliana nao ni kwamba atatangulia Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utawala Bora, Mheshimiwa Sophia Simba, kwa muda wa dakika zisizozidi dakika 15 na atahitimisha Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Mheshimiwa Hawa Ghasia, kwa muda usiozidi dakika 30.

Sasa namwita Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora, Mheshimiwa Waziri Sophia Simba. (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu.

Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa leo. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa dhamana hii aliyonikabidhi. Nami nampongeza kwa kuendelea kuiongoza nchi yetu kwa amani na hekima kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kumpongeza sana Mtoa hoja, Mheshimiwa Hawa Ghasia, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, kwa kuwasilisha hotuba yake vizuri sana. Aidha, namshukuru kwa ushirikiano mzuri uliopo kati ya Ofisi zetu ambao umetuwezesha kutekeleza majukumu yetu ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika, pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kutuongoza vizuri katika kikao hiki cha Bajeti na vikao vyote vilivvyotangulia.

Vilevile kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Wenyeekiti na Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala Bora kwa miongozo na ushauri wao mzuri ambao umetuwezesha kufikia hapa tulipo. Pia shukrani kwa hotuba ya Upinzani ilijojaa changamoto ambayo ilitolewa na Mheshimiwa Grace Sindato Kiwelu. (*Makofi*)

Nawashukuru pia Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao ambayo imesaidia katika kuboresha utendaji wetu wa kazi kwani inatoa changamoto kubwa katika suala zima la utawala wa Sheria, uwazi na uwajibikaji.

Kwa namna ya pekee nawashukuru wanawake wote wa Tanzania kwa imani kubwa waliyoionyesha kwangu kwa kunichagua kwa kura nyingi kuwa Mwenyeekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT). (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, eneo la Utawala Bora ni pana sana lakini ni eneo ambalo linasemwa sana hapa Bungeni, nje ya Bunge na kwenye vyombo vyahabari hususani masuala ya rushwa ambayo ni kero kubwa kwa taifa letu. Rushwa ni adui wa haki na ni lazima idhibitiwe.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya awamu ya nne imejizatiti katika eneo hili na ipo mikakati madhubuti ambayo inalenga kuleta uadilifu katika utendaji wa Serikali na jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, suala la kupamba na na kuzuia rushwa ni suala mtambuka, kwa kuelewa hivyo Serikali inaendelea na jitihada zake katika kuboresha utawala katika nyanja zote. Kwa mfano, maboresho katika utumishi wa Umma, sekta ya fedha, Serikali za Mitaa, Sekta ya Sheria pamoja na program ya kupambana na umaskini kama vile MKUKUTA, TASAF NA MKURABITA. (*Makofi*)

Aidha, kutungwa kwa sheria mpya ya rushwapamoja na kuundwa kwa Kamati za Maadili katika Idara zote za Serikali kwa lengo la kutathimini kila wakati maadili, hali ya rushwa pamoja na kuziba mianya ya rushwa kutasaidia sana katika mapambano dhidi ya rushwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo haya ya utangulizi naomba sasa kujibu hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge. Hata hivyo, mengi yaliyoulizwa ni ushauri na mengi yametolewa ufanuzi mzuri sana na Mheshimiwa Waziri Mkuu na haitakuwa busara kiongozi wangu wa juu ameshazungumza masuala haya na mimi kuyarudia.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nianze kujibu hoja mbalimbali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuanza na Mheshimiwa John Paul Lwanji Mbunge wa Manyoni, ye ye kwanza amefurahi kwamba MKURABITA imepiga hodi Singida na kwamba kuna vijiji vimepimwa kama kijiji cha Sanjaranda na vinginevyo na wananchi wamefurahi. Lakini anatoa rai kwamba Serikali iyatarishe mabenki ili wananchi watakaopewa hati miliki za kimila waweze kukopesha bila usumbufo.

Mheshimiwa Spika, awamu ya nne ya MKURABITA pamoja na mambo mengine itashirikiana na vyombo vy ya fedha ili kuwezesha raslimali zilizorasimishwa kutumika kama dhamana ya mikopo na katika kupata fursa nyingine za kiuchumi.

Mheshimiwa Juma H. Killimbah wa Iramba Magharibi, Mheshimiwa Mhonga said Ruhwanya Viti Maalum nao pia wameshauri kwamba MKURABITA itenye fungu maalum kwa wananchi ili kupata uelewa wa kutosha ili waweze kutumia fursa hiyo vizuri kujikomboa kiuchumi. Aidha, taasisi zinazohusika na MKURATIBA zishirikiane na chombo hiki ili kuongeza ushirikiano.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mkakati wa habari, elimu na mawasiliano utaanza katika mwaka wa fedha wa 2009/2010. Utekelezaji wa mkakati huu utawezesha kutoa elimu, habari na mawasiliano kwa wananchi. Aidha, MKURABITA pia itashiriki katika maonyesho ya kitaifa ikiwa ni pamoja na maonyesho ya NANENANE. (*Makofi*)

Katika mpango wake wa kazi ambao utekelezaji wake umeanza mwaka 2008/2009 MKURABITA inashirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo Aizar ya Ardhi katika kushughulikia masuala ya urasimisha wa ardhi na biashara.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo haya ya utangulizi naomba sasa kujibu hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge. Hata hivyo, mengi yaliyoulizwa ni ushauri na mengi yametolewa ufanuzi mzuri sana na Mheshimiwa Waziri Mkuu na haitakuwa busara kiongozi wangu wa juu ameshazungumza masuala haya na mimi kuyarudia.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nianze kujibu hoja mbali mbali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuanza na Mheshimiwa John Paul Lwanji , Mbunge wa Manyoni, yeye kwanza amefurahi kwamba MKURABITA imepiga hodi Singida na kwamba kuna vijiji vimepimwa kama kijiji cha Sanjaranda na vinginevyo na wananchi wamefurahi. Lakini anatoa rai kwamba Serikali iyatarishe mabenki ili wananchi watakaopewa Hati Miliki za kimila waweze kukopeshwa bila usumbufu.

Mheshimiwa Spika, awamu ya nne ya MKURABITA pamoja na mambo mengine itashirikiana na vyombo vya fedha ili kuwezesha raslimali zilizorasimishwa kutumika kama dhamana ya mikopo na katika kupata fursa nyingine za kiuchumi.

Mheshimiwa Juma H. Killimbah wa Iramba Magharibi na Mheshimiwa Mhonga said Ruhwanya, Viti Maalum nao pia wameshauri kwamba MKURABITA itenye fungu maalum kwa wananchi ili kupata uelewa wa kutosha ili waweze kutumia fursa hiyo vizuri kujikomboa kiuchumi. Aidha, taasisi zinazohusika na MKURATIBA zishirikiane na chombo hiki ili kuongeza ushirikiano.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mkakati wa habari, elimu na mawasiliano utaanza katika mwaka wa fedha wa 2009/2010. Utekelezaji wa mkakati huu utawezesha kutoa elimu, habari na mawasiliano kwa wananchi. Aidha, MKURABITA pia itashiriki katika maonyesho ya kitaifa ikiwa ni pamoja na maonyesho ya NANENANE. (*Makofii*)

Katika mpango wake wa kazi ambao utekelezaji wake umeanza mwaka 2008/2009 MKURABITA inashirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo Wizasra ya Ardhi katika kushughulikia masuala ya urasimishaji wa ardhi na biashara.

Mheshimiwa Riziki Omar Juma, amezungumza kwamba, pamoja na kwamba ana wasiwasni kwamba, MKURABITA imefika Wete na haijafanya kitu chochote. Ningependa kutofautiana naye na kumfahamisha kwamba, kazi kubwa imefanyika huko Kiungoni Wete, Pemba na imeanza urasimishaji kama ifuatavyo:-

Mashamba 800 yametambuliwa na kuorodheshwa. Mashamba 400 yamepimwa *beacons* zimewekwa, kazi za kuandaa Hati zimeanza. Kazi hizi zimefanywa na vijana wa Shehia ya Kiungoni. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge afuatilie ataona kwamba, hayo yanafanyika.

Mheshimiwa Spika, ningependa sasa nijielekeze kwenye maswali yaliyoulizwa na michango kuhusu *TASAF*. Mheshimiwa Ramadhan Maneno, Mbunge wa Chalinze, ambaye ametoa maoni ya Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria, ameshauri kwamba, *TASAF* itenye asilimia fulani ya ziada kwenye makisio ya miradi inayohusika, ili kumudu ongezeko lolote lile la bei litakalotokea ili kukamilisha utelezaji wa miradi.

Mheshimiwa Spika, ningependa kumfahamisha kuwa, katika kutekeleza miradi inayoibuliwa na wananchi, kila Halmashauri ilitengewa mgao wa fedha zake za utekelezaji wa miradi ya jamii na kushauriwa kutenga asilimia 10 ya mgao wake kwa ajili ya kugharamia ongezeko lolote la bei za vifaa vya ujenzi, kama lingetokea. Kwa hiyo, hilo linafanyika.

Pia Mheshimiwa Lwanji, ye ye ameipongeza *TASAF* kwa kazi nzuri. Wengine walioipongeza ni pamoja na Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Stephen Galinoma, Mheshimiwa Felix Kijiko na Mheshimiwa Khadija Salum Al-Qassmy, tunawashukuru kwa pongezi zao na naamini Wabunge wengi wanakubaliana nao kwamba, *TASAF* inafanya kazi nzuri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Profesa Sarungi, ye ye alitoa maoni yake kwamba, mpango maalum uandaliwe wa kutoa taarifa kila baada ya miezi Sita, pia alizungumzia kwamba, idadi ya miradi iliyoidhinishwa Mkoa wa Mara, hususani Halmashauri ya Wilaya mpya ya Rorya ambayo katika awamu ya pili ya *TASAF* iliekezwa asilimia kubwa, miradi mipyä haikuonyeshwa katika jedwali la pili.

Ningependa nimfahamishe kwamba, *TASAF* ina mpango maalumu wa kutoa taarifa kuititia vyombo vya habari, magazeti kila robo mwaka, inayoonyesha hali ya utekelezaji kwa kila Halmashauri ya Tanzania Bara na Tanzania Visiwani. Vilevile kuhusu Wilaya Mpya ya Rorya, miradi ya Halmashauri ya Wilaya ya Rorya, imeunganishwa na miradi ya Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, kwa kuwa, Halmashauri mpya ya zimekuja baada ya kuwa mgao wa fedha za mradi zimekwisha gawiwa kwa Halmashauri zilizokuwepo na kwa kuwa, utekelezaji wa awamu ya pili ulikwishafika zaidi ya nusu ya muda wa utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, naye pia anaipongeza sana *TASAF* lakini amezungumzia kuhusu ucheleweshaji wa kuanza miradi hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mwambalaswa kwamba, ucheleweshaji unaweza kutoka tu kama matayarisho ya andiko la mradi yanakuwa na mapungufu. Hii husababisha muda mwangi kupotea hasa pale inapobidi kufanya mawasiliano na waratibu ili kasoro zilizo jitokeza zirekebishwe. Jinsi waratibu wa Halmashauri wanavyowasilisha nyaraka kamili au wanavyorekebisha mapungufu mapema ndivyo, fedha za miradi zinavyotolewa mapema. Kwa hiyo, suala hili lipo katika uwezo wenu ndani ya Halmashauri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Juma Kilimbah, naye pia alitoa maoni kuhusu mafunzo ambayo kwa kweli tunaendelea nayo. Katika uendeshaji wa miradi wanapata mafunzo. Mheshimiwa

Mwanne, alizungumzia kuhusu miradi ambayo haijakamilika. Mkakati wa kuhakikisha miradi yote inakamilika unaendelea kutekelezwa, ikiwemo kuhamasisha na kuhakikisha utekelezaji wa miradi unafanywa katika muda muafaka.

Mheshimiwa Spika, majibu mengine tutawaandikia kwa sababu ya muda naona unakimbia. Mheshimiwa Ndugai, miradi ya *TASAF* katika Wilaya Kongwa, haipo kabisa katika Bajeti. Fedha zote za utekelezaji wa miradi ya Jamii, ni \$ 120 ziligaiwa kwa kila Halmashauri. Mgao wa Wiala ya Kongwa ulikuwa ni \$ 1.059 Milion.

Mheshimiwa Spika, ningependa sasa niende kwa kifupi tu kwenye masuasla ya Usalama wa Taifa. Kambi ya upinzania kwa kupitia Mheshimiwa Grace Kiwelu, alishauri kwamba, Sheria ya Usalama wa Taifa ya mwaka 1970 na ile inayouunda Idara ya Usalama wa Taifa, zitazamwe upya.

Mheshimiwa Spika, katika mazingira ya sasa tunakubaliana naye, kuwa upo umuhimu wa kufanya mabadiliko ya Sheria za Usalama wa Taifa, ya mwaka 1970 na ile inayounda Idara ya Usalama wa Taifa ya mwaka 1996.

Mheshimiwa Shibuda, pia ametoa ushauri kwamba, kuwepo na manadiliko na hivi sasa inaadaliwa rasimu ya Sera ya Usalama wa Taifa, ambayo baada ya kupitishwa na Serikali itaweza kufanyiwa mabadiliko.

Mheshimiwa Spika, sasa niende kwenye upande wa Utawala Bora. Mheshimiwa Mohammed Habib Mnyaa, alitaka ufanuzi kuhusu fedha zinazombwa katika Ofisi ya Rais. Ningependa kumfahamisha kwamba, majukumu ya Ofisi ya Rais, ambayo yanajumuisha Ofisi ya Rais Ikulu na Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, TAKUKURU na Idara ya Usalama wa Taifa, ni makubwa na raslimali zinazohitajika kutekeleza majukumu hayo ni kubwa. Pia kiasi kilichotengwa kwa matumizi mengineyo, ni Shilingi Bilioni 165.7 ni katika Fungu 20 na Fungu 30, kwa undani zaidi nitampatia taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, alizungumzia ukiukwaji wa haki za binadamu katika Gereza la Maswa, Mheshimiwa Shibuda amelizungumzia vizuri nadhani amelijibu kwa vile yeye yuko kule. Hatua zimechukuliwa na nadhani kilichobakia ni kwamba, Wizara inayohusika nayo itafuatilia. Mheshimiwa Riziki, anazungumzia Mahakama nyingi ni chakavu, lakini anasema kuna sehemu nyingine kesi zinaendeshwa chini ya mti. Mimi kwa ufahamu wangu hakuna Mahakama zinazoendeshwa chini ya mti, najua ni kweli ziko katika hali mbaya lakini Waziri wa Sekta atawenza kutolea maelezo zaidi.

Mheshimiwa Halima Mdee, Serikali itoe maelezo kuhusu ilivyoshughulikia ugomvi wa Wafanyabiashara mafisadi wanaojiita Nyangumi.

Mheshimiwa Spika, kazi kuu ya Serikali ni kusimamia na kuhakikisha kuwepo kwa amani na utulivu nchini. Hivyo yalipotokea malumbano ya wafanyabiashara hao,

Serikali iliingilia kati na kuwataka kuacha malumbano yasiyo na tija. Maelekezo ya Serikali kwa wahusika ni kuwataka kupeleka mgogoro wao kwenye vyombo vy ya Sheria badala ya kuwavuruga wananchi kwa kutumia magazeti, na hilo limefanyika tunashukuru wametii.

Mheshimiwa Spika, naona muda wangu unakimbia, niende kwenye TAKUKURU. Mheshimiwa Grace Kiwelu, msemaji wa Kambi ya Upinzani alitaka kujua, sisi tulizungumzia pesa ambazo tumeziokoa katika uendeshaji wa kesi 515 lakini, amesema tumetumia jumla ya Milioni 24.7 Ningependa kumfahamisha kwamba, ni kweli ni gharama. Kazi inayofanywa na TAKUKURU, ni kutoa huduma. Kwa hiyo hatutegemei kupata faida. Hii ni huduma lakini tuliona ni busara kuonyesha ni kiasi gani TAKUKURU imeweza kuokoa kutokana na ufanyaji kazi wake.

Mheshimiwa Ramadhan Maneno, ametoa ushauri mzuri kwamba, TAKUKURU ibuni mbinu mpya. Tunapokea ushauri wake. Mheshimiwa Felix Kijiko na Mheshimiwa Riziki Omar Juma, TAKUKURU iendelee kubaini na kudhibiti rushwa ya mapenzi.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 25 cha Sheria ya Kuzuia na Kupamba na Rushwa, Sheria Na. 11 ya mwaka 2007, kinaipa TAKUKURU mamlaka ya kuchunguza rushwa za mapenzi kwa hiyo hilo liko katika uwezo wetu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Bujiku Sakila, nini hatima ya chombo cha TAKUKURU iwapo rushwa hapa nchini itakwisha? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, TAKUKURU haitokuwepo iwapo rushwa itaisha. Aidha, TAKUKURU imeundwa kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na.11 ya mwaka 2007, kudhibiti rushwa ambalo ni tatizo la kidunia na ipo ndani ya jamii.

Mheshimiwa Anne Kilango Malecela na Mheshimiwa Anna Komu, Serikali iandae mikakati endelevu kubaini suala la rushwa, ushauri umepokelewa na kuzingatiwa. Kwa sasa Serikali inatekeleza Mkakati wa kitaifa wa Kupambana na Rushwa awamu ya Pili (*NACP II*).

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Diana Chilolo, anasema Serikali iwe na ajira za aina mbili, moja iwe ambayo Mtumishi anajulikana kwa wenzie kwa utumishi katika kazi anayoifanya na ile ambayo hatajulikana kwa watumishi wenzi kwamba, anafuatilia masuala ya rushwa kazini. Ushauri umepokelewa. Aidha hili ni jambo la kawaida na hutumika ndani ya vyombo vyetu vya uchunguzi ikiwemo TAKUKURU.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Diana Chilolo pia amezungumzia kuhusu mfuko wa Rais wa kujitegemea (*Presidential Trust Fund*), anasema kwa kuwa sasa *PTF* inatoa mikopo mbalimbali anapenda kuishauri Serikali kuwa, mabiloni ya JK, kiasi cha fedha kipewe *PTF* ili waweze kutoa mikopo. Suala hili pia limezungumzwa na

Mheshimiwa Cellina ambaye ameonyesha fueraha yake kwamba, *PTF* wamefika Wilayani kwake.

Mheshimiwa Spika, Ofisi yangu itaufanya kazi ushauri huu ili kuwezesha Mfuko wa Rais wa kujitegemea upate mgao mkubwa kwa vile mwaka uliopita pia walipata kidogo. Mfuko huu ni mfuko ambao unajitegemea na kwa muda ulikuwa haupati hata pesa kutoka Serikali kwa sababu ni *Revolving Fund* na una maendeleo makubwa sana na ni Mfuko wa kuigwa na mifuko mingine.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi. Mheshimiwa Grace Kiwelu, anazungumzia kwamba, wapo viongozi ambao hawajazi fomu za Tamko la mali na ni hatua gani zinachukuliwa? Na wale viongozi wote ambao wameshindwa kurejesha fomu za Tamko la mali, lakini pia wakati nikijibu nitakuwa namjibu Mheshimiwa Cynithia Ngoye, ambaye ushauri wake tunauchukua na kazi hiyo ambayo ameisema inaendelea.

Mheshimiwa Spika, kutotoa Tamko la Mali na Madeni ni ukiukwaji wa maadili kwa mujibu wa kifungu cha 15 (a) ikiwa hakuna sababu za msingi za kufanya hivyo. Aidha, ni ukiukwaji wa maadili na kosa la jinai kutoa tamko la uongo. Kwa kuwa kifungu cha 15 (a) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, kinabaini kuwepo kwa sababu za msingi za kiongozi kushindwa kutoa Tamko, Sekretarieti imekuwa ikiwafutilia viongozi wasiowasilisha Tamko kwa kuwataka watoe maelezo ya kushindwa kwao kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli wapo wengi ambao hawajazi fomu na wengi ni Madiwani wetu. Kwa hiyo, sisi tukiwa sehemu ya Madiwani, tuwashauri Madiwani wajaze hizi fomu kama ni viongozi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge ya Sheria na Katiba, pia inashauri kwamba, Serikali ifanye jitihada za haraka kufanikisha ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Sekretarieti ya Maadili. Ni kweli majengo haya yamechakaa na Sekretarieti ya Maadili kwa kushirikiana na Wakala wa Majengo, imeanza mchakato wa kuandaa ramani za jengo jipya la Ofisi ya Sekretarieti.

Mheshimiwa Spika, kutokana na muda kuwa finyu, majibu mengi tutawapelekea Waheshimiwa Wabunge, wale ambao sikuweza kupata muda wa kuwajibu na niseme tu kwamba, ninaunga mkono hoja Mia kwa Mia. (*Makofi*)

**SPIKA.** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora. Sasa namwita mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejementi ya Utumishi wa Umma, Mheshimiwa Hawa Ghasia.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu,

mwingi wa Rehema kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili niweze kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, napenda nichukue fursa hii kwanza, kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii ya kujibu hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa imani yake aliyonayo juu yangu ya kunitua kuwa Waziri wa Nchi katika ofisi yake tangu alipoingia madarakani. Napenda kumwahidi kwamba, nitatekeleza majukumu ambayo amenikabidhi kwa uadilifu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, napenda nimshukuru Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa ushauri na maelekezo wanayonipatia katika kuboresha Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru wapiga kura wangu wa Mtwara Vijijini, kwa ushirikiano wao mkubwa katika kuleta maendeleo ya Jimbo. Napenda kumshukuru Baba yangu mpendwa, Mzee Abdulrahman Ghasia na Mama yangu Mpandwa, Bi.Kashu Balozi, kwa malezi yao mema kwangu.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kumpa shukrani nyingi za dhati Mume wangu Yahaya Muhata, kwa mapenzi yake kwangu na watoto na hivyo kuniwezesha kufanya kazi zangu kwa ufanisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda niwashukuru watumishi wa Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumisi wa Umma, na watumishi wote wa Ofisi ya Rais, kwa ushirikiano wanaonipatia. Shukrani za pekee kwa Bwana George Daniel Yambesi, kwa ushirikiano anaonipatia katika majukumu yangu.

Mheshimiwa Spika, pia napenda nimshukuru Mheshimiwa Sophia Simba, kwa ushirikiano lakini kwa kujibu hoja nyingi sana ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge. Mwisho naomba niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia Bajeti ya Ofisi ya Rais.

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizo, naomba niwatambue Waheshimiwa Wabunge waliochangia Bajeti yetu kama ifuatavyo:- Lakini nilikuwa naomba kwa kuwa muda ni mchache basi huu muda wa kuwatambua Waheshimiwa Wabunge, usihesabiwe katika muda wangu ambaa umenipatia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, sawa sawa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nimirambue Mheshimiwa Ramadhan Maneno, Mbunge wa Chalinze, ambaye amezungumza kwa niaba ya Mwenyekiti wa

Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Bunge. Pia nimtambue na kumshukuru Mheshimiwa Grace Kiwelu, ambaye amewakilisha Kambi ya Upinzani, kwa maoni yao na michango yao mizuri ambayo ninaamini kabisa itatusaidia katika kuboresha Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, napenda niwatambue wote ambao wamechangia kwa kuzungumza, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Stephen Galinoma, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa John Shibuda na Mheshimiwa Cynithia Ngoye.

Mheshimiwa Spika, pia napenda niwashukuru waliochangia kwa maandishi. Kwanza ni Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Severina Mwijage, Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mheshimiwa Juma Hassan Kilimba, Mheshimiwa Ramadhan Athuman Maneno, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga na Mheshimiwa Job Y. Ndugai.

Waliochangia wengine ni Mheshimiwa Stephen Galinoma, Mheshimiwa Manju S. O. Msambya, Mheshimiwa Anna Komu, Mheshimiwa Mohammed Mnyaa, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, Mheshimiwa Kaika Telele, Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge, Mheshimiwa Khadija Salum Al-Qassmy, Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda, Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Charles Keenja, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Charles Mwera, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Hemed Mohammed Hemed na Mheshimiwa Eng, Stella Manyanya.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwatambua Waheshimiwa Wabunge, waliochangia katika hotuba yetu ya Bajeti kwa kuongea na kwa maandishi. Sasa naomba kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza, ilikuwa ni kwamba, Serikali ipanue wigo wa ajira ili kutosheleza mahitaji ya watumishi katika Wizara, Idara za Serikali za Mitaa, pamoja na Taasisi za umma.

Mheshimiwa Spika, Serikali inajitahidi kuhakikisha kwamba, tunatoa vibali vya ajira vya kuhakikisha kwamba, watumishi wanaohitajika katika Taasisi za Umma, wanatosheleza. Katika mwaka 2009/2010 ajira mpya 45,568 zitatolewa.

Mheshimiwa Spika, lakini pia ningependa hapo niongezee kwamba, pamoja na kutoa vibali na nia nzuri ya Serikali ya kutaka kuongeza watumishi katika Sekta zetu kama za elimu na afya, tatizo tunalolipata ni kwamba, watumishi wa kada hizo hawapo katika soko la ajira ndiyo maana Serikali sasa hivi, iko katika jitihada za kupanua vyuo

vya sekte za elimu na afya ili watumishi wanaozalishwa kutoka katika vyuo hivyo, waweze kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, kuna suala ambalo lilizungumzwa na Mheshimiwa Riziki Omar Juma, kuhusu watumishi kuzingatia Kanuni, Sheria na Taratibu zilizopo na akatolea mfano wa askari Magereza wa kule Maswa.

Mheshiwa Spika, nashukuru kwamba, Mheshimiwa Shibuda ametusaidia kuelezea hatua ambazo zimefikiwa katika kumshughulikia mtumishi aliyehusika, na hivyo nitoe wito kwa Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu mko karibu na Watumishi wetu na Wananchi, basi yanapojoitokeza matatizo kama hayo muwe mnatupatia taarifa ili tuweze kuchukua hatua zinazostahili.

Kwa hiyo, tunashukuru sana lakini tunawaahidi kwamba, kila tutakapokuwa tunapokea malalamiko, tutakuwa tunayashughulikia kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kuna suala ambalo lilizungumzwa na Mheshimiwa Felix Kijiko, kuhusu Mwajiri aliyekataa kumlipia Mtumishi kwenda masomoni lakini pale Mtumishi alipoamua kujilipia mwenyewe wakati anakaribia kumaliza, ye ye akaamua kumfkuza kazi.

Kwa kweli tunasikitika sana na kitendo hicho, lakini kwa vile hatukijui kimefikiaje hivyo, ningependa kumshauri Mheshimiwa Kijiko, aidha awasiliane namimi, au awasiliane na Katibu Mkuu, Wizara ya Mambo ya Ndani, ili tuone jinsi ganai tunavyoweza tukalitatua suala hilo.

Mheshimiwa Spika, suala jingine ambalo limezungumzwa sana na Waheshimiwa Wabunge, ni suala zima la Watumishi wa Umma wana ndoa, kwamba, ndoa nydingi zinatengenishwa kutokana na uhamisho.

Mheshimiwa Spika, suala hili lina sura nydingi sana. Kwanza, wakati mwininge kuna tofauti ya majina, nichukue mimi mwenyewe, nilikuwa nafanya kazi na mme wangu katika kituo kimoja.

Lakini ye ye Mwajiri anamtambua mme wangu kama Yahaya Muhata, na ananitambua mimi kama Hawa Ghasia, kwa hiyo siyo rahisi Mwajiri anavyotaka kumhamisha mme wangu au mimi, akajua kwamba, hawa watu ni wawili ni wanandoa. Kwa hiyo anaweza akaanza kumhamisha mme, au kumhamisha mwanamke. (*Makof*)

Lakini wakati mwininge linakuwa ni suala la vyeo, kwa sababu unaweza ukakuta labda mwanamke umeteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya, katika Wilaya fulani, na mume wako labda ni tuseme ni Mkurugenzi katika Wilaya nydingine.

Kwa hiyo, haiwezekani likawa ni suala la wakati mmoja kwamba, Mume wako anavyoteuliwa au Mke anavyoteuliwa tu kuwa, Mkuu wa Wilaya, na huyu mwanamke atahamishwa kwa nafasi yake ya Ukurugenzi kwenda katika kile kituo kinachofuata.

Mheshimiwa Spika, lakini pia wakati mwingine ni uwepo wa nafasi ile kwa yule mtu katika eneo lile analokwenda. Unaweza ukakuta kwamba, mwanaume labda ni Mkurugenzi wa Halmashauri na Mke wake ni Mkurugenzi wa Bima ya afya.

Sasa huyu mume Mkurugenzi anahamishwa kupelekwa Mtwara, sasa Mtwara sio Makao Makuu ya Mfuko wa Bima ya Afya. Kwa hiyo, haiwezekani huyu Mke, labda umshushe cheo ili uweze kumsaidia umpeleke kwa mume wake na ukisema huyu Mwanaume akae katika eneo lile kuna kazi nyingine ambazo mtumishi hawezikuhama akapelekwa eneo jingine.

Kama Mwalimu anafundisha Sokoine huwezi kusema kama Mke wake ni Mkurugenzi, awe Mkurugenzi katika Halmashauri ile kwa miaka yote ile. Kwanza Waheshimiwa Wabunge watakuwa wa kwanza kulalamika kwamba, Mkurugenzi huyu amekaa katika kituo hiki zaidi ya miaka 20 lakini ni katika kusema hayo masuala ya ndoa.

Mheshimiwa Spika, suala jingine ni Ndoa zingine ambazo zenyewe zina migogoro. Kwa hiyo, hawa watumishi wanachukua kama njia ya kupata kuachana na wenzi wao.

Nasema hili nina ushauri na mimi mwenyewe nimeishaingilia ndoa zaidi ya Tatu. Kwanza, mtu alikuwa anaomba uhamisho kutoka Singida kwenda Mtwara, sitaji jina. Lakini wenyewe watajijua kwa ajili tu ya kumkimbia mume wake kwa sababu hana kazi na kwa mtizamo wake ye ye mwenyewe alikuwa anaona ni mzigo. (*Makofi*)

Kwa hiyo, mimi nilikataa, nikasema haiwezekani ataendelea kukaa huko huko asihamishwe na uhamisho huo ulisimamishwa.

Mheshimiwa Spika, mfano wa pili, kuna mama ambaye alinijia kabisa akiongozana na mme wake, ananiambia mme wangu yuko mko fulani, bahati mbaya ikatokea huo mko ndio ambao mimi natoka. Mimi niko Dar es Salaam, kwanini mume wangu usimhamishie karibu na Dar es Salaam ili angalau tukasaidiana kulea watoto. Nikamwambia kwamba, mko hapa wawili, mwambie mume wako aandike barua ya kuomba uhamisho ya kuelezea matatizo hayo ili niweze kumsaidia.

Mheshimiwa Spika, huu ni mwaka wa pili yule mwanaume hajaandika barua mpaka sasa hivi. Kwa hiyo, wakati mwingine naomba tusizilaumu mamlaka za ajira kwamba, tunatenganisha ndoa.

Mheshimiwa Spika, suala jingine ni kwamba, unakuta mara nyingi uzoefu wetu kwamba, watu mara nyingi wanaolewa kutokea *either* Kigoma, Mtwara au Rukwa, wakiolewa Dar es Salaam. Hatujaona mtu anayesema kwamba, mimi niko Dar es Salaam. Mume wangu yuko Mtwara au yuko Rukwa au yuko Singida naomba nimfuate huko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tusipokuwa makini lipo tatizo la kuwa na watumishi wengi mjini au maeneo yale ambayo tunayaona kwamba, yanapendwa na wengi na maeneo yale tunayoita ya pembezoni yakabaki yakiwa hayana watumishi.

Mheshimiwa Spika, ushahidi huo tumeupata wakati tunahakiki raslimali watu ili tuone je, watumishi katika Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa, wanatosheleza?

Mheshimiwa Spika, unakuta katika Wilaya moja watumishi ni wengi katika maeneo ya mijini, vijijini kuna upungufu na ukichukua mfano Dar es Salaam.

Wilaya ya Kinondoni kuna walimu ambao wamepata uhamisho kuwafuata waume zao pale, lakini hawajapangiwa shule mpaka sasa hivi kwa kuwa hakuna shule ya kuwapeleka shule zote zimejaa., walimu ni wengi kuliko mahitaji. Unakuta yaani ulinganisho wa mwalimu kwa mwanafunzi. Dar es Salaam iko moja kwa 25 wakati mikoa mingine iko mwalimu mmoja kwa wanafunzi 70, sasa hatuwezi kuiendesha nchi hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni suala ambalo lilizungumzwa na Mheshimiwa Saverina Mwijage ni suala la unyanyasaji wa watumishi kwamba wale waliopewa madaraka kuwanyanya wale walioko chini. Kwa kweli sisi kama Serikali tusingependa hivyo na kila tunapopata taarifa huwa tunachukua hatua. Mfano ambao ameutolea Mheshimiwa Mwijage yeye mwenyewe ni shahidi kwamba Mheshimiwa Rais alimchukulia hatua yule Mkuu wa Wilaya ambaye aliwapiga viboko walimu. Naomba Mheshimiwa Mwijage aridhike sana na hatua ambayo Mheshimiwa Rais ameichukua kwa kosa lile.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lwanji yeye alichangia suala la kwamba wawekezaji wa nje wanaleta watumishi wengi sana kutoka nje na kuwaacha Watanzania wenzetu walioko ndani kwa kisingizio cha lugha. Napenda nimhakikishie kwamba Serikali kwa ujumla inalisimamia kuhakikisha kwamba tunapunguza kuingiza wataalamu wa kigeni na tunayo Kamati kabisa mtu akiomba kuingiza mtumishi wa kigeni inajadili na kuishauri Serikali kama tukubali au tusikubali.

Mheshimiwa Spika, suala lingine lililozungumzwa ni suala kwamba viwango vya mishahara viongezwe na pia kumekuwa na malalamiko mengi sana kwamba Wabunge wanalipwa mishahara mingi kwa nini hiyo mishahara isipelekwe wakaenda kuongezwa labda watumishi wengine. Ningependa wananchi waelewe kwamba mshahara wa Mbunge ni sawasawa na mshahara wa Mkuu wa Wilaya. Mishahara yote ya Wabunge wote ni asilimia 0.4 ya mshahara wa watumishi wanaolipwa katika Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, lakini ukichukua mshahara wa Wabunge na maslahi ya Wabunge yote ukayaweka pamoja unakuta bado haifiki hata asilimia moja ya mishahara. Nikajaribu kuangalia hivi tukisema tuwaondoe Wabunge wasilipwe chochote mwaka huu halafu tuwaongeze mishahara kima cha chini kitaongezeka kwa asilimia ngapi. Ujisema uchukue mishahara itaongezeka kwa asilimia moja.

Kama tutasema tuchukue na maslahi yao yote Waheshimiwa Wabunge tuseme mwaka huu Waheshimiwa Wabunge fanyeni kazi msilipwe hata senti tano tutaongeza asilimia 2 tu ya mshahara kwa kima cha chini amba ni sawa sawa na shilingi ngapi kwenye shilingi laki moja asilimia 2 ni shilingi ngapi. Kwa hiyo, naomba tujue kwamba kwa kweli si kwamba kima cha chini hawalipwi vizuri kwa sababu wanalipwa Wabunge, ni uwezo wa Serikali.

Serikali ina nia nzuri sana ya kuongeza kima cha chini cha mshahara na tumekuwa tukifanya hivyo, lakini pia wananchi wafahamu majukumu waliyonayo Waheshimiwa Wabunge. Kimbilio lao katika hali ya kawaida wananchi wanajua na sisi wenye tunajua. Mwananchi akipata shida mtu wa kwanza kumkimbilia sio Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi na wala sio Afisa Mipango ni Mbunge. Wabunge ndio wanaolipa ada za shule za wanafunzi, ndio wanaotibia wagonjwa, ndio wanaofanya kila kitu. Ndio kimbilio la kwanza kwa wananchi wa kawaida. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kuna suala limetolewa mchanggo kwamba pia kuna suala la watumishi kukaa katika kituo kimoja. Ni kweli tumeliona na Serikali mara nyingi imekuwa ikijitahidi kuhakikisha watumishi wanahamishwa mara kwa mara kupelekwa katika maeneo mengine, lakini tunapatwa na vikwazo. Kikwazo cha kwanza uhamisho ni gharama, kwa hiyo tusingependa uhamisho uende mara kwa mara. Ninji wenye mnasikia kila siku fedha ambazo walimu tukisema tunalipa sasa hivi fedha za uhamisho unakuta ni fedha nyingi sana na ndiyo maana sasa hivi tunesema mtu asihamishe mtumishi mpaka fedha iwe imetengwa kwenye bajeti na tumehakikisha mwaka huu kwamba uhamisho, matibabu kama alivyozungumza Mheshimiwa Kombani vyote vimezingatiwa katika Bajeti.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya pili tunayoipata wakati mwingine mtumishi amekaa katika kituo kimoja miaka 15 ukimhamisha wakati mwingine unaweza ukakuta Mkuu wa Wilaya ile, Mkurugenzi, Mheshimiwa Mbunge anakuja anasema msituondolee huyu ndiye mtumishi wetu mzuri. Sasa wakati mwingine unafika mahali unachanganyikiwa. Huku unaambiwa amekaa muda mrefu na wakati mwingine unaweza ukakuta jimbo moja lina Wabunge wawili, mwingine anakwambia amekaa muda mrefu muondoe, mwingine anasema ukimwondo huyu tutamalizana Bungeni.

Mheshimiwa Spika, hizo ndizo *challenge* tunazozipata. Kwa jimbo lile lenye Mbunge mmoja wakati mwingine unaweza ukamwelewesha na akakuelewa, lakini wanapokuwa wawili au watatu kuwaweka pamoja wakawa na lugha moja nayo pia ni ngumu.

Mheshimiwa Spika, kuna suala ambalo ulilisema kwamba taarifa zetu zinasema walimu 38,000 walipandishwa vyeo na kwamba katika Bajeti tulitenga shilingi bilioni 43,000,000,000 lakini Chama cha Walimu kinasema kwamba walimu 60,000 ndio walistahili kupandishwa vyeo. Je, matumizi ya hizo fedha shilingi bilioni 43,000,000,000 yamekwenda wapi?

Katika wale walimu 38,000 ambao mwaka jana tuliwaweka kwenye Bajeti tuwapandishe vyeo. Kwa kweli tuliwapandisha walimu 43,575 isipokuwa fedha hatukutumia zote shilingi bilioni 43,000,000,000 badala yake tulitumia bilioni 42,000,000 kwa sababu baadhi ya walimu hatukuwakuta wale ambao tuliowapandisha vyeo wengi wao walikuwa wamefariki hata kabla ya hivyo vyeo havijapendekezwa, wengine walishaacha kazi. Wengine yaani hawapo kabisa unawatafuta kila mwajiri anakwambia huyo mtu simtambui.

Lakini bado suala la kupandisha vyeo walimu waliolundikana katika kituo kimoja linaendelea, si suala la kwamba ukipandisha leo vyeo unakaa kwa sababu watumishi wanaajiriwa siku tofauti, miezi tofauti. Kwa hiyo, kila mwaka tutakuwa tukipandisha walimu vyeo.

Lakini tatizo kubwa tulilolipata kuna kipindi nchi yetu ilisimamisha kuajiri kwa muda mrefu vyeo watumishi walikuwa hawapandishwi lakini pia kulikuwa na mabadiliko ya miundo ya watumishi. Kwa hiyo, kutokana na hivyo sio suala kwamba watumishi ambao hawakupandishwa vyeo kwa miaka zaidi ya 10, 15 kwamba kazi hiyo utaweza ukaifanya kwa siku moja.

Mheshimiwa Spika, niko pamoja na watumishi wa umma kuhakikisha wanapandishwa vyeo kwa wakati na tumesema lazima waweke katika Bajeti zao. Mimi nilikuwa ni mtumishi mwenzao nisingependa katika kipindi changu mtumishi yoyote wa umma anyanyasike. Kwa hiyo, nalisimamia kwa hali na mali.

Mheshimiwa Spika, suala la *extra duty allowance*, posho ya kazi maalum kwamba kwa nini hiyo posho isiongezwe kwenye mishahara. Kazi maalum si watumishi wote wanaofanya kazi maalum na si za muda wote mara nyingi hizi kazi maalum ni za vipindi maalum na mara nyingi unataka hiyo kazi iishe kwa kipindi kile kile ulichokusudia kiishe. Kwa hiyo, wakati mwingine unakuta watumishi wanafanya kazi zaidi ya ule muda unaotakiwa na wakati mwingine anakwenda kazini Jumamosi mpaka Jumapili.

Mheshimiwa Spika, nichukue tu mfano mdogo, sasa hivi tuko katika kupitisha Bajeti zetu tunao watumishi hapa. Tunao Makatibu Wakuu, Wakurugenzi, Masekretari na watumishi ambao wametoka Dar es Salaam kwa ajili tu ya kushughulikia hii Bajeti yetu wakimaliza warudi. Tuchukue tu mfano wa jana Waheshimiwa Wabunge wamemaliza kuchangia tulivyoondoka wengine tumekwenda kubadilisha nguo, tumekwenda kuburudika kwa Mbilia Bell. Lakini watumishi wa Ofisi ya Rais walikuwa kwenye ukumbi wa Pius Msekwa mpaka saa 6.00 za usiku na kuna watumishi ambao

mimi juzi tumelala saa 8.00, siku ya pili tumelala saa 5.00, siku iliyofuatia tumelala saa 6.00 tukijiandaa na Bajeti hii hivi ni kweli huyu mtu useme asilipwe chochote. (*Makofi*)

Katika hali ya kawaida Waheshimiwa Wabunge wanawauliza kweli wafanye kazi kwa zaidi ya masaa hayo anasikia kabisa Mbilia Bell huku anatumbuiza yeye bado yuko kwenye kompyuta kule halafu atoke umwambie bwana mshahara ni ule ule. Kwa kweli tutakuwa tunawakatisha tamaa watumishi na hizi kazi zetu zitakuja nusu nusu hapa.

Mheshimiwa Spika, mwenyewe jana kuna mtumishi mmoja alikuwa anakuja ananiambia naomba nikupitishe kwenye yifungu vitoke sawa nikamwambia tutakufa. Twende kule kwa Mbilia Bell tukirudi tutakuja kukesha na kweli tulikesha tumelala saa 7.00 baada ya kutoka kwa Mbilia Bell. Sasa naomba Waheshimiwa Wabunge waelewe kwamba hizi *extra duty allowance* na posho maalum zina sababu maalum na ndizo zinazofanya kazi mnazoziona zinakwenda. (*Makofi*)

Pia suala lingine ambalo limezungumzwa kwamba suala la semina, makongamano ni kweli Mheshimiwa Waziri Mkuu. Hakusema kwamba Makongamano kila kitu kifutwe, alichosema ni lazima tuombe kibali kwake tuangalie kama hicho kitu kina tija. Kuna mikutano mingine, kuna semina zingine haziwezi kuepukika kwa ajili ya kuboresha utumishi wetu.

Mfano katika Ofisi yangu ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma tuna mikutano ya Wakurugenzi wa Idara anayoshughulikia masuala ya rasilimali watu, tuna mikutano ya Makatibu Tawala ya kila mwaka ile ndiyo tunafanya tathmini. Je, katika huu mwaka mambo gani mimi kama Waziri nimeyaona kama Makatibu Wakuu wangu wameyaona. Kwa hiyo, ile ni mikutano kwa kweli ni ya kuboresha yale ambayo yanakusudiwa katika Utumishi wa Umma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna suala la Prof. Sarungi amesema suala la miongozo ya kushughulikia malalamiko kwamba iwafikie katika Taasisi, ni kweli tutahakikisha tunasambaza tulikuwa tunafanyia baadhi ya Wizara tu kama majoribio na sasa hivi tumesharekebisha kila kitu. Kwa hiyo, miongozo itasambazwa na elimu itatolewa kwa watumishi wetu wa umma ili waweze kuwashughulikia wananchi ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Kaka yangu, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga na Mheshimiwa Mama Mwanne Mcemba wamezungumzia suala la Chuo cha Utumishi wa Umma cha Tabora kwamba majengo yale yakarabatiwe. Napenda niwahakikishie kwamba mwaka huu tumetenga shilingi 600 milioni kuhakikisha kwamba kile chuo kinaboresha na pia Mheshimiwa Siraju ameomba kwamba Makao Makuu ya Chuo cha Utumishi wa Umma yahamishiwe Tabora, ombi tumelipokea naomba utuachie tutafakari.

Mheshimiwa Spika, pia tumeambiwa kuangalia suala la muundo wa Tume ya Mipango na kama tujaribu kujifunza kutoka maeneo mengine tuone kama ule muundo tulioupitisha kama unakidhi haja iliyokusudiwa. Napenda niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba muundo ule tumeufanyia utafiti na kwa mahitaji ya sasa hivi unakidhi.

Lakini ushauri tunaupokea na kwa kawaida muundo ukishatengenezwa sio kwamba haubadiliki mnaufanya mapitio kuangalia je kwa mahitaji ya kila muda uliopo unakidhi haja. Pale unapouona kwamba bado una mapungufu huwa tunabadilisha. Ndio maana kila mwaka na kuna Idara katika Ofisi yangu kazi yake ni kupitia miundo ya Wizara na kila mwaka Wizara ikiona ule muundo kwamba kuna vitu haviendi kwa sababu ya muundo au kuna kazi zimeongezeka huwa wanaleta mapendekezo kwetu na tunaupitia na tunaubadilisha. (*Makofī*)

Mheshimiwa Spika, kuna suala la pensheni kwa Waheshimiwa Wabunge kwamba kwa nini wasipewe pensheni. Mheshimiwa Waziri Mkuu alilieleza vizuri na kwamba pendekozo hilo limepokelewa. Kuna vitu tunavyoviangalia kwanza ni sababu zilizofanya utaratibu huo uondolewe kwa sababu ulikuwepo huko nyuma. Lakini pia vipindi nya kazi nya kazi ya Mbunge na pia tunaangalia umri wenyewe wa Wabunge kwa sababu wengine walishafanya kazi wakastaifu wengine wana pensheni zao si vizuri mtu kuwa na pensheni mibili ingawa tunaweza tukawa na muundo huu tukawa na pensheni mtu akachagua kama vile ambavyo mtu anawenza akawa Mbunge na akawa Mkoo wa Mkoa halipwi mishahara miwili anachagua mshahara upi analipwe.

Kwa hiyo, hata Waheshimiwa Wabunge wanaweza wakaamua kuchagua pensheni ipi anaitaka ile aliyokuwa nayo akiwa mtumishi au hii ya ubunge. Kwa hiyo vyote hivyo tunavifanya kazi, naomba tu Waheshimiwa Wabunge watuachie. (*Makofī*)

Mheshimiwa Spika, kuna suala la watumishi wa zamani wastaifu kwamba pensheni ni ndogo. Ni kweli pensheni ya zamani ni ndogo na hiyo ilitokana na kwamba mishahara yenye we waliokuwa wamechangia kwa kipindi hicho ilikuwa midogo pia. (*Makofī*)

Lakini tunaliangalia kuhakikisha kwamba kadri uchumi unavyoongezeka tunaboresha na kwamba sasa hivi imeongezwa hadi kufikia Shilingi 50,114/= kwa mwezi kuanzia mwezi Julai, 2009. (*Makofī*)

Mheshimiwa Halima Mdee alizungumzia kwamba wewe ndio unaoshughulikia wastaifu. Kwa kiasi kikubwa wastaifu wale wako kwa Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Mkulo. Wastaifu ambao nawashughulikia ni 12 tu ambao ni Marais Wastaifu, Makamu wa Rais Wastaifu na Mawaziri Wakuu Wastaifu na wajane wa wale viongozi ambao sheria inawazungumzia. Kwa hiyo, pale ukiona vitu vyovoyote vinavyohusu Wastaifu kwenye Bajeti yangu, ni viongozi hao tu na siyo wale wengine.

Mheshimiwa Spika, muda kama unavyoona pia ni mdogo. Lakini Waheshimiwa Wabunge wajue kwamba mambo yao mengi tumeyajibu na watapewa kwa maandishi, lakini kulikuweko na suala la watumishi kwamba tunachelewesa vibali nya watumishi vitoke kwa haraka hasa watumishi wa sekta ya Afya na Walimu.

Napenda niseme kwamba vibali vya walimu mara tu vikiombwa na hasa sekta za afya sasa hivi na Wahasibu na Kilimo huwa tunapeleka kwenye sekta husika. Zile sekta kwa sababu hatuhitaji wafanye ushindani wowote, ila wanachotakiwa ni kuwapangia tu. Isipokuwa tunaweza tukakupa kibali leo lakini hao walimu wenyewe au Madaktari wako chuoni. Kwa hiyo, itakuwa mpaka watakapomaliza mafunzo ndiyo ile Wizara husika inawapangia, lakini sisi tunatoa kwa wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna suala la kukaimu Wakuu wa Idara hasa kwenye Halmashauri. Hili suala tumeshawakabidhi TAMISEMI wana madaraka yote hata Wakurugenzi wana mamlaka ya kuwathibitisha wale wanao kaimu. Lakini tatizo maeneo mengine wale wanao kaimu wengi hawana sifa au pale wanapokaimu hawaonyeshi uwezo kwamba wakipewa ile nafasi wataiweza. Kwa hiyo mara nyingine unaona akaimu wakati unamtafuta mtu mwingine wa kuja kufanya ile kazi.

Mheshimiwa Spika, suala lingine lililozungumzwa ni kwamba hizi nafasi za Wakurugenzi au nafasi nyingine kubwa zitangazwe badala ya sasa hivi kuwateua kama tunavyofanya. Ni kweli ziko faida za Wakurugenzi wa Halmashauri au Wizara kuwa na ushindani na utaratibu huo ulikuwa ukifanyika tumeusimamisha kama miaka miwili au mwaka mmoja uliopita, baada ya kuona kwamba hasara ni nyingi zaidi kuliko faida. (*Makofi*)

Kwanza ilikuwa inawakatisha tamaa wale waliokuwepo katika Utumishi wa Umma. Unakuta mtu ameanzia kazi Serikalini anafanya ile kazi ameweza amesota inapofika sasa nafasi ya Ukurugenzi mnatangaza anakuja mtu kutoka katika sekta binafsi anaomba na anakuja anafanya kazi. Lakini kwa vile hakuzoea kufanya kazi Serikalini unakuta utendaji wake nao pia hauridhishi. Kwa hiyo, tuliona faida ni chache. Lakini kwenye zile Taasisi uwakala kwa sababu tunafanya kazi kwa mikataba hizo tunaendelea kuzitangaza na wanachaguliwa watu kwa ushindani.

Mheshimiwa Spika, nadhani mengi nimeyazungumza na sasa hivi hata nikisema nikimbie kwa *speed* ipi kwa kweli sidhani kama nitaweza kuyalipa. Lakini suala lingine ambalo nilitaka nilizungumzie ni suala la watumishi kucheleva kupata mishahara yao pale wanapoajiriwa na pia kucheleva kubadilishiwa mishahara yao pale wanapopandishwa vyeo.

Hili tatizo tumeliona na tunachokifanya sasa hivi ni kwamba mitandao yetu ile tunayotumia katika kuingiza watumishi kwenye mishahara, kurekebisha kwa kweli imepitwa na wakati. Sasa hivi tunahama kutoka *Lawson Version seven (7)* kwenda *Version nine(9)*. Hii itatusaidia mwajiri mwenyewe badala ya kubebe makaratasii kuleta Utumishi sasa atawenza kumjazia akiwa kule kule kwenye Wilaya yake na siku ile ile ambayo anaingiza kwenye ule mtandao Utumishi tutaona tutaweza ku-*approve* siku hiyo hiyo na itaweza siku hiyo Hazina wakaiona na Utumishi tunaweza kufanya hiyo shughuli ikafanyika kwa muda wa siku moja.

Pia hiyo *version* itawezesha yaani utakuwa unaweka kwenye ile *payroll* jina na cheo chake, ukiweka na tarehe yake ya kuajiriwa basi itarekebisha pia na mshahara wake

wa nyuma. Itakuwa imemwingizia moja kwa moja. Sasa hivi tuko katika hatua za mwisho za mikataba na Benki ya Dunia wanatusaidia suala hilo tukishamaliza Mheshimiwa Spika nakuhakikishia kwamba mtumishi ataajiriwa mwezi huo huo na atapata mshahara wake mwezi huo huo na kama ikishindikana hivyo tutakuwa tunawenza kujua ni nani amesababisha asipate huo mshahara. Ni mwajiri hakuingiza jina au Utumishi hatuku-*approve* au Hazina wenyewe hawaku-*forward* yaani itakuwa inajitengeneza yenyewe *payroll*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nadhani mengi sana amenijibia Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora. Naomba baada ya hayo Waheshimiwa Wabunge waridhike kwamba ambao sikuwataja majibu nimeyajibu yote na kwamba tutakuja kuwapa kwa maandishi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

## KUHUSU UTARATIBU

**SPIKA:** Kuhusu utaratibu Mheshimiwa Killimbah, Kanuni ipi?

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana,

**SPIKA:** Taja Kanuni.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Kanuni ya 68 kifungu cha Kwanza.

**SPIKA:** Hiyo ni Mwongozo wa Spika.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Naomba Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Endelea endelea.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika,

Katika hotuba zilizotolewa hapa tangu jana ni hotuba za Wizara mbili, Wizara ya Menejimenti na Utumishi wa Umma na pia imetolewa hotuba ya Ofisi ya Rais Utawala Bora. Lakini katika muda wa kutoa majibu kwa kadri ninavyoelewa bahati nzuri mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama na pia Ofisi ya Rais, Utawala Bora inahusika na Kamati yetu.

Katika kutolewa majibu Waziri wa Utawala Bora amepewa dakika 15 tu jambo ambalo naona ni tofauti na kanuni kama inavyoagiza kuhusiana na Waziri anatakiwa apewe muda wa saa moja kujibu hoja. Sasa nilikuwa naomba Mwongozo wako kuhusiana na hii kwa sababu Waziri Ofisi ya Rais Utawala Bora anazo Idara zipatazo

karibu 8. Kwa hiyo, yeye amepewa kama Idara kuweza kujibu hoja. Ahsante sana.  
(*Makofii*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge ufanuzi ni kama ifuatavyo. Inapokuwa imeandikwa hotuba moja muda unagawiwa kama tulivyofanya, tofauti na kuja ni kama vile wakati wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI naye alisoma hotuba yake, sasa hapo muda unaangaliwa tofauti. Tungeweza kabisa kwa mwaka ujao tukaangalia namna ya kuweza kubadili hilo, ili kumpa nafasi zaidi pia Waziri wetu wa Nchi, Utawala Bora.

Ila tunapoendesha hapa mambo msidhani hatuoni hayo wale ambao wangkuwa wanatazama saa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora ingawa nilitamka anapewa dakika 15 saa ilirudishwa nyuma. Sasa hii mnapelekwa jikoni kuona baadhi ya mambo huwa tunafanya hapa, lakini inabidi niseme kwa sababu huwa haipendezi kumgongea Waziri yoyote kengele ya pili, kwa hiyo mtaona kwamba badala ya dakika 15 kwa mujibu wa Makatibu hapa walivyonieleza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Utawala Bora alizungumza kwa dakika 23 sio 15. Ahsante sana.  
(*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge hoja iliyopo mbele yetu ya Bunge kukubali kupitisha Makadirio ya Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma ambaye inajumuisha pia Utawala Bora.

Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Kwa mujibu wa Kanuni inabidi tupitie hatua nyingine ili tuweze kuiamua. Kwa hiyo, sasa nitamwomba Katibu atutangazie hiyo hatua.

### **KAMATI YA MATUMIZI**

### **MATUMIZI YA KAWAIDA**

### **Fungu 20 - Ofisi ya Rais Ikulu**

Kif. 1001 – *Administration and General...* ...Shs. 7,229,345,000/=

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatumia kifungu hiki cha Programu ya 10 ili niweze kupata ufanuzi nitasimamia pale kwenye mshahara wa Waziri, lakini si kwa dhamira ya kuushika mshahara huo.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa niwakumbushe tu, samahani, Waziri wa Wizara hii ni Rais mwenyewe. Kwa hiyo msijaribu hapa mshahara maana mtakuwa mnajaribu kuchukua mshahara wa Rais, haiwezekani hiyo. Hawa ni Mawaziri wa Nchi, kwa hiyo mnachotakiwa kufanya ulenge vizuri sana kwenye *sub votes*, zipo tu, someni muangalie,

nitakupa dakika 2 Mheshimiwa Kaboyonga uangalie angalie hapo. Nikusaidie ni suala lipi?

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Suala la msingi Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kupata tu ufanuzi kuhusu pendekezo nililoipa Wizara kwamba tunategemea sana Bajeti kwa maana ya *allocation* ya Bajeti kufanya mambo yetu. Pale Tabora kuna Chuo cha Utumishi, chuo kile kinalipisha karo. Kwa hiyo, kina pato la kutosha..

**MWENYEKITI:** Kama ni hivyo basihapa siyo penyewe zungumzia kwenye *training domestic* 2208 aah!!! liko kwenye 32 hilo basi usubiri. Nimeshauriwa kumbe hapa ni mambo ya Ikulu tu hapa, subiri kwenye fungu 32.

(*Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote*)

### **Fungu 30 – Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri**

Kif. 1001	<i>Administration and General</i>	Shs 154,042,106,700/-
Kif. 1002	<i>Finance and Account</i> .. . . .	Shs 510,832,500/-
Kif. 1003	<i>Policy and Planning</i> .. . . .	Shs 503,727,700/-
Kif. 1004	<i>Internal Audit Unit</i> ... . . .	Shs 369,238,300/-
Kif. 1005	<i>Management Inf, System Unit</i> ...	Shs. 348,920,000/-
Kif. 2001	<i>Cabinet Secretariat</i> .. . . .	Shs 1,206,939,000/-
Kif. 2002	<i>Government Communication</i> ..	Shs. 419,773,700/-
Kif. 2003	<i>Good Governance</i> .. . . .	Shs 493,241,400/-
Kif. 2004	<i>Public Service Appeal</i> ... .	Shs 315,125,900/-
Kif. 2005	<i>Public sector Reform Coordination Unit</i> .. . . .	Shs 300, 920,800/-

(*Vifungu Vilivyotajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Madaliko yoyote*)

### **Fungu 32 – Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.**

Kif. 1001	<i>Adm and Human Resources MGT.</i>	
Division	.....	.....Shs 11,709,977,200/-

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge labda niwafahamishe kwamba, Mheshimiwa Waziri Mkuu yupo Dar es Salaam kwa udhuru maalum na amemwachia shughuli za Serikali ndani ya Bunge Mheshimiwa Mohamed Seif Khatib. Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed Kiongozi wa Kambi ya Upinzani amesafiri kwenda Zanzibar amemwachia shughuli za kuongoza Mheshimiwa Salim Hamis Hemed bahati mbaya

naona huyu Mheshimiwa Salim kama hajazoeazoea mambo haya. Kwa sababu badala ya kuwepo hapa anatokatoka tu.

Kwa hiyo, nadhani baadaye Mheshimiwa Mnyaa mfahamishe Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed kwamba labda atazame uteuzi wake upya maana yake ukimwachia mtu ambaye hata kwenye Kamati ya Matumuzi hayupo sasa inakua matatizo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Kaboyonga tuendelee.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu inasimama kwenye *training* na hususan *training* kwa maana ya Chuo chetu cha Utumishi cha Tabora.

Nilitaka ufanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri ni kwamba katika ushauri wangu nimesema hivi, tusitegmee *budget allocation* kwa ajili ya maendeleo ya pale chuoni. Kwanini tuisitumie utaratibu wa kukopa hasa tukizingatia kwamba Chuo kile kinaijidesha kwa njia ya karo. Karo zile zinaweza kulipia madeni hayo.

**MWENYEKITI:** Samahani Mheshimiwa Kaboyonga, uzuri wa hapa kwenye 32 hoja yako inakuja programu ya 30. Nimearifiwa na Sekretarieti hapa. Ukurasa wa 111 nitakuruhusu usimame hapo, hicho Chuo cha Tabora, ndiyo mahali pake hapo.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na nishukuru nafasi hii niwapongeze kwa kujibu hoja za Wabunge nikianza Mheshimiwa Sofia Simba Mwenyekiti wa UWT wa Taifa letu lakini na Mheshimiwa Hawa Ghasia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hapa kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu jana alihitimisha hoja yangu ambayo nilitoa wakati nachangia hotuba yake inayohusu watumishi katika Halmashauri yangu.

Namshukuru Waziri Mkuu kwanza kabisa alikubaliana nami kwamba tatizo hili kwa kweli ni la muda mrefu toka kipindi akiwa Waziri wa TAMISEMI lakini baadaye alithibitisha kwamba wale watumishi wote niliokua nawasemea bahati mbaya sana wote ni watumishi ambao wanaelimu ya darasa la saba. Kwa hiyo hoja ile haikua na msingi sahihi wa kuwashughulikia kwa sababu hawajakidhi vigezo vya kimiundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe uthibitisho wa hoja yangu kama Mbunge wa Jimbo nikiwakilisha wale wananchi na watumishi hao nilikua makini na hivyo nilipokuwa nawakilisha hoja ile nilikua sahihi kabisa nikiwa na vielelezo. Nitaomba nikabidhi mbele yako vyeti vya Mtendaji mmoja ambaye anaitwa Nd. Hamis Lwambano, amemaliza kidato cha nne akiwa na *division two* amemaliza kidato cha sita akiwa na *division four* lakini pia ana-Diploma ya Takwimu kutoka Chuo cha Takwimu cha Afrika Mashariki kilichopo Dar es Salaam. Huyo ni mmoja katika hao watumishi niliokua nawazungumza. Naomba ushahidi huu nitaukabidhi kwako, lakini mwingine

amemaliza pia kidato cha nne anaitwa Canisius Lingoye, kamaliza shule ya Sekondari Kigonsera Wilaya Mbanga mwaka 1993 shule ambayo viongozi wengi wa taifa hili wamesoma pale.

Kwa hiyo huo ni ushahidi wa kwanza wa kuthibitisha kwamba hoja yangu ilikuwa na msingi halali. Hivyo nitaomba pia nikabidhi ahadi niliyopewa ya kushughulikia suala hili ninayo hapa, nitaomba pia nikabidhi Waraka wa Utumishi unaowazungumzia hata wale wa darasa la saba ambao unasema kwamba kama walishapata mafunzo yanayoendana na ajira walizonazo wana haki ya kuajiriwa kwa mujibu wa Waraka wa Utumishi wa mwaka 2002 pamoja na Waraka wa Utumisi namba moja wa mwaka 2004 na Waraka huo ultolewa tarehe 10 Aprili, 2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Waziri akubali tu kwamba hawa ambao tayari wanavigezo wanahaki ya kuajiriwa kwa kuwa wana sifa zote za kimiundombinu na wale ambao wanaona kwamba bado hawana sifa na kwa kuwa wanaendelea kuijendeleza na wengine wamekwisha jiendeleza kwa mujibu wa waraka ninaomba waingizwe kwenye *Payroll* kama nilivyoomba wakati nachangia hotuba ya Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupatiwa maelezo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli hao watu wamekaa muda mrefu tangu walipoajiriwa mfano nikimchukua Mariam Z. Mbawala cheo kilichooneshwa hapa anaomba aingizwe kama Mhasibu Msaidizi lakini kumbukumbu ambazo ziko katika Ofisi yetu zinaonesha bado ni darasa la saba na aliajiriwa mwaka 1980 wakati huo kwa kumbukumbu tu za Waheshimiwa Wabunge mimi nilikua darasa la tano shule ya msingi. Kwa hiyo, kuchelewa kwake kuingia kwenye *payroll* kwa kweli naomba kwa kiasi kikubwa nisibebeshwe sana mzigoto, wabebeshwe waliokuwepo tangu mwaka 1980 Mawaziri wenzangu, Wakurugenzi waliokuwepo katika Halmashauri, Waziri aliyekuwepo TAMISEMI wakati huo sijui kama ilikuwa inaitwa TAMISEMI na Mawaziri waliokuwepo Utumishi bahati nzuri ukifika pale orodha inaonekana ni wangapi wapo. Lakini pia niseme kwamba suala hili nilijitahidi sana kulishughulikia na nilijitahidi sana kuzungumza na Mheshimiwa Mbunge.

Ninao mashahidi Mheshimiwa Job Ndugai amenisaidia sana kumuelewesha sana Mheshimiwa Mbunge, kwamba naomba atuachie ili hili suala tulishughulikie kwa sababu ni la muda mrefu na tayari mimi na Waziri wa TAMISEMI tulishakubaliana kwa sababu wako watumishi zaidi ya 1900 ambao wana matatizo yanafanana na haya ambayo tulisema tukae tuone tunaweza tukalimaliza. Kama hatuwezi tuwashauri wawape viinua mgongo vyao waondoke na kikao hicho tulikubaliana baada ya bajeti ya Mheshimiwa Kombani na Bajeti yangu kupita kwa sababu Katibu Mkuu wangu na Katibu Mkuu wa TAMESEMI na Waziri wa TAMISEMI watakuwa hapa. Nikamwomba Mheshimiwa Mbunge nipe muda lakini alisema hawezi kunipa muda hata wa dakika mbili.

Sasa kama aliweza kuwa na subira ya miaka 20 yote hiyo alishindwa nini kuwa na subira na mimi ya siku tatu ambayo ni leo kama Bajeti yangu ingepita ijumaa? Lakini hata hivyo kwanini hawa watumishi mpaka leo hawajaingia kwenye *payroll* pamoja na hizo sifa alizozisema?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ili mtumishi aweze kuingia kwenye *payroll* ni lazima hiyo nafasi inayoombwua iwe imewekwa kwenye ikama. Hizi ni pesa tunaposema kuajiri ni sawasawa na vile ambavyo unasema unajenga barabara. Kwa mwaka unasema utajenga barabara tatu kwa shilingi milioni 10 na watumishi unasema utaajiri watumishi 45, lazima utengenee Bajeti. Unapoajiri zaidi ya 45,000 kuna watumishi watakosa mishahara kwa sababu pesa haipo.

Kwa hiyo, ni lazima kibali kipatikane. Sasa suala jingine, pamoja na kuwa tunatoa kibali ni lazima tunayempa kibali azingatie taratibu, sheria, kanuni zilizopo; kwamba lazima anaowaajiri aangalie sifa kama wanazo. Lakini pia pamoja na kuwa na sifa siku hizi wenye sifa ni wengi. Kwa hiyo, tunataka watu washindanishwe ili kweli yule mwenye sifa haswa ndiyo achaguliwe. Sasa hivi tunazo Sekondari kila kata hivi ni sahihi kumchukua mtu wa darasa la saba akawe Mtendaji wa Kata kwenye Kata ambayo wananchi wake baada ya miaka miwili wenye elimu ya kidato cha nne watakuwa wengi?

Ni kweli ametoa ushahidi amewataja wachache, amemtaja Luambano, amemtaja Khalifa lakini yupo Feloteo Mhagama, yupo Teophenos Mrema mbona wale wengine hajaniambia kama wanazo hizo sifa.

Lakini pamoja na kuwa na sifa siku ya tarehe 22 baada ya kuwa nimemsihi sana Mheshimiwa Mbunge kwamba anipe muda suala lake nalishughulikia na kwamba si lake peke yake, alivyosema hanipi hata dakika mbili atafanya anachokifanya na kweli alikifanya kwa sababu alisema amezungumza kwa mara ya mwisho.

Niliwasiliana na Katibu Mkuu wangu tarehe 22 mwezi wa sita nikamwambia naomba ulifuatilie hili suala na unipe majibu kwanini hawa watu hawajaingia kwenye *payroll*? Akaniambia kwamba alimwandikia barua Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea Vijijini Mr. Mruma. Tarehe 3/5/2007 akimwomba ajibu hoja ambazo ofisi yetu ilihoji; ili mtu aingizwe kwenye *payroll* lazima kuwe na vielelezo. Sasa hivyo vielelezo vilikua havipo, lakini pia kulikuwa na masuala ya utata ya kama je kuna kibali, wameshindanishwa au kuna vitu gani.

Lakini tangu tarehe 5/5/ 2007 mpaka tarehe 22/6/2007 ambapo Katibu Mkuu wangu aliongea kwa simu na Mkurugenzi wa Songea vijijini kumwuliza kwanini hajajibu hiyo barua ya tarehe hiyo. Akasema ameshindwa kujibu hizo kwa sababu watumishi hao hawana sifa.

Mheshimiwa Spika, kama ungekuwa wewe ni Waziri katika mazingira kama hayo unafanyeje kazi. Kwa sababu mimi nafanya kazi kwa kushirikiana na Katibu wangu na Katibu Mkuu wangu anafanya kazi kwa kushirikiana na Wakurugenzi walioko kule. Sasa

kama hawatupi ushirikiano. Mimi naomba niishie hapo, Mheshimiwa Waziri Mkuu amejibu, sina ufanuzi zaidi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa kweli umetoa maelezo ya ziada marefu lakini mimi ninavyoliona sasa; alichoomba Mheshimiwa Mbunge sasa hivi ndicho kinatushughulisha hapa.

Mheshimiwa Mbunge alichoomba mtazame upya wale wenye sifa ambao ameleta vielelezo hivi na mimi nitawafikishieni muone sasa haki itendeke na wale wanaoangukia katika ile secular ya Serikali sijui ya mwaka gani ambayo inasema wale wa darasa la saba wanaojiendeleza kuna namna ya kuweza kuwashughulikia ili wapate haki zao. Mimi nadhani tukikubaliana hilo basi tumekaa pazuri.

Badala ya kurudi kwenye historia na mambo mengi yametokea huko nyuma, pamoa na kinachoelekea kuwa ni uzembe wa huyu Mkurugenzi wa Songea vijijini ambaye hajibu barua kwa wakati na hilo ni jukumu lako Waziri mkisaidiana na TAMISEMI anahitaji naye kupata changamoto kidogo. Kwa sababu asingechelewesha pengine mambo haya yangekaa vizuri. Sasa tuendelee. (*Makofi*)

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru kwa kunipa nafasi. Jana wakati nachangia nilizungumzia suala zima la marupurupu ya Walimu wetu, hali kadhalika na Polisi na wafanyakazi wengine ambao wapo kwenye sekta ya umma.

Sasa wakati Mheshimiwa Waziri akitoa majumuisho hajazungumzia lolote kuhusiana na haya marupurupu hasa kwa Walimu wetu ambao limekua ni suala la muda mrefu sana. Sasa nataka anisaidie ama anieleweshe kama katika fungu la mwaka huu kuna kiasi chochote kilichotengwa mahususi kwa ajili hawa watumishi wetu ambao ni muhimu sana katika taifa letu.

**MWENYEKITI:** Nadhani Mheshimiwa Mdee unazungumzia malimbikizo ya madai ya watumishi mbalimbali; Polisi, Walimu, Waganga, Afisa Magereza labda hata na *TPDF*. Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la malimbikizo ya madeni ya watumishi naomba nizungumzie kwa watumishi wa umma. Wale wa vyombo vyaa ulinzi na usalama haswa majeshi na polisi naomba niwaachie wenzangu lakini naomba na lenyewe nilijibu. Yote hayo mengi tumeyazingatia katika Bajeti.

Mheshimiwa Rais alitoa maelekezo na tumepita tukihakiki kama Waziri wa TAMISEMI alivyofanya, tulihakiki upande wa Elimu Shule za Msingi na tulihakiki madeni ya watumishi wa Sekondari. Kwa hiyo mengi yamezingatiwa kwenye Bajeti.

**MWENYEKITI:** Nikukumbushe Mheshimiwa Halima Mdee tulivytengua Kanuni hairuhuswi kusimama zaidi ya mara moja.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002	<i>Finance and Account</i> ... ... ... Shs. 252,012,100/-
Kif. 1003	<i>Inf, Edu. and Communication</i> ... Shs. 131,220,600/-
Kif. 1004	<i>Procurement Management Unit</i> Shs.128,992,500/-
Kif. 1005	<i>Internal Audit Unit</i> ... ... ... Shs. 95,040,700/-
Kif. 1006	<i>Planning Division</i> ... ..... Shs. 264,717,600/-
Kif. 2001	<i>Policy Dev. Division</i> .... .... Shs. 483,086,900/-

*(Vifungu Vilivyotajwa Hapo Juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila ya Madaliko yoyote)*

**MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, programu ya 20. Nilipochangia jana nilitaka kujuu *Public Service Management* wana mpango gani wa hii *human resources* kuhamahama kuhamia *private sector* wengine wakaenda nchi za nje hasa madaktari na nchi yetu hivi sasa tunajua tuna upungufu wa madaktari.

Sasa tuna mpango gani wa kustawisha hali hiyo na kurekebisha ili hawa watu wanaohamahama kukimbilia nchi za jirani na *private sector* wakabaki Serikalini? Kwa sababu ya vivutio vilivyoko huko na sisi tunafanya katika wakati huu wa ushindani kuwabakisha hawa watu wetu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Serikali inajitahidi katika kuboresha maslahi ya watumishi hasa hiyo kada anayoizungumzia ya afya.

Sasa hivi nimhakikishie kwamba kwa maana ya ndani ya nchi watumishi, madaktari na manesi wanahama kutoka katika hizi hospitali binafsi, wanatoka kwenye hospitali za mashirika ya dini na sasa hivi napenda nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba wapo watumishi ambao unaona wanafanya kazi kwenye hospitali za mashirika ya dini wanalipwa mshahara wa Serikali kwa sababu vinginevyo maeneo hayo wataondoka na Serikali haina hospitali hapo ili kuwabakisha wasikimbie na huko wawepo.

Tunawasaidia na wapo Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi kwamba hospitali zao za misheni watumishi wao wanalipwa na mishahara ya Serikali kwa sababu watu wanaondoka huko. Wapo baadhi ya watumishi sasa hivi kwenda nje sio sana, isipokua tatizo tulilokuwa nalo ni kwamba vyuo vyetu vinatoa watumishi wachache kuliko mahitaji yaliyopo suala ambalo tunalifanyia kazi.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Mawaziri, nadhani kwenye Bajeti hii Serikali imeongeza pensheni kufikia 50,000 kwa mwezi si haba, maana ilipokuwa 20,000/-

ilikuwa haivutii sana. Lakini sasa hamsini, ule utulivu ule ukijua kwamba ukishatoka unahamsini zako hata lile wazo tu kwamba zitakua zinaendelea kupanda inasaidia.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2002	<i>Management Services Division</i>	Shs. 309,830,100/-
Kif. 2003	<i>Establishment Division</i> ... ....	Shs. 870,221,200/-
Kif. 2004	<i>Ethic Promotion Division</i> ... ...	Shs. 242,004,000/-

*(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Madaliko yoyote)*

Kif. 3001      *Human Resources Dev. Division* Shs. 570,643,700/-

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli si swali sana ni mawazo tu kwa Serikali kupitia Wizara hii kwamba kwa kuwa Serikali inakubali kwamba kuna haja ya kufundisha watumishi kwa wingi kile chuo cha Tabora kimelemewa. Katika Bajeti hii kuna shilingi milioni 600 kwa ajili ya matengenezo ya chuo.

Nilitoa rai kwamba kwa kuwa chuo hicho kinalipisha karo kwanini Serikali isiangalie utaratibu mwingine wa kupata fedha kwa kupitia *bonds* au mikopo kwenye taasisi za fedha kwa pamoja zikajenga na kupanua chuo kwa mara moja kuliko hii ya 600 600 kila mwaka. Katika maelezo yake Mheshimiwa Waziri hakulielezea hilo kwa hiyo naomba ufanuzi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Mbunge aliletu mapendekezo hayo na kwamba nilijibu kwamba mwaka huu tumetenda shilingi milioni kwa ajili ya chuo cha Tabora lakini wazo lake naona ni zuri sana naomba atuachie tulitafakari tuone tutakavyolishughulikia.

**MHE. BALOZI ABDI MSHANGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *program* ya 30. Ninaomba ufanuzi kwa Mheshimiwa Waziri kwamba kuna mifuko ipi, mafungu yapi, wafadhili wapi na taratibu zipyi ambazo zinasaidia kuwaendeleza watumishi wanawake?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi wanawake kama jana nilivytangaza tunapata pesa kutoka Serikali ya Ubelgiji, tunapata pesa kutoka Australia lakini pia

tunapata pesa kutoka Serikali ya Jamhuri ya Korea Kusini na nchi nyingi tu, nimezitaja kwenye kitabu cha hotuba zinaonekana.

Lakini pia tunapata pesa kutoka Benki ya Dunia kupitia maboresho ya Utumishi wa Umma. Kwa hiyo kila inapopatikana fursa tunajitahidi tunawapeleka watumishi wanawake ili kuwajengea uwezo waweze kushika nafasi za maamuzi.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 3002	<i>Tanzania Public Service College</i> Shs. 1,274,285,000/-
Kif. 3004	<i>Diversity Management Unit ...</i> Shs. 68,849,200/-
Kif. 4002	<i>Management Inf. System Division</i> Shs. 288,509,700/-
Kif. 4003	<i>Records and Archives Division ...</i> Shs. 711,298,500/-

(*Vifungu Vilivyotajwa Hapo Juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila ya Madaliko yoyote*)

### **Fungu 33 – Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi**

Kif. 1001      *Administration and General ...* Shs. 2,144,181,000/-

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyaa, Mheshimiwa Magdalena Sakaya. Mtaje *Sub-vote* mnayosimamia hapa isije ikawa suala la mshahara hapa. Kama ni mshahara umekosea kabisa kwa sababu hatuchukui mshahara wa Mwenyekiti wala Mtendaji Mkuu Sekretarieti.

**MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kwenye *program 10, sub-vote 1001* kifungu kidogo 221000 *Travelling in Country 221200 Communication and information*. Nilipochangia tulizungumza kuhusu hii Sekretarieti ya Maadili namna wanavyopata taabu na wanavyopaswa kuhangaika nchi nzima, Majimbo yote 232 waliko Wabunge na viongozi wengine kufuatilia mali zao.

Walipokuja kwangu shida waliiona, kuna sehemu gari haifiki inabidi ukodi hata punda kwenda kuwaonesha mashamba ya mikarafuu yenyenye mabonde na milima. Hakuna baiskeli hakuna chochote na hakuna farasi kwa hiyo tunakodi punda.

Sasa hii *travel* iliyooneshwa nikilinganisha na *Human Right Commission* ambao wao wana milioni 82390 ukilinganisha na *Human Rights* ambao wana milioni 187 naona ni ndogo. Na tunaposema hii *travel* in *country* hatuna maana kwamba hiyo *travel* ndiyo iondoshwe moja kwa moja. Tuna maana ziko *section* ni ndogo kuna *section* wanapangwa hela nyingi kwa hiyo nilitaka maelezo kwa Mheshimiwa Waziri inakuwaje hawa hawawezeshwi vizuri kwanini fungu hili lisiongezwe. (*Makofifi*)

La pili kifungu cha (2) *air communication information* kuna viongozi ambao hawakurejesha fomu za maadili lakini hakuna taarifa yoyote. Je, wako juu ya sheria hatua gani zimechukuwa Waziri alipofafanua hajatueleza tunaomba atufafanulie kuwa hawa wamechuliwa hatua gani ahsante.

**MWENYEKITI:** Hili la pili halihusiki hapo kabisa haya ni matumizi tu ya idara husika. Kwa hiyo, nitamwomba Waziri aweze kujibu lile la kwanza la Bajeti finyu kwa sekretarieti kuweza kukagua mali za viongozi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante napenda kumjibu Mheshimiwa Mnyaa kwamba ni kweli na sisi tunakubaliana kwamba Bajeti finyu na sote tunajua kwamba kasungura haka ni kadogo lakini Sekretarieti inajitahidi kufanya kazi zake kwa kutumia hiyo Bajeti finyu lakini hali ya fedha ikiwa nzuri wataongezewa hatuwezi tukatoa huku tukatia huku lakini ikipatikana pesa ya kutosha kidogo kidogo ataongezewa.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, programu hiyo 10 subvote 1001, nilikuwa nahitaji tu ufanuzi...

**MWENYEKITI:** Endelea, nenda zaidi sio *sub vote*, lazima uende kwenye *item* ni suala lipi nikusaidie.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia nilizungumzia suala la jinsi gani viongozi wanavyopokea maagizo ya Serikali tofauti na kutenda tofauti. Kwa hiyo naona iko kwenye *Administration in General* sasa kama inatakiwa kifungu kidogo zaidi labda iwe kwenye *Communication and Information*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia nilieleza jinsi gani ambapo Serikali inatoa maagizo na watendaji wanayapokea tofauti kinyume na yalivyotolewa na hivyo kusababisha wananchi kuteseka na saa nyingine natoa mfano wa uhamishaji wa mifugo jinsi ambavyo ulivyotolewa tofauti wananchi wameteseka wakati huo huo nikataka kujua kwamba wakati Serikali inatoa maagizo Wizara ya Utawala Bora inashirikishwa kiasi gani ili kuweza kufuutilia na kuhakikisha kwamba maagizo yalivyotolewa ndivyo yanavyotekelawa na viongozi. Nilikuwa nataka ufanuzi huo mdogo.

**MWENYEKITI:** Sijui Mheshimiwa kama anaweza kufanya subira kidogo, tukifikia Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi ili waweze kutupa majibu halisi kwenye hilo kwanza kwa sababu ndiyo mfano ulioutoa tufanye subira kidogo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts* ..... 34,170,000/=

Kif. 1003 - *Policy and Planning* ..... 313,410,000/=

Kif. 1004 - <i>Information, Education, and Communication</i> ... .....	117,090,000/=
Kif. 1005 - <i>Procurement and Management Unit</i> ... .....	56,982,000/=
Kif. 1006 - <i>Internal Audit</i> ... .....	20,920,000/=

(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)

### **Fungu 66 - Ofisi ya Rais Tume ya Mipango**

Kif. 1001 - <i>Administration and Human Resource Management Division</i> ... .....	1,886,526,000/=
Kif. 1002 - <i>Finance and Accounts</i> ... .....	445,980,000/=
Kif. 1003 - <i>Planning and Monitoring Division</i> ..... .... .....	578,699,000/=
Kif. 1004 - <i>Information Education and Communication Unit</i> ... .....	246,424,000/=
Kif. 1005 - <i>Internal Audit Unit</i> ... .....	91,104,000/=
Kif. 1006 - <i>Procurement Management Unit</i> ..	377,241,000/=
Kif. 1007 - <i>Library and Documentation Unit</i> ..	184,222,000/=
Kif. 1008 - <i>Management Information System</i>	127,228,000/=
Kif. 2001 - <i>Macro Economy Cluster</i> ... .....	858,680,000/=
Kif. 2002 - <i>Productive Sector Cluster</i> .....	881,076,000/=
Kif. 2003 - <i>Infrastructure and Services Cluster</i> ..	883,846,000/=
Kif. 2004 - <i>Social Service and Demographics Cluster</i> .....	889,023,000/=
Kif. 2005 - <i>International Trade and Economic Relation C.</i> .....	862,947,000/=
Kif. 3001 - <i>Social Service and HR. Development</i>	-
Kif. 3002 - <i>Poverty Eradication and Economic Empower</i> .....	-
Kif. 3003 - <i>Economic Empowerment</i> .....	-
Kif. 5001 - <i>Public Investment Planning</i> .....	-
Kif. 5002 <i>Growth Strategies</i> .....	-

(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)

### **Fungu 94 Ofisi ya Rais Tume ya Utumishi wa Umma**

Kif. 1001 - <i>Administration and General</i> ...	2,926,317,000/=
Kif. 2001 - <i>Civil Service</i> ... .....	1,108,634,000/=
Kif. 2002 - <i>Local Government Service</i> ... .....	444,706,200/=
Kif. 2003 - <i>Teachers' Service</i> ... .....	4,280,661,000/=
Kif. 2004 - <i>Fire and Immigration Service</i> ...	251,994,000/=
Kif. 2005 - <i>Health Service</i> ... .....	311,572,000/=

(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)

## MIPANGO YA MAENDELEO

### Fungu 30 - Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri

Kif. 1003 - *Policy and Planning* ... ... ... 47,437,672,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)

### Fungu 32 - Ofisi ya Rais Menejiment ya Utumishi wa Umma

Kif. 1001 - *Adm and Human Resources*

*Mgt Division* ... ... ..... .... 3,589,340,400/=

Kif. 1002 - *Finance and Accounts Unit* ... 130,961,800/=

Kif. 1003 - *Information, Education*

*and Communication* ... ... ..... .... 913,140,000/=

Kif. 1004 - *Procurement Management Unit*.. 240,800,000/=

Kif. 1005 - *Internal Audit Unit* ... ... ..... 15,000,000/=

Kif. 1006 - *Planning Division* ... ... ..... 897,110,000/=

Kif. 2001 - *Policy Development Devision* ... 946,150,500/=

Kif. 2002 - *Management*

*Services Devision* ... ... ..... 1,649,873,200/=

Kif. 2003 - *Establishment Division* ... 1,212,415,200/=

Kif. 2004 - *Ethic Promotion Devision* ... 523,846,800/=

Kif. 3001 - *Human Resources*

*Development Devision* ... ... ..... 2,460,200,500/=

Kif. 3002 - *Tanzania Public Service*

*College* ... ... ..... .... 1,798,516,000/=

Kif. 3004 - *Diversity Management Unit* ... 484,662,100/=

(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)

Kif. 4002 - *Management Information*

*System Division* ... ... ..... .... 2,754,175,000/=

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa mimi nilikuwa naomba ufanuzi tu, kifungu hiki ukikiangalia ukikisoma pamoja na kifungu cha ambacho tumeshakipitisha lakini ni kwa ajili ya ufanuzi cha 2002 suala ni kwamba kwa nini isiwe kimoja badala ya kuwa viwili tofauti?

**MWENYEKITI:** Sijakuelewa.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Kifungu tunachokizungumzia sasa hivi Mwenyekiti cha *Management Information System Division* ukikisoma kwa pamoja na kifungu cha 2002 *Management Services Division* na uliza kwanini vimewekwa viwili tofauti na sio kimoja?

**MWENYEKITI:** Kwanza havisomeki sawa lakini sijui kwanini unataka vichanganywe.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mantiki ni ile ile labda Wizara ituambie kwanini viko tofauti, maana yake masuala ya *Management Information System* na *Management Services Division*...

**MWENYEKITI:** Ni tofauti.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi nakubaliana na wewe.

**MWENYEKITI:** *Management Services* ni kitu tofauti kabisa hata idara.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Ahsante.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 4003 - *Records and Archives Division* 3,138,687,5000/=

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote*)

### **Fungu 33 - Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi**

Kif. 1001 - *Administration and General* ... 500,000,000/=

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote*)

### **Fungu 66 - Ofisi ya Rais Tume ya Mipango**

Kif. 1001 - *Admn. and HR Management Division* 146,000,000/=

Kif. 1003 - *Planning and Monitoring Division* -

Kif. 1004 - *Info. Education and Comm. Unit* -

Kif. 2001 - *Macro Economy Cluster* ..... -

Kif. 2002 - *Productive Sector Cluster* ..... -

Kif. 2004 - *Social Service and*

*Demographics Cluster* ..... 98,567,000/=

Kif. 3001 - *Social Service and HR. Development* ... -

(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)

### **Fungu 94 - Ofisi ya Rais Tume ya Utumishi wa Umma**

Kif. 1001 - *Administration and General ... ... 696,568,000/=*

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)

(*Bunge lilirudia*)

### **T A A R I F A**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, kabla sijatoa hoja naomba kumtambua Mheshimiwa Bujiku Sakila alichangia kimaandishi, kwa bahati mbaya tulikuwa hatujamtaja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imepitia Makadirio ya Bajeti ya Ofisi ya Rais kwa mwaka wa fedha 2009/2010 kifungu kwa kifungu bila ya mabadiliko yoyote.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:**  
Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)  
(*Hoja ili amuliwa na Kuafikiwa*)

(*Makadiro ya Matumizi ya Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora yalipitishwa na Bunge*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja iliyombele yetu ni kukubali kuyapitisha Makadirio ya Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na pia Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2009/2010 Waziri Utawala ameitoa hoja na imeungwa mkono. Sasa kwa mujibu wa Kanuni nitawahoji kupitisha makadirio haya.

Naona ni Mheshimiwa Mercy tu ndiye amesema hapa kwa hiyo naye kwa jinsi alivyoinama naona anaona aibu. Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba Makadirio ya Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na pia eneo la Utawala Bora yamepitishwa Rasmi na Bunge letu hivi leo tarehe 27 Juni, 2009. (*Makofi*)

Nawapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa mchango wenu na shukrani maalum kwa wale ambao wanahoji kwa sababu mambo haya hayatakiwi yapite pite tu bila sisi kuelewa. Lakini pia nawashukuru

Waheshimiwa Mawaziri kwa ufanuzi mzuri sana ambao umetuweka sote pamoja, ahsante sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa ni matangazo machache. Mheshimiwa Estherina Kilasi, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya *POAC* anaomba wajumbe wote wa Kamati wa Hesabu za Mashirika ya Umma wawe na mkutano mfupi sana Ukumbi Namba 227 mara baada ya Kuahirisha Bunge.

Mheshimiwa Mohamed Rajab, *Assistant Coach* wa timu yetu ya Bunge *Sport Club* anatangaza kwamba leo zile mechi za mpira wa miguu *football* na pia *netball* zipo mechi zote mbili kati ya Waheshimiwa Wabunge na madaktari wa hospitali ya Mirembe, saa kumi jioni pale uwanja wa Jamhuri, Dodoma. Nadhani pamoja na wauguzi.

Sasa naomba Mwenyekiti wetu wa *Bunge Sports Club* Mheshimiwa Bendera achukue tahadhari zote na marefa wa leo isije ikawa hawa wenzetu Mirembe wakaingiza mamluki wale wa aina nyingine wale. Hatupendi Waheshimiwa Wabunge muumie. Kwa hiyo, hakikisheni muone vitambulisho kwamba ni madaktari na wauguzi peke yao, wale wengine hapana. (*Kicheko/Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge baada ya maeleozo hayo nakutakie *weekend* njema. Nawashukuru sana mwanzo wetu huu kazi za Jumamosi zimeanza vizuri. Kwa hiyo, sasa naliahirisha Bunge hadi hapo siku ya Jumatatu, tarehe 29 Juni, 2009 saa tatu asubuhi ndani ya ukumbi huu wa Bunge.

(*Saa 5.47 Mchana Bunge liliahirishwa Mpaka  
siku ya Jumatatu, tarehe 29 Juni, 2009 saa tatu Asubuhi*)